# Nipashe

Jumatano Machi 25, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580188

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Ajali ilivyoua 5 daraja lililobomoka Morogoro

UKURASA 4




UKURASA 13

**TISHIO CORONA**

# Utata wajitokeza gharama karantini

**WALIOPELEKWA** hotelini wakimbia bei kubwa, waziri aagiza ma-DC kutafuta hoteli za gharama nafuu, waajiri waonywa kupunguza wafanyakazi... *Endelea ukurasa 2 &3*



Rais John Magufuli, akipimwa joto la mwili kabla ya kuingia ukumbini, kuongoza kikao cha Baraza la Mawaziri, Chamwino, Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Mahakama sasa kutopokea kesi zisizokamilisha upelelezi

UKURASA 4



## BAA LA CORONA

IDADI ya wagonjwa wa virusi vya corona katika nchi za Afrika Mashariki za Uganda na Rwanda imeongezeka, Uganda ikiwa na wagonjwa wanane na Rwanda 17, huku Afrika Kusini ikirekodi maambukizo kwa watu 402 hadi jana mchana. Chukua tahadhari!

- **Epuka mikusanyiko ya watu**
- **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
- **Epuka kusalimiana na kushika mikono na kukumbatiana**
- **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**

## SERIKALI YAMWAGA AJIRA 610 MADAKTARI

UKURASA 4




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


**MICHEZO** **SADNEY, BALINYA WAISHTUA YANGA** UK. 32

**MAONI, KATUNI UK.6**

## TISHIO CORONA



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Masanja Kadogosa, akiongoza waombolezaji kutoa heshima za mwisho kwa waliokuwa wafanyakazi wa shirika hilo, waliofariki dunia katika ajali wakati wa kuwaaga kwenye Hospitali ya Lugalo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Utata wajitokeza gharama karantini

**Na Waandishi Wetu**

UTATA umeibuka kwa wasafiri kutoka nchi mbalimbali zenye maambukizo ya homa ya mapafu inayotokana na virusi vya corona (COVID-19), kushindwa kumudu hoteli walizopelekwa baada ya kuingia nchini.

Jana, ilisambaa video kwenye mitandao ya kijamii, ikionyesha wasafiri zaidi ya 10 waliokuwa wakilalamika kuhusu gharama za hoteli walizopangwa na kwamba hakuna utaratibu maalum wa kuwahifadhi huku wakichanganyikana na watu wengine.

Vilevile, haijajulikana walikokwenda wageni hao baada ya uongozi wa hoteli walikopelekwa, kugoma kuwapokea na wenyewe kushindwa kumudu gharama hizo, huku usafiri uliotumika kuwapeleka hotelini kutoka uwanja wa ndege ukiondolewa eneo hilo la hoteli.

Katika video hiyo, mwanamke mmoja ambaye hakufahamika jina lake, alisema kuwa baada ya kufika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam, walipangwa kukaa kwenye hoteli ambazo gharama zake ni za kuanzia Dola za Marekani 55 kwa siku.

"Tulivyofika, tuliwaambia tukae nyumbani na tuwe tunakaguliwa, lakini kukawa na mabishano ya maneno ya kukaa hotelini tutakuwa tunakuja kukaguliwa wakaikataa, wakasema watatupeleka hotelini," alidai.

Alizitaja hoteli walizotakiwa kwenda kuwa ni pamoja na Peacock, Rungwe, Southern Sun, Dar City Palace, Hot Reef na Lucky.

"Hizi ni hoteli ghali sana Mheshimiwa Rais, Waziri Mkuu na Waziri Ummy, hatuwezi kulipia kwa siku 14 na mnavyotuona tumebwagwa na hakuna mtendaji yeyote wa Wizara ya Afya na tayari tumekuwa hatarishi kwa watu tuliowakuta," alisema dada huyo huku akiungwa mkono na wenzake.

Waliiomba serikali kuwasaidia kwa kuwa hoteli hizo ni ghali na bei zinaanzia Dola za Marekani 55 (Sh. 126,800), 78 (Sh. 179,800), 83 (Sh.191,400) na 105 (Sh. 242,100), huku kila hoteli ikiwa na kiwango chake cha kubadilishia dola kwa shilingi ya Tanzania.

Katika ukurasa wake wa Twiter jana, Waziri Ummy Mwalimu, aliandika huku akiambatanisha na video ya mwanamke huyo akilalamikia juu ya mahali pa kuhifadhiwa.

Waziri Ummy aliandika: "Tumepokea hii changamoto ya sehemu zilizobainishwa kwa ajili ya siku 14 za kijitenga kwa wasafiri waliotoka nchi zilizoathirika zaidi na COVID-19.

"Nawaelekeza Ma-RC (wakuu wa mikoa), RAS (Katibu Tawala wa Mkoa) na DC (wakuu wa wilaya) zote kubainisha hoteli/sehemu ambazo wasafiri wengi watamudu gharama."

Nipashe iliutafuta uongozi wa Hotel ya Peacock na kuongea na Joel Mfugale, ambaye alikiri watu hao walifika hotelini kwao juzi na walivyowakataa, waliondoka na hawajui walikokwenda.

"Mkuu wa Wilaya alitangaza kuwa hoteli yetu ni moja ya hoteli itakayopokea watu hao, lakini sisi tulikataa kwa kuwa kwa wiki mbili inatakiwa hoteli isiwe na wageni wengine na wawapo madaktari au wataalamu wa afya, tulishindwa kuelewana," alisema na kufafanua zaidi:

"Kuhusu bei kubwa, ilikuwa ni mpango wa mameneja ili tusiwapokee watu hao kutokana na kwamba hakuna maandalizi yoyote, na walivyoona hatuwapokei na waliowaleta (serikali) wameondoka, basi nao waliondoka na hatujui walielekea wapi.

"Sisi tuna wageni wengine, haiwezekani tukawa 'quarantine' (eneo la kujitenga) tutawahudumiaje wateja wetu? Na pia hakuna elimu yoyote iliyotolewa, ni ngumu na hatari sana kwetu kutunza watu hao."

Katika hatua nyingine, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, amesema wamefanya vipimo mara ya pili kwa mgonjwa wa kwanza wa COVID-19 yaliyoonesha hana maambukizi.

Aidha, amesema wanasubiri kumfanyia vipimo mara ya tatu na ya mwisho wakati wagonjwa wengine 12 waliokuwa wakihisiwa kuwa na maambukizi hayo kukutwa hawana virusi vya corona.

***Imeandikwa na Salome Kitomari na Mary Geofrey***

# Kariakoo ilivyo hatarini kupata maambukizi

**Na Romana Mallya**

AGIZO la serikali la kuwataka wafanyabiashara kuweka maji na vitakasa mikono kwenye maeneo ya biashara zao, baadhi ya wafanyabiashara eneo la Kariakoo wameonekana kupuuza agizo hilo ambalo lina lengo la kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona.

Nipashe ilishuhudia baadhi ya maduka sokoni humo yanayotembelewa na mamia ya watu yakiwa hayana ndoo zenye majisafi yenye mabomba ya kuyatiririsha, sabuni za maji na vitakasa mikono.

Wakizungumza na mwandishi wa habari hizi kwa nyakati tofauti, wafanyabiashara hao walisema hawajaweka vifaa hivyo kwa sababu vinauzwa ghali.

Hussein Mjema ni mfanyabiashara wa vyombo vya nyumbani anayeuza eneo la Soko Kuu Kariakoo ambaye alisema kuwa hawajaweka vifaa hivyo kwa sababu hawajaelimishwa.

"Jumamosi na Jumapili nimeambiwa na wenzangu kuwa magari ya manispaa yalipita kutoa elimu ya matumizi ya vitakasa mikono au sabuni za maji na maji yanayotiririka.

"Baada ya wenzangu kunielimisha ndiyo tupo kwenye harakati ya kutafuta fedha ili kununua vifaa hivyo kwa ajili ya kujikinga sisi na wateja wetu."

Muuza urembo sokoni hapo, Elia Jackson alisema elimu ya corona ameipata, lakini changamoto inayowakabili wafanyabiashara wadogo ni gharama ya vifaa hivyo.

Uchunguzi uliofanywa na gazeti hili ulibaini ndoo maalumu ya kunawia mikono inauzwa kati ya Sh. 10,000 hadi 20,000, sabuni za maji zinauzwa kati ya Sh. 3,500 hadi 4,500 sokoni hapo.

Jackson alijitetea kuwa bei ya vitakasa mikono ni kubwa ndiyo maana asilimia kubwa ya wafanyabiashara hawajaweka.

"Sisi wafanyabiashara wadogo tunashindwa kuweka kwa sababu ukitazama misingi yetu ni midogo," alisema.

Gazeti hili liliutafuta uongozi wa Soko Kuu la Kariakoo na kufanikiwa kuzungumza Meneja wa soko Donald Sokoni, ambaye alisema utaratibu waliouweka ni kutoa elimu kwa wafanyabiashara wanaozunguka soko hilo ili kila mmoja awajibike kuweka vifaa hivyo.

"Tangu serikali itoe maagizo kuhusu virusi vya corona na kutaka maeneo yenye mikusanyiko yote yachukue tahadhari ikiwa ni pamoja na kuweka vifaa vya kunawia mikono, uongozi wa soko umefanya hivyo.

"Kutokana na gharama ya vitakasa mikono kuwa juu, tulipata ushauri kutoka ofisi ya Mganga Mkuu Halmashauri ya Manispaa ya Ilala ambao walituelekeza tuchukue kidonge viwili vya chlorine ambavyo tunavichanganya kwenye ndoo ya maji ya lita 20 na kupata mchanganyiko wa kitakasa mikono."

Alisema kwa siku soko hilo limekuwa likitumia ndoo 15 zenye mchanganyiko huo zinazowekwa kwenye milango 12 ya kuingilia ambazo hutumika kuwanawisha watu wanaoingia na kutoka ndani ya soko hilo ikiwamo shimoni.

"Tunawashauri wafanyabiashara sokoni hapa ambao mpaka sasa hawajaweka vifaa vya kunawia kwenye maeneo yao wafanye hivyo ili kutoruhusu ugonjwa huu kusambaa zaidi," alisema.

Alisema kama bei ya vitakasa mikono ni kubwa, wanaweza kutumia mchanganyiko huo wa kidonge cha chloride au sabuni ya kawaida ya maji.

Pia alitaja changamoto nyingine ni baadhi ya watu ambao hawana makazi kulala sokoni hapo ambao wengine huwa ni wagonjwa.

"Kumekuwa na changamoto hii, kwa mwaka jana pekee walikuwa kama wanne, watu wa aina hii tunawataka wachukue tahadhari kwa maana akipata mmoja maambukizi ni rahisi kuambukiza wengi.

"Wanalala hapa na wengine wanazidiwa wanakuja kuomba msaada ukimuuliza vipi anakwambia siwezi kutembea, tunaangalia hali yake ikoje tukiona imezidi sana tunatoa taarifa Polisi na baadaye anapelekwa hospitali, wengine unakuja unakuta wamekufa usiku."

TISHIO CORONA

# TPSF: Tusitumie corona kupunguza wafanyakazi

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), imeasa wanachama wa taasisi hiyo wasitumie ugonjwa wa corona kupunguza wafanyakazi katika viwanda au kampuni wanazozimiliki.

Mwenyekiti wa Taasisi hiyo, Angelina

Ngalula, ndiye aliyetoa angalizo hilo alipokuwa akizungumza na wanahabari jana jijini Dar es Salaam, kwa kusema kwamba Tanzania na dunia kwa jumla zinapita katika kipindi kigumu kutokana na ugonjwa wa corona.

Hata hivyo, alisema kuwa siyo busara kutumia tatizo hilo kupunguza wafanyakazi.

"Kupunguza wafanyakazi litakuwa ni tatizo kubwa kwa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla. Hivyo nawaomba waajiri kote nchini tushughulikie changamoto zilizopo kwa pamoja ili kulinda ajira nchini. Kutumia matatizo kujinufaisha siyo utamaduni wa Watanzania," alisisitiza Ngalula.

Alisema kongani, mfano utalii na kilimo, ambazo zimeathirika moja kwa moja kutokana na ugonjwa wa corona zikusanywe taarifa zinazoonyesha namna mtu mmoja mmoja alivyoathirika na taarifa hizo ziwasilishwe kwenye kikosi kazi ambacho kimeshaundwa.

"Taarifa hizo zitachambuliwa na wataalamu wetu na kufikishwa serikalini. Msitengeneza makundi yenye lengo la kujinufaisha," alieleza Ngalula na kuongeza kwamba jambo muhimu ni kuendelea kufanya kazi kama ambavyo Rais John Magufuli amewaomba Watanzania.

"TPSF tutaendelea kuunga mkono jitihada za serikali za kufanya kazi na kuongeza tija kwa taifa, lakini lazima kuchukua hatua zinazofaa katika maeneo ya kazi ili kuwalinda wafanyakazi wasipate maambukizi ya virusi vya corona," alisema.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), Dk. Aggrey Mlimuka, alisema huu si wakati mwafaka kwa watu kufungiwa ndani kwani athari zake zitakuwa kubwa kwenye ajira na uchumi wa nchi utaporomoka.

"Zipo nchi zimefunga ofisi zote za umma na binafsi kukabiliana na ugonjwa wa corona. Sisi kama Chama cha Waajiri tunaunga mkono kauli ya Rais John Magufuli inayowataka Watanzania kuendelea kufanya kazi, huku tahadhari za kukabiliana na corona zikiendelea kuchukuliwa," alisema Dk. Mlimuka na kuiomba serikali kuondoa baadhi ya tozo kwa taasisi au kampuni zitakazoathiriwa na ugonjwa wa corona.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Biashara (TNBC), Dk. Godwill Wanga, aliwataka wafanyabiashara kuacha ubinafsi na kufikiria maslahi mapana ya nchi badala ya kutumia matatizo ya corona kujinufaisha.

"Wote tunafahamu kwamba dunia nzima inapambana na virusi vya corona. Tanzania bado hali haijawa mbaya sana na tunaomba tusiathirike zaidi," alisema na kuongeza:

Kutumia janga la corona kupunguza ajira ni kuhatarisha uchumi wetu. Tuwe wawazi na kuelekeza changamoto zetu katika maeneo husika ili kunusuru uchumi."

# Tatoa wachangishana kukabili corona mipakani

**Na Mwandishi Wetu**

**"Tumekabidhi vifaa hivi kwa TPSF ili iwezekukabidhi vifaa Ofisi ya Waziri Mkuu mapema wiki ijayo," alisema Lukumai na kuongeza kuwa wametoa siku tatu zaidi kwa wanachama wao kuendelea kuchangia vifaa hivyo muhimu.**

WANACHAMA wa Chama cha Wamiliki wa Malori Tanzania (TATOA) kupitia kampuni zao binafsi, wamechangishia vifaa vya kusafisha mikononi maji ya sanitizer kwa ajili ya kusambazwa kwenye maeneo ya mipaka na nchi jirani.

Akizungumza jijini Dar es Salaam wakati akikabidhi vifaa hivyo kwa Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Angelina Ngalula, Makamu Mwenyekiti wa Tatoa, Elias Lukumai, amesema Tatoa ambayo ni miongoni mwa kongani 14 za TPSF wamejitolea kuchangia vifaa hivyo ili kuchangia jitihada za serikali kuzuia maambukizi ya ugonjwa nchini.

"Tumekabidhi vifaa hivi kwa TPSF ili iwezekukabidhi vifaa Ofisi ya Waziri Mkuu mapema wiki ijayo," alisema Lukumai na kuongeza kuwa wametoa siku tatu zaidi kwa wanachama wao kuendelea kuchangia vifaa hivyo muhimu.

Alisema vifaa hivyo vitasambazwa kwenye maeneo ya mipaka ya Tunduma, Rusumo, Kasumulo na Kabanga na kuwaomba wanachama kuendelea kuonyesha uzalendo na upendo kwa kuchangia vifaa ili visaidie kuzuia maambukizi yasienee zaidi.

"Elimu imeendelea kutolewa kwa madereva wetu wanaosafiri nje ya mipaka umuhimu wa kujikinga na maambukizi ya corona. Hata hivyo, mpaka sasa ninafurahi kusema kuwa hana dereva aliyepata maambukizi," alisema.

Ngalula mbali ya kuishukuru Tatoa kwa mchango wake wa vifaa, alirudia tena wito wake kwa kongani zingine ndani ya TPSF kuendelea kujichangisha na pia kuiga mfano wa Tatoa.

"TPSF tumejielekeza zaidi katika mambo makuu matatu ambayo ni kutoa elimu zaidi kuhusu maambukizi ya ugonjwa huu kwa muongozo na maelekezo ya serikali kupitia Wizara ya Afya," alisema.

Alisema wataendelea kuhamasisha zaidi upatikanaji wa rasilimali vitu kutoka kwa wanachama wake ili kuchangia juhudi zinazofanywa na serikali..

Naye Mjumbe wa Tatoa, Saad Ismail, aliwahamasisha wamiliki wa malori kuendelea kuchangia vifaa na kusema kuwa mpaka sasa kuna malori zaidi ya 20,000 ambayo yanafanya kazi.

"Kila mwanachama wa Tatoa ni lazima achukue hatua ya kuchangia kwani janga hili ni kubwa na vizuri tukachukua hatua za kujikinga mapema," alisema.


IITA Transforming African Agriculture 50 1967 - 2017

**POSITION ANNOUNCEMENT**

**COMMUNICATION ASSISTANT**

**IITA-TZ2020-CRS-003-NRS-DSM**

**Background:**

The International Institute of Tropical Agriculture (IITA) invites applications for the position of Communication Assistant.

The International Institute of Tropical Agriculture (IITA) is a member of a world-wide network of International Agricultural Research Centers. IITA's research focuses on smallholder cropping systems in sub-Saharan Africa. IITA has a regional hub in Dar es Salaam, Tanzania which co-ordinates the work of the institute in East Africa.

**Duty Station:**

This is a Nationally Recruited Position and the incumbent will be based in Dar es Salaam, Tanzania

**Responsibilities:**

- Document and communicate news, updates and stories from various projects for wider dissemination and contribute to the various IITA communications tools including blog, web and bulletin.
- Monitor and archive stories in the print and news media in Tanzania that cite IITA.
- Provide editorial and communication support and documentation of project activities.
- Support the production and dissemination of communication materials on IITA" s technologies and success stories through writing features, press releases, production of books, training manuals, posters etc.
- Support planning and implementing information campaigns organized to promote IITA's generated findings and knowledge as needed.
- Contribute to the dissemination of knowledge and experiences of the project through participation in related events such as field visits, training and workshops.
- Perform any other activities as may be assigned by the Regional Corporate Communications Officer, Eastern Africa.

**Qualification and Experience**

Bachelor's Degree in Communication with at least 3 years' experience or a Post Graduate Diploma in Communications or Journalism or a related field from a recognized university.

**Skills:**

- Ability to conceptualize, design and implement communication campaigns, strategies and programs.
- Very good knowledge of oral and written English.
- Communication and facilitation 'generalist' – editing, writing, policy communication, community engagement, Internet tools and skills, information management, process facilitation, reporting and administration.
- Experience in working with different national media.
- Excellent knowledge of modern communication tools and approaches, and solid experience in knowledge management, including ICT and web 2.0 tools applications like wiki, Flickr, slideshare, Yammer, Youtube, Dropbox and blogging.
- Self-starter able to work on agreed priorities and deliverables.
- Excellent interpersonal and networking skills in an international environment.
- Good knowledge of the agricultural development scene.

**General information:**

The initial contract for the position is for two years: renewable subject to performance and availability of funds. The duty station for the position will be IITA in Dar es salaam. This is a nationally recruited position and IITA offers a competitive remuneration package.

**Applications:**

Applications including curriculum vitae, copies of certificates, telephone number, email address, and names and addresses of two referees should be sent to the Country Representative, IITA-Tanzania, Plot No. 25, Mwenge – Coca-Cola Road, Mikocheni Industrial Area P.O. Box 34441, Dar es Salaam, Tanzania or by email to IITA-Tanzania@cgiar.org

Applicants are requested to please indicate the reference number for the position as indicated on the heading of the announcement in your application as well as on the subject of your email if sending by email. If sending by post or hand delivery, please indicate the reference number on your application as well as on the left-hand side of your envelope.

**Please note that any applications without the reference indicated will be automatically disqualified.**

115678902

Closing date: Two weeks from the date of advertisement appearing in the newspaper.

Please note that only shortlisted candidates will be contacted.

# Mahakama sasa kutopokea kesi zisizokamilisha upelelezi

**Na Hellen Mwango**

MAHAKIMU wa Mahakama ya Hakimu Mkazi na Wilaya nchini, wameagizwa kuzingatia maelekezo ya tangazo la serikali namba 296 la mwaka 2002 linaloeleza kesi zote zilizokamilika upelelezi zipokelewe mahakamani na kuanza kusikilizwa mara moja.

Kadhalika, kesi ambazo upelelezi wake haujakamilika wasizipokee wazingatie tangazo hilo kufuatia agizo la serikali kuzuia mkusanyiko kupunguza maambukizi ya ugonjwa wa corona.

Rai hiyo ilitolewa jana jijini Dar es Salaam na Jaji Kiongozi wa Mahakama ya Tanzania, Dk. Eliezer Feleshi, katika mkutano wake na waandishi wa habari, kuhusu mhimili huo unavyounga mkono juhudi za serikali.

"Imefika wakati sasa mahakimu wafawidhi wa Mahakama za Hakimu Mkazi na Wilaya wafanye kazi kwa kuzingatia tangazo hilo na kama kesi upelelezi haujakamilika, basi ziishie hukohuko na si kupelekwa mahakamani kufuatia agizo la serikali kutoka kwa Rais Dk. John Magufuli, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na Waziri wa Afya, Jinsia na Watoto, Ummy Mwalimu," alisema Jaji Kiongozi.

Alisema mahakama imeongeza kasi ya matumizi ya mifumo hiyo kwa kanda ya Dar es Salaam kwa kesi zote za jinai zinazoahirishwa kutokana na sababu mbalimbali, watuhumiwa waliopo katika Gereza la Keko na Segerea watasikiliza, yataendelea kuahirishwa kwa njia ya Mahakama Mtandao (Video Conference) ili kuepuka msongamano na mkusanyiko wa mahabusu na wafungwa mahakamani.

Pia, alisema Kanda ya Mbeya na Bukoba zina vifaa vya mahakama mtandao, utaratibu unakamilishwa kwa uwekaji wa vifaa hivyo katika Magereza yaliyopo katika kanda hizo ili huduma hiyo ianze mara moja.

"Juhudi za kuweka vifaa hivyo kwa kanda zingine zilizosalia zinaendelea na baada ya muda mfupi huduma kama hizo zitatolewa, utumiaji wa mfumo wa usajili wa kesi kwa njia 'E-Filing' (kielektroniki). Mahakama inaimarisha na kuwasisitiza wadau wote (wananchi, mawakili wa serikali na mawakili wa kujitegemea) kusajili kesi kwa njia hii ya mitandao ili kupunguza msongamano na mchanganyiko wa watu katika maeneo ya mahakama," alisema Jaji Kiongozi, Dk. Feleshi.

Alisema muhimili huo utaongeza wigo wa matumizi ya Tehama kwa njia ya barua pepe na simu za mkononi kwa kutumia mfumo wa 'SMS notification' na 'USSD' katika usambazaji na upatikanaji wa taarifa za mashauri ambao hautawalazimu wadaiwa kufika mahakamani kupata taarifa hizo.

Mahakama itakuwa ikiendesha programu ya elimu ya namna ya kusajili mashauri, kupata taarifa pamoja na kutoa msaada wa usajili wa kesi kwa njia ya kielektroniki kwa kuanza na mahakama zenye kesi nyingi ambazo zinaweza kusababisha mkusanyiko wa watu wengi.

Naye Jaji Mfawidhi wa Kanda ya Dar es Salaam, Lameck Mlacha, alisema wanatumia Mahakama Mtandao kwa lengo la kupunguza maambukizi ya corona.

Vile vile, ameshawaagiza mahakimu kupunguza idadi ya watu wakati wa usikilizwaji kesi katika vyumba vya mahakama na badala yake zitumike kumbi za wazi.




Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Dk. Eliezer Feleshi, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu mahakama hiyo, kufanya kazi kwa kutumia mfumo wa Tehama ili kuepuka msongamano , ili kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa Corona. Kushoto ni Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, Lameck Mlacha. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ajali ilivyoua watano daraja lililobomoka

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

JESHI la Polisi mkoani Morogoro linamsaka dereva Saidi Kifaila (30), anayedaiwa kutoweka baada ya gari alilokuwa anaendesha kusababisha ajali kwa kugonga magari matatu, likiwamo aina ya Noah, lililotumbukia korongoni na kusababisha vifo vya watu watano na kujeruhiwa wengine sita katika la Daraja la Kiyegeya wilayani Kilosa.

Katika ajali hiyo, gari hilo aina ya Noah lenye namba za usajili T 403 DQP, lililokuwa linaendeshwa na Ramadhan Mohamed (28), lilisimama katika mteremko na magari mengine yaliyokuwa yakitokea Dar es Salaam na Morogoro kusubiri zamu yao kupita kwenye daraja hilo la mchepuko katika Barabara Kuu ya Morogoro- Dodoma.

Imedaiwa na Jeshi la Polisi kwamba, Kifaila alikuwa akiendesha gari kubwa la mizigo aina ya FAW lenye namba za usajili T 623 DGY lenye tela T 233 BXZ, mali ya Kampuni ya Road Stell Haulage na alikuwa akitoka Dar es Salaam kwenda Dodoma.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa huo, Wilbroad Mutafungwa, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo, akibainisha kuwa ilitokea Machi 22 mwaka huu majira ya saa 12 na nusu jioni maeneo ya Daraja la Kiyegeya katika Mto Mkange, tarafa ya Magole wilayani Kilosa.

Alidai dereva huyo, akiwa na gari hilo akitoka Dar es Salaam kwenda Dodoma, alipofika eneo hilo la daraja, breki za gari zilishindwa kuhimili na kukosa uelekeo na hivyo kuyapita magari ya mbele yake upande wa kushoto na hatimaye kuyagonga kwa nyuma magari matatu likiwamo aina ya Noah lililokuwa na abiria.

Alisema watu wanne waliokuwa kwenye Noah wakitoka Dumila kwenda Gairo, walifariki dunia papo hapo na mmoja alifariki dunia wakati akipatiwa matibabu kwenye Kituo cha Afya cha St. Joseph Dumila na kwamba miili yao imehifadhiwa chumba cha maiti katika kituo hicho ikisubiri utambuzi wa ndugu.

Aliwataja waliofariki kwenye gari aina ya Noah kuwa ni Sijaona Chamene (29), mkulima na mkazi wa Kijiji cha Majawanga wilayani, Mahungo Martine (25), mkazi wa Gairo na wengine watatu ambao majina yao yalikuwa hayajatambuliwa, mmoja wao akiwa ni mwanamke.

Waliojeruhiwa kwenye Noah ni dereva Ramadhan Mohamed, mkazi wa Dumila, Eliwahad Mshana (28), mkazi wa Dumila, Mkoa Michael (25), mkulima na mkazi wa Gairo , Elimalek Msigula (28) na Neema Braiton (27), wote wakazi wa Pandambili wilayani Kongwa mkoani Dodoma.

Kamanda Mutafungwa alisema majeruhi walikuwa kwenye hali mbaya na waliwahishwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro kwa ajili ya matibabu zaidi.

Alisema mbali na kuparamia Noah, lori hilo pia liliyagonga magari mengine matatu yenye namba za usajili T 611 DHE aina ya Brevis, lililokuwa linaendeshwa na Makuka Robert (36), mkazi wa Manispaa ya Morogoro na gari lenye namba za usajili T 826 DCF Toyota Harrier, lililokuwa linaendeshwa na Manoro Martin (41), Mhasibu wa Utumishi na mkazi wa Dar es Salaam.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro, Dk. Rita Lyamuya , alithibitisha kupokea majeruhi sita na kusema kuwa hali zao kiafya zilikuwa zinaendelea kuimarika baada ya kupatiwa matibabu.

# Serikali yamwaga ajira 610 madaktari

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SERIKALI imetangaza ajira za madaktari 610 ili kujaza nafasi kwenye hospitali za Halmashauri na vituo vya afya nchini.

Hatua hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa ahadi ya Rais John Magufuli aliyoitoa Februari mwaka huu jijini Dar es Salaam wakati wa maadhimisho ya Siku ya Madaktari Duniani, ya kutoa ajira mpya kwa madaktari 1,000 nchini.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Joseph Nyamhanga, madaktari watakaoajiriwa ni wa binadamu na meno waliohitimu katika vyuo mbalimbali vya Elimu ya Juu vinavyotambulika na serikali.

"Tamisemi imepata kibali cha kuajiri kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa madaktari na wataanza leo(jana) kuwasilisha maombi yao na waombaji wawe tayari kufanya kazi Halmashauri yoyote watakayopangiwa," alisema.

Aliongeza: "Maombi yote yatumwe kwa njia ya mtandao (online) kupitia mfumo wa kielektroniki unaopatikana kupitia anuani ya ajira.tamisemi.go.tz. na maombi yoyote yatakayowasilishwa kwa njia ya posta au kuletwa moja kwa moja ofisini hayatafanyiwa kazi."

Alisema mwisho wa kupokea maombi ni Aprili, 10 mwaka 2020 saa 9:30 alasiri.

Akizungumza katika mkutano wa madaktari pamoja na watumishi wa sekta ya afya uliofanyika katika ukumbi wa kimataifa wa mikutano wa Julius Nyerere (JNICC), jijini Dar es Salaam, Rais Magufuli alisema anafahamu kuna madaktari takribani 2,700 hawajaajiriwa.

"Nitalifanyia kazi. Nafikiri tunaweza tukaanza polepole hata tukachukua 1,000 eti Waziri wa Utumishi (George Mkuchika) hatuwezi kuajiri hata 1000, hela si zipo kidogo? Basi tuajiri 1,000 madaktari, tuanze na 1,000 mambo yakiwa mazuri tena tunaajiri wengine kwa sababu tunahitaji madaktari mpaka vijijini," alisema.

HABARI KITAIFA

# Anayedaiwa kubaka mtoto asomewa mashtaka matano

**Na Pendo Thomas, KIGOMA**

MAHAKAMA ya Wilaya ya Kigoma, imeanza kumsomea maelezo ya awali mshtakiwa Jeremia Kirahunja (49), anayekabiliwa na makosa matano ya kubaka mtoto wa miaka sita kwa miaka mitano mfululizo.

Mshtakiwa huyo anakabiliwa na makosa matano ya ubakaji kesi namba 19 ya mwaka 2020 kosa alilolitenda kwa nyakati tofauti na maeneo tofauti dhidi ya mtoto huyo.

Akisoma maelezo ya awali ya makosa hayo, Wakili wa Serikali, Reymond Kimbe, mbele ya hakimu wa mahakama hiyo, Kitalo Mwakitalu, alisema mshtakiwa alitekeleza makosa hayo katika eneo la Airport mara mbili na Katubuka mara tatu, tangu mtoto huyo akiwa darasa la kwanza hadi darasa la tano alipofikisha miaka 10 baada ya mzazi wake kubaini.

Wakili Kimbe alisema kosa hilo ni kinyume na kifungu cha 130 kifungu kidogo cha kwanza na cha pili (e) na kifungu cha 131 kifungu kidogo cha tatu cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 marejeo ya mwaka 2002.

Mshtakiwa aliposomewa makosa yake, alikana na kesi hiyo imepangwa kusikilizwa tena Aprili 9.




Madereva wa Bajaj wa Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam, wakiwa wameweka pipa la maji yenye dawa kijiweni kwao, ili kila abiria anayetaka usafiri anawe kwanza kabla ya kuanza safari kama njia ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Walia ubovu barabara kwenda Msumbiji, TCCIA yaingilia kati

**Na Mwandishi Wetu, SONGEA**

WAFANYABIASHARA wilayani Songea mkoani Ruvuma, wamelalamika kuhusu ubovu wa barabara inayounganisha mkoa huo na nchi jirani ya Msumbiji, wakisema imeathiri shughuli zao za kibiashara.

Kijiografia, Mkoa wa Ruvuma ambao ni miongoni mwa mikoa vinara kwa uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara nchini, unapakana na nchi za Msumbiji na Malawi kupitia mipaka ya Mkenda na Bambabei.

"Barabara kutoka Manispaa ya Songea mpaka mpakani Mkenda yenye urefu wa kilometa 124 ni mbovu na haipitiki hususani wakati wa mvua. Kipindi hiki cha mvua, shughuli za kibiashara zimedolola," alisema Samson Swedi, mfanyabiashara wa mahindi kutoka Songea wakati wa mkutano na maofisa kutoka Chemba ya Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo (TCCIA) uliofanyika jana wilayani Songea.

Mfanyabiashara huyo ambaye aliwawakilisha wafanyabiashara wenzake kwenye mkutano huo, aliongeza kwamba ubovu wa barabara hiyo unahusisha pia kipande cha zaidi ya kilometa 240 kwenye upande wa Msumbiji ambacho kinaunganisha miji ya Congress na Lichinga.

"Naiomba Serikali ya Tanzania kufanya mazungumzo na Msumbiji ili kuhakikisha barabara inafanyiwa marekebisho haraka iwekezekanavyo kwani barabara hii ni muhimu kwa uchumi wa Ruvuma na nchi kwa ujumla," alishauri.

Swedi alisema ana matumaini makubwa kwamba baada ya barabara hiyo kurekebishwa, itasaidia kukuza biashara ya mazao ya chakula na biashara baina ya Tanzania na Msumbiji na mikoa ya nyanda za juu kusini kwa ujumla.

Moja ya shughuli za kibiashara zinazofanyika kupitia mpaka wa Mkenda ni usafirishaji wa mahindi na unga wa mahindi kutoka Tanzania kwenda Msumbiji.

Takwimu za serikali zinaonyesha Mkoa wa Ruvuma una jumla ya ekari 4,007,746 zinazotumika kwa shughuli za kilimo.

Takwimu hizo zinaonyesha kwa mwaka wa kilimo 2018/19, mkoa huo ulizalisha jumla ya tani 1,255,134 za mazao ya chakula na biashara. Kati yake, tani 644,934 ni za mahindi.

Rais wa TCCIA, Paul Koyi, wakati wa mkutano na wafanyabiashara hao, aliuomba Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads) na mamlaka zingine za serikali kulifanyia kazi suala hilo ili kukuza biashara baina ya Tanzania na Msumbiji.

"Tutalifanyia kazi hili suala kwa kuzungumza na viongozi wa ngazi ya juu, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ili kuhakikisha tatizo hili linashughulikiwa.

"Matengenezo ya barabara hii ambayo inatumika kama 'shortcut' (njia ya mkato) baina ya nchi hizi mbili, yatasaidia kupunguza muda wa wafanyabiashara kusafirisha bidhaa zao," aliahidi.

Akizungumzia hali ya biashara mkoani Ruvuma, Kaimu Katibu Tawala Msaidizi (Uchumi na Uzalishaji), Deogratius Sibula, alikiri kufahamu malalamiko ya wafanyabiashara mkoani humo juu ya ubovu wa barabara inayounganisha Tanzania na Msumbiji kupitia mpaka wa Mkenda.

"Ni kweli tumekuwa tunapokea malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara kuhusiana na ubovu wa barabara hii. Nachukua nafasi hii kuwahakikishia wafanyabiashara wote kwamba serikali tushaanza kulifanyia kazi suala hili kwa kushirikiana na mamlaka husika kutoka Serikali ya Msumbiji, lengo likiwa kumaliza tatizo hili.

"Tayari tushafanya mawasiliano na mamlaka za Msumbiji na hivi karibuni tutaanza kurekebisha barabara," aliahidi.

Sibula pia alisema shughuli za kibiashara kati ya wafanyabiashara wa Tanzania na Malawi kupitia mpaka wa Mbababei zinafanyika pasi na vikwazo vyovyote vya miundombinu.

Meneja wa Tanroads mkoani Ruvuma, Lazeki Alinanuswe, aliwahakikishia wafanyabiashara kwamba ofisi yake italifanyia kazi suala hilo baada ya mvua kuisha.

"Toka jana wanarekebisha daraja lililokatika pale Nakawale kijijini," alisema meneja huyo.

# NHC yatangaza kibano wakwepa kodi wake 265

**Na Mary Geofrey**

SHIRIKA la Nyumba la Taifa (NHC), limetoa mwezi mmoja kwa wapangaji wake 265 nchini waliohama na wanaoendelea na upangaji kulipa madeni yao kabla ya kuchukuliwa hatua za kisheria.

Tangazo lililotolewa na NHC katika gazeti hili jana, liliwataka wadaiwa wote waliohama na wanaoendelea kuishi wameacha deni la Sh. trilioni 1.399.

Taarifa hiyo ilitaja wapangaji waliohama na kuacha madeni katika mikoa husika na kiasi wanachodaiwa kuwa ni Arusha Sh. bilioni 9.253, Dodoma Sh. bilioni 5.606, Ilala Sh. bilioni 964, Iringa Sh. bilioni 1.992 na Kigoma Sh. milioni 399.

Mingine ni Kilimanjaro Sh. bilioni 15.973 na Kinondoni Sh. bilioni 115.462.

Mikoa mingine ni Lindi Sh. bilioni 14.892, Mara Sh. bilioni 1.117, Mbeya Sh. bilioni 15.979, Morogoro Sh. bilioni 2.168, Mtwara Sh. bilioni 4.086, Tanga Sh. bilioni 15.401 na Temeke Sh. bilioni 232.928.

"Shirika linatoa rai kwa kila anayedaiwa kuhakikisha amelipa madeni yake ili kuepuka usumbufu utakaoweza kujitokeza kwa kutangazwa na kuchukuliwa hatua za kisheria. Ni matumaini yetu kuwa wadaiwa wote watatimiza wajibu wao wa kulipa madeni yao bila usumbufu," ilieleza taarifa hiyo.

Taarifa ilifafanua kuwa, wataendelea kuwatangaza wadaiwa sugu wote waliohama na wanaoendelea na upangaji hadi hapo madeni yao yote yatakapokuwa yamelipwa.

**"Shirika linatoa rai kwa kila anayedaiwa kuhakikisha amelipa madeni yake ili kuepuka usumbufu utakaoweza kujitokeza kwa kutangazwa na kuchukuliwa hatua za kisheria. Ni matumaini yetu kuwa wadaiwa wote watatimiza wajibu wao wa kulipa madeni yao bila usumbufu," ilieleza taarifa hiyo.**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Angalizo la TPSF kuhusu kupunguza wafanyakazi sahihi

TAASISI ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), imewaasa wanachama wa taasisi hiyo, wasitumie ugonjwa wa corona kupunguza wafanyakazi katika viwanda au kampuni wanazozimiliki.

Mwenyekiti wa Taasisi hiyo, Angelina Ngalula, ndiye aliyetoa angalizo hilo alipokuwa akizungumza na wanahabari jana jijini Dar es Salaam, kwa kusema kwamba Tanzania na dunia kwa jumla zinapita katika kipindi kigumu kutokana na ugonjwa wa corona.

Hata hivyo, alisema kuwa siyo busara kutumia tatizo hilo kupunguza wafanyakazi.

Alisema kupunguza wafanyakazi litakuwa ni tatizo kubwa kwa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla, hivyo aliwaomba waajiri kote nchini tushughulikie changamoto zilizopo kwa pamoja ili kulinda ajira nchini.

Ngalula alieleza zaidi kuwa kutumia matatizo kujinufaisha siyo utamaduni wa Watanzania.

Alizitaka baadhi ya sekta mfano utalii na kilimo, ambazo zimeathirika moja kwa moja kutokana na ugonjwa wa corona zikusanywe taarifa zinazoonyesha namna mtu mmoja mmoja alivyoathirika na taarifa hizo ziwasilishwe kwenye kikosi kazi ambacho kimeshaundwa.

Kwa mujibu wa Ngalula, taarifa hizo zitachambuliwa na wataalamu wao na kufikishwa serikalini, na kuonya kuwa waajiri wasitengeneza makundi yenye lengo la kujinufaisha badala yake Watanzania waendelee kufanya kazi kama Rais John Magufuli alivyoelekeza.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), Dk. Aggrey Mlimuka, aliiomba serikali kuondoa baadhi ya tozo kwa taasisi au kampuni zitakazoathiriwa na corona. Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Biashara (TNBC), Dk. Godwill Wanga, alisema kutumia corona kupunguza ajira ni kuhatarisha uchumi wa nchi.

Taasisi hizi mbili zimetoa angalizo hilo pengine baada ya kufuatilia kinachoendelea katika sekta mbalimbali, na kubaini kuwa kuna uwezekani kwa wafanyakazi kupoteza ajira zao kwa kisingizio cha ugonjwa wa corona.

Tunakubaliana na angalizo hili tukiamini kuwa wako baadhi ya waajiri ambao watatumia kisingizio cha janga la corona kuwaondoa kazini wafanyakazi wakati hakuna athari zozote kiuchumi ambazo zimetokea nchini hadi sasa.

Maelekezo yaliyotolewa na Rais Magufuli Jumapili, tunaona kuwa yanaweza kuwa mwarobaini wa athari za kiuchumi kwa nchi yetu, kwa kuwa wananchi wakiendelea na uzalishaji bila kujifungia ndani, wataendelea kuzalisha na kujipatia kipato na wakati huo huo serikali ikiendelea kupata kodi na kutoa huduma muhimu zikiwano za kijamii.

Ndiyo maana ATE kupitia kwa Dk. Aggrey Mlimuka, imesema huu si wakati mwafaka kwa watu kufungiwa ndani kwani athari zake zitakuwa kubwa kwenye ajira na uchumi wa nchi utaporomoka.

Zipo nchi zimefunga ofisi zote za umma na binafsi kukabiliana na ugonjwa wa corona, lakini kwa nchi yetu na nyingine zinazoendelea hazina uchumi mkubwa wala bajeti ya ziada kwa ajili ya kufanya hivyo.

Msisitizo wetu ni kuwa hatua za tahadhari zilizoshatolewa na zinazoendelea kutolewa na serikali yetu ziendelee kutekelezwa, huku kila mwananchi popote alipo akiendelea kuchapa kazi kwa bidii ili taifa letu lisisimame.

Tunaamini serikali itatumia mamlaka yake kuhakikisha waajiri wenye nia ovu kupunguza wafanyakazi bila sababu za msingi wanadhibitiwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Vita hii iunganishe wanasiasa nchini

KISWAHILI kina methali kadhaa zenye maana sawa kama 'umoja ni nguvu utengano ni udhafu, jiwe moja haliinjiki chungu na ndege wanaofanana huruka pamoja' ambazo zinahimiza umoja.

Methali hizi nimezilinganisha na wito ambao umetolewa na Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi kwa wanasiasa na wadau wa siasa, kwamba waache itikadi za vyama waungane kutoa elimu kuhusu virusi vya corona.

Wanasiasa wanatakiwa kuweka pembeni itikadi zao za kisiasa na kutumia ushawishi kuwaleta Watanzania pamoja kwa ajili ya kukabiliana na ugonjwa huo ambao unaoendelea kukatiza maisha ya watu.

Kwamba bila kufanya hivyo, ugonjwa utaendelea kusambaa na athari zake zitaonekana kijamii kisiasa na kiuchumi, kwa maana hiyo vyama na wadau wote wa siasa hawana budi kuwa kitu kimoja.

Anawataka waunge mkono miongozo iliyotolewa na serikali ili kupambana na maambukizi ya ugonjwa huo, ambao tayari umeingia nchini, hivyo vyama vya siasa viendelee kuwa mstari wa mbele kuhamasisha wanachama na wafuasi wao kutekeleza kwa vitendo maelekezo ambayo yameshatolewa.

Umoja katika kukabiliana na tatizo la virusi vya corona ni wa muhimu na lifanye Watanzania kuwa kitu kimoja bila kujali itikadi zao za kisiasa na kusaidiana kuelimisha wengine jinsi ya kuliepuka.

Dhana ya umoja imejengwa katika kuungana, kushikamana na kushirikiana au kufanya mambo kwa nia moja hata kuwa kitu kimoja, kwani kadiri umoja unavyoimarika ndivyo nafasi kubwa ya kufanikiwa huonekana.

Kwa maana hiyo, kilichosemwa na Jaji Mutungi ni kama jukumu la wanasiasa wote kwani ni vyema Watanzania wakaacha chuki na itikadi za kisiasa na kuwa wamoja kwa kutambua kwamba umoja ni nguvu.

Mambo ya kuwafanya Watanzania wachukiane hadi washindwe kushirikiana yasipewe nafasi, badala yake umoja utawale katika vita hii ya virusi vya corona kwa kutoa elimu, ili hatimaye viishe nchini.

Jaji Mutungi anawakumbusha wanasiasa kuwa ugonjwa huo ni hatari kama wataalamu wa afya wanavyosema, athari zake zinahusu kuondoa uhai, hivyo kama taifa bila kujali itikadi za kisiasa, ni muhimu kushikamana katika kukabiliana nao.

Umoja au ushirikiano wa vyama vya siasa usiishie kuungana kwa lengo la kukikabilia chama tawala katika uchaguzi tu, bali hata kwenye mambo ya msingi kama hayo ya kupambana na virusi vya corona.

Kinachotakiwa ni vyama kujishughulisha kwa dhati na masuala muhimu ya taifa, yenye umuhimu kwa wananchi, badala ya masuala ya kibinafsi zaidi ambayo yanaweza kujenga utengano badala ya umoja.

Siamini kama nchi ilirejesha mfumo wa vyama vingi vya siasa ili kujenga chuki miongoni mwa Watanzania, bali umoja ambao ni msingi mkubwa wa ushirikiano kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

Hivyo wito unapotolewa wa kuacha itikadi za kisiasa na kuungana kwa ajili ya kutoa elimu kuhusu madhara ya virusi vya corona, wanasiasa na wadau wa siasa wote waone umuhimu wa wito huo.

Penye wengi, pana mengi na Tanzania kuna vyama takribani 20 vya siasa na vipo vyenye ushawishi mkubwa kwa wananchi, vyote vijitose kutoa elimu ili kusaidia Watanzania kuepuka ugonjwa.

Ikumbukwe kuwa shughuli zenye mkusanyiko wa watu wengi imezuiwa kwa muda ili kukabiliana na ugonjwa huo, hivyo wakati hatua hizo zikiendelea kuchukuliwa, wanasiasa nao waungane na serikali katika vita hiyo.

Mtindo wa kubezana ambao umeanza kujitokeza kwa wanasiasa, usipewe nafasi kwani unaweza kuchangia kuwagawa na hivyo kusababisha wito wa Jaji Mutungi usizae matunda.

Kila Mtanzania kwa nafasi yake anatakiwa kuelimisha au kuelimishwa ili ajue jinsi ya kujikinga na virusi vya ugonjwa huo, kwani hiyo siyo kazi ya mtu fulani au chama fulani, bali ni jukumu la wote.

Ni muhimu kuzingatia kwamba dhana ya kuwa "umoja ni nguvu utengano ni udhahifu" ina nafasi kubwa katika kufanikisha jambo liwe la siasa au kutoa elimu wakati huu dunia inapokabiliana na virusi vya corona.

Hivyo kila mwanachama wa chama cha siasa awiwe na atumie muda wake, akili yake, nguvu zake na hekima yake kuhakikisha anashiriki kikamilifu katika kutoa elimu inayomwezesha Mtanzania kuwa salama.

BARUA / MJADALA

# Chonde chonde wazazi likizo hii tuwajali watoto

*MHARIRI*
*Salamu zangu kwa Nipashe,*

*NAPENDA kuwapongeza wana timu ya Nipashe kwa kazi nzuri ya kutuhabarisha sisi Watanzania na kutupa taarifa motomoto.*

*Hongereni kwa kazi na kwa juhudi nyingi mnazofanya ili kutuvutia wasomaji wenu.*

*Nikirudi kwenye barua yangu napanda kama mzazi kusikitika kuwa tatizo la corona limesababisha shule kufungwa hadi karibu na mwishoni mwa mwezi wa Aprili.*

*Ni ombi langu kwa wazazi na walezi kuwa kuwajali watoto wetu liwe ndilo jambo la muhimu tusiwaache wacheze na kuzurura na kuambukizwa maradhi, kupata ujauzito na hata kufundishwa uhalifu.*

*Najua kuwa kila mmoja ana shida na majukumu mengi yanayomweka mbali na familia, lakini tukumbuke kuwalinda na kuwajali watoto wetu wadogo kwa wakubwa.*

*Wazazi na walezi tuweke ratiba ya watoto kujisomea wakiwa nyumbani au pamoja na marafiki zao hasa majirani badala ya kuwaacha wakae bila msaada hadi shule zitakapoanza tena.*

*Kwa vile pia ni msimu wa mvua tusiwaache kucheza na kupotea kwenye madimbwi wala kusombwa na mafuriko kwa kukosa uangalizi.*

*Tukumbuke mtoto wetu ni kama mboni ya jicho kwani hakuna chenye thamani kuliko watoto wetu.*

***Mwamvita Masoud***
***Goba D'Salaam.***

## WASILIANA NASI:

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

# Usajili kwa alama za vidole mwarobaini unyanyasaji kijinsia

**Na Mwandishi Wetu**



Usajili wa laini za simu kwa alama za vidole ulivyofanyika. **PICHA: MTANDAO**

WATUMIAJI wa mitandao ya kijamii kama facebook, twitter, whatsApp na instagram pamoja na wale wanaochangamkia ujumbe mfupi (SMS) kwa sababu hawana simu janja au smartphone , zama hizi wako makini na yale mambo ya kujisahau na kusambaza picha za aibu.

Aidha, 'sms' za kutaka kuibia watu fedha nazo kwa kiasi fulani zilipungua kutokana na ukweli kuwa kabla ya kusajili simu kwa alama za vidole, kila leo watu walikutana na ujumbe uliokuwa unawaelekeza kutuma fedha ukitoka kwa matapeli.

Uchunguzi wa Nipashe, unaofanywa hivi karibuni kwa kuwahoji baadhi ya wanawake na wanafunzi wa kike kwenye baadhi ya vyuo, umebaini kuwa zama hizi watu wako makini na kwa kiasi kikubwa watumiaji wa simu janja wameachana na kusambaza picha za utupu.

AIdha, inaelekea kuwa wanafahamu kuwa kufanya hivyo kuna matokeo mabaya na hasa kwa vile kuna sheria za makosa ya mitandaoni.

Matumizi mabaya ya mitandao yanayohusisha usambazaji picha zinazoonyesha mambo ya aibu dhidi ya wanawake au unyanyasaji mitandaoni nao umepungua na huenda unatoweka, kwani kulikuwa na wakati picha za ngono zilikuwa zinasambazwa dhidi ya wanawake kwa kuwakomoa.

Ni wazi kuwa faida mojawapo ya kusajili namba kwa utaratibu wa 'baiometriki' ni kupunguza wizi, usumbufu, vitisho na la muhimu matukio ya unyanyasaji wanawake na watoto kwenye jamii.

Usajili huu umeepusha watu na uhalifu kama wizi, utapeli, kunyanyasa wanawake kwenye mitandao mambo ambayo hapo awali yalileta maafa vikiwamo vifo vya baadhi ya watumiaji wa mawasiliano hasa mabinti ambao walioamua kujiua ili kuachana na aibu.

Ni wazi kuwa wasichana hasa vyuoni walikuwa wakinyanyaswa kupitia facebook au whatsapp mambo yanayotokea baada ya mabinti kuzoea 'kuchati' na watu mbalimbali wakiwamo wanaume wasiofahamiana ambao wanaamini kuwa wangekuwa marafiki au hata wachumba na baadaye wenza wa maisha.

Kupitia mtandao wanafunzi hutumia kamera ya mtandao (web camera) iliyoko kwenye kwenye kompyuta kuona sura za wale wanaowasiliana nao na kujenga mazoea na hufikia kipindi cha kujiachia na kuwatumia picha za aibu wakati mwingine za utupu.

Japo wanaliona kuwa si jambo baya lakini iwapo kuna marafiki wenye nia mbaya ya kuwachafua mabinti mwisho huwa ni aibu na majuto. Kupitia mazoea hupeana picha zikiwamo za utupu, nyingine zikionyesha matiti ya mtumiaji na mambo mengine ya aibu.

Kunyanyasana huko licha ya kwamba kulianzia kwa wanawake au mabinti wenyewe watu waliokuwa na nia mbaya walizisambaza kwenye mitandao hiyo na kumfanya mtumiaji kujisikia vibaya kwani ndiye kitovu cha aibu na matendo ya ngono yasiyotizamika.

Kabla ya usajili huo walioathirika na unyanyasaji mitandao walikuwa mabinti kwa kuwa taarifa zinapowafikia wazazi, marafiki, walimu na majirani watoto hawa wanakosa pa kukimbilia na kuamua kujitia kitanzi.

Kutumia simu kunyanyasa wanawake kuliwafanya wajione kama wasio na pa kukimbilia kwani wakiwa shuleni ilikuwa ni aibu kadhalika nyumbani, mitaani na hata kwa marafiki zao ndiyo maana wakati mwingine waliamua kujiua.

Si hivyo, usajili na kupiga marufuku mazoea ya kusambaza picha za aibu si kwamba umenufaisha mabinti pekee bali pia umeongeza maadili kwenye jamii kwa kuwa umedhibiti uhalifu huo, kwani hapo awali baadhi ya waliosambaza picha, waliendelea kuwakomoa kwa kuzirudisha kila wakati kwenye mitandao hata pale zilipokuwa zimefutwa.

Kwa kutumia sheria na kufuatilia namba zinazotuma picha hizo, wahalifu hao wamedhibitiwa.

Wanafunzi vyuoni waliumia zaidi kwa kuwa athari moja kubwa ya unyanyasaji wa mitandao ni mhusika kushindwa kujinasua kwa maana kuwa huwezi kuikimbia aibu yake kwa vile ni ushahidi wa wazi na unaomgusa moja kwa moja.

Picha zako zinasambazwa kila mahali, kila wakati na popote mnyanyasaji anaposikia kufanya hivyo ndiyo maana mwathirika alikuwa hana pakuponea na wakati mwingine ilikuwa inatumiwa kama silaha ya kumkomoa.

Wasichana sehemu nyingine duniani wanatajwa kuwa wako kwenye hatari zaidi ya kunyanyaswa kuliko wanaume. Hawa wamo hatarini kwa vile hushawishika na kuhadaika haraka na wengi ni hawajafahamu kuwa kutoa picha za namna hiyo kunaweza kuwa na athari.

Mtumiaji anakuwa hana cha kufanya pale hasimu wake au mwenye nia ya kumwaibisha anapofungua ukurasa maalumu wa kumtukana na kumchafua.

Hata hivyo jitihada kama za kulalamika zinaweza kuwasaidia walioumizwa kwani mitandao inawapa nafasi ya kuandika kile wasichokitaka mtandaoni hasa kwenye facebook au kwingineko na kutuma ujumbe wa kulalamika.

Hata hivyo pamoja na kudhibiti mambo haya hapa nyumbani huenda wahusika wengine wa nje ya nchi wanaweza kufanya unyanyasaji huo.

Kwa hilo, kadhalika ni vyema kuwasiliana na mamlaka za mawasiliano za nchi kwa mfano TCRA kulalamika na kutaka picha hizo kuondolewa mitandaoni au kwenye blogi.

Licha ya kwamba Tanzania imedhibiti na kusajili simu ni vyema pia wasichana na vijana wengine wakaacha kupeleka picha za ngono na za aibu kwenye mitandao kwa kuwa mambo haya yanaweza kuathiri maisha yao.

KABWELA — NA FADHILI MOHAMMED



# Wazazi wanaopeleka watoto 'tuition' waonywa

**Na Waandishi Wetu, DODOMA**

NAIBU Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) anayeshughulikia elimu, Gerald Mweli, amewaonya wazazi wanaopeleka watoto wao 'tuition' baada ya serikali kufunga shule na vyuo kwa mwezi mmoja kutokana na tishio la virusi vya corona.

Alisema serikali imejipanga kuhakikisha wanafunzi wanakamilisha mtaala watakaporejea shule kipindi hicho kumalizika.

Akizungumza jana katika kipindi cha asubuhi kwenye runinga ya taifa, Mweli alisema ni vyema wazazi hao wakaacha watoto wakae nyumbani na kuzingatia ushauri wa wataalamu.

"Wazazi msiwaongezee mzigo watoto na kuwaweka kwenye hatari, wabaki ndani kila mara serikali itakuwa inatoa matangazo na kuelimisha jinsi ya kujikinga na corona kupitia vyombo vya habari," alisema.

"Sisi kama serikali tunafahamu jinsi gani tutawezesha watoto kukamilisha mtaala wao watakaporudi, tumejipanga, tumeandaa ratiba, kupitia vipindi vya likizo ile nyingine na saa za ziada tutakamilisha mtaala wao," alisema.

Katika hatua nyingine, Askofu wa Kanda ya Kati wa Kanisa la EAGT, Denis Livingstone, amewashauri wazazi na walezi kuwalinda na kuwanawisha mikono watoto wao kwa maji na sabuni ili kuwaepusha na ugonjwa huo.

"Ni imani yangu kama serikali inavyosisitiza kujilinda na ugonjwa huo ili usilete maafa ya kifo, Watanzania kamwe hawatazembea bali watakuwa mstari wa mbele kuzingatia maelekezo yanayotolewa na viongozi wetu na wataalamu," alisema.

Aliwashauri Watanzania kutoudharau ugonjwa kwa kupuuza maelekezo yanayotolewa na serikali pamoja na viongozi mbalimbali ili kujilinda dhidi ya ugonjwa huo.

Naye, Kada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Samwel Chimanyi, aliomba serikali kuvigawa vitasaka mikono katika maeneo ya vijijini bure ili kunusuru maisha ya wananchi.

Pia alishauri kwa kutumia wataalamu wa afya wafike vijijini kutoa elimu ya jinsi ya kujikinga na ugonjwa huo.



Baadhi ya wakazi wa Kata ya Muhoro, Kijiji cha Shela, wilayani Rufiji, mkoani Pwani, wakishuka kwenye mtumbwi wanaoutumia kuvuka na kuyafikia makazi yao, jana, baada ya barabara kujaa maji kutokana na athari ya maafa ya mafuriko. Miundombinu ya barabara, shule na zahanati katika wilaya hiyo, imeathiriwa na maafa hayo. **PICHA: OWM**

# Mabilioni kugharamia miradi ya maji Tarime

**Na Ambrose Mwita, TARIME**

SERIKALI imetoa Sh. bilioni 1.4 kugharamia miradi ya maji inayoendelea kutekelezwa katika Wilaya ya Tarime, mkoani Mara kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20.

Miradi hiyo inayotekelezwa katika halmashauri mbili za vijijini na mjini, itanufaisha pia mji mdogo wa mpakani wa Sirari na takribani wakazi 32,000 wanatarajiwa kufikiwa na huduma hiyo.

Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), wilayani hapa, Marwa Muraza, alisema maandalizi ya awali yamekamilika ikiwa pamoja na upembuzi yakinifu na kinachosubiriwa ni hatua ya mwisho ya utekelezaji.

Alisema utekelezaji wa mradi huo unahusisha ujenzi wa tangi kubwa litakalokuwa na ujazo wa lita milioni sita katika eneo la Rebu nje kidogo ya mji wa Tarime tofauti na ilivyo sasa, wakazi hutegemea vyanzo viwili pekee vya Nyandurumo na Tagota.

"Vyanzo hivi vilitengenezwa miaka mingi iliyopita na hivyo kushindwa kuhimili mahitaji ya wakazi wanaoongezeka kila kukicha na isitoshe vinakaribia kufutika kutokana na kuongezeka shughuli za kibinadamu maeneo hayo," alisema.

Alifafanua kwamba miongoni mwa wanufaika wakuu wa mradi huo ni jengo la Afrika Mashariki lililopo katika mpaka wa Sirari, lenye taasisi 15 za serikali, pia tangi la maji limejengwa.

"Mradi huu ukikamilika, maji yatavunwa kutoka Ziwa Victoria kwa kutumia pampu zilizo imara na yatatibiwa na kusambazwa Wilaya ya Tarime na viunga vyake, tayari tumefanya ununuzi wa vifaa na hivi sasa tunakarabati pampu za mkono zipatazo 40 zitakazotumika kuvuna maji ya dharura kutoka visima virefu," alisisitiza.

Mwishoni mwa mwaka 2019 akiwa ziarani wilayani hapa Rais Dk. John Magufuli aliahidi kutoa fedha zaidi ya Sh. bilioni 1.5 kutekeleza miradi ya maji wilayani hapa baada ya kusikiliza kilio cha Mbunge wa Jimbo la Tarime Mjini, Esther Matiko.

Matiko alisema kwamba wakazi wa mji wa Tarime na viunga vyake wamekosa huduma ya majisafi na salama kwa miaka mingi na katika wakati huo wameendelea kutumia maji kutoka vyanzo vya asili ambavyo havikidhi matakwa ya kiafya.

# Mafuriko Rufiji yaathiri barabara, shule, zahanati

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI za usimamizi wa maafa wilayani Rufiji mkoani Pwani, zimeshauriwa kuchukua hatua za haraka kurejesha miundombinu ya barabara, shule na zahanati zilizoathirika na maafa ya mafuriko.

Kata ya Muhoro na Chumbi ni miongoni mwa zilizoathirika na maafa hayo na kwa sasa madaraja matatu ya barabara ya Nyamwage - Utete inayoelekea makao makuu ya wilaya hiyo yameathirika.

Akiongea baada ya kukagua athari za maafa na kukabidhi misaada kwa waathirika juzi, Mkurugenzi Idara ya Uratibu wa shughuli za maafa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kanali Jimmy Matamwe, alisema Kamati za Usimamizi kuanzia ngazi ya kijiji hadi wilaya, kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa maafa Na. 7 ya mwaka 2015 zinawajibika kutekeleza operesheni za dharura.

"Nimezishauri kamati za usimamizi wa maafa katika wilaya hii kuwa na mipango ya muda mfupi ya kuhakikisha barabara zinapitika kipindi chote ili wananchi wasishindwe kutumia miundombinu hiyo, kwa kuwa zipo barabara zinaunganisha mikoa ya kusini na zipo zinawasaidia wananchi kuzifikia huduma za kijamii," alisisitiza Kanali Matamwe.

Awali, akiongea baada ya kupokea misaada kutoka kwa Idara ya Uratibu wa maafa Ofisi ya Waziri Mkuu, Mkuu wa wilaya hiyo, Juma Njwayo, amefafanua kuwa mpaka sasa kuna zaidi ya watu 20,000 walioathirika na maafa hayo baada ya nyumba 100 kuzingirwa na maji.

"Tunaishukuru Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kutuletea magodoro, mikeka, vyandarua, ndoo na sabuni na naamini kamati za maafa zitawajibika kugawa vifaa hivi kwa mujibu wa taratibu za menejimenti ya maafa. Wilaya tunaendelea kukabiliana na maafa kwa kaya 6,000, kama tulivyoshauriwa kuhusu miundombinu, kwa kushirikiana na Tanroads tunaendelea kwa kasi kuchukua hatua za kurejesha miundombinu yote iliyoathirika," alisisitiza Njwayo.

Mbunge wa Jimbo la Rufiji, Mohamed Mchengerwa, alisema tangu maafa ya mafuriko yatokee wilayani humo, wanapata ushirikiano wa kutosha kutoka kwa ofisi hiyo, kupitia Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu mwenye dhamana ya masuala ya maafa, Jenista Mhagama, kwa kuwatuma wataalamu.

Kwa mujibu wa taarifa ya Mamlaka ya Hali Hewa iliyotolewa mwezi Februari, mwaka huu kutakuwa na mvua za juu ya wastani katika eneo kubwa la nchi kati ya mwezi Machi hadi Mei.

**"Tunaishukuru Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kutuletea magodoro, mikeka, vyandarua, ndoo na sabuni na naamini kamati za maafa zitawajibika kugawa vifaa hivi kwa mujibu wa taratibu za menejimenti ya maafa. Wilaya tunaendelea kukabiliana na maafa kwa kaya 6,000, kama tulivyoshauriwa kuhusu miundombinu, kwa kushirikiana na Tanroads tunaendelea kwa kasi kuchukua hatua za kurejesha miundombinu yote iliyoathirika," alisisitiza Njwayo.**

HABARI KITAIFA

# H/shauri kuchangia ukarabati wa mialo

**Na Restuta Damian, BUKOBA**

HALMASHAURI za wilaya za Muleba, Missenyi, Bukoba na Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera, zimetakiwa kuchangia fedha kwa lengo la kurekebisha miundombinu ya mialo iliyosombwa na maji.

Maji hayo yaliyotokana na kujaa kwa Ziwa Victoria. Mialo hiyo iliyoko katika halmashauri hizo imekuwa ikichangia makusanyo ya mazao ya samaki ambayo ni sehemu ya mapato ya sekta ya uvuvi mkoani Kagera.

Miundombinu hiyo ni ofisi za usimamizi wa rasilimali za mialo (BMU), jengo la kupokelea samaki, vyoo na maeneo ya kuegesha mitumbwi iliyokumbwa maji ya Ziwa Victoria kutokana na mvua nyingi zinazoendelea kunyesha.

Akizungumza na Nipashe, Ofisa Uvuvi wa mkoa huo, Efraz Mkama, alisema uchangiaji huo ni kuangalia namna ya kuendelea kuwa mialo ambayo ni vyanzo vya ukusanyaji.

Mkama alisema kuwa tatizo la maji linaweza kusababisha wavuvi kuhama maeneo hayo na kutafuta shemu nyingine ili kuendelea na shughuli zao.

"Taarifa zilizopo ni halmashauri nne na kila halmashauri ina zaidi ya mialo mitatu iliyoathiriwa hasa miundombinu, na inayoongoza ni Muleba yenye mialo 22 iliyoathiriwa," alieleza Mkama.

"Halmashauri ya Missenyi ambayo ina mwalo wa Kaishebu ambao jengo lake la mapokezi ya samaki lipo katika katikati ya maji kabisa," alisema Mkama.

Aidha, alisema mkoa una mialo 116 yakiwamo maziwa madogo ambayo yanategemewa kwenye ukusanyaji wa mazao ya samaki ambapo mwaka wa fedha 2017/201 8 iliweza kukusanya shilingi bilioni 1.86, wakati lengo lilikuwa shilingi bilioni 1.44.

Aliendelea kusema kuwa, mwaka 2018/2019 likusanya shilingi bilioni 2.8 ingawa lengo lilikuwa Sh. bilioni 1.83 kutoka kwenye nyanzo vya usajili wa vyombo vya uvuvi, wavuvi, leseni za ukusanyaji wa mazao ya samaki na ushuru wa mialo.

> **"Taarifa zilizopo ni halmashauri nne na kila halmashauri ina zaidi ya mialo mitatu iliyoathiriwa hasa miundombinu, na inayoongoza ni Muleba yenye mialo 22 iliyoathiriwa," alieleza Mkama.**

# Mapato yaufunga mnara mawasiliano

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

WAKAZI wa Kijiji cha Bunango Kata ya Bugarama, Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wameufunga mnala wa mawasiliano wa kampuni ya Vodacom kwa madai ya kushindwa kulipa mapato ya serikali ya kijiji kwa miaka 19.

Walidai kuwa tangu mwaka 2001 wasimamizi wa mnala huo hawajawahi kulipa fedha za mapato ya serikali na kusababisha kijiji kushindwa kutatua baadhi ya changamoto zilizopo hasa za uharibifu wa miundombinu kutokana na mvua za masika zinazoendelea.

Walidai wapo katika mazungumzo na kampuni zingine za simu zenye minala ili ijulikane zinalipa fedha kwa nani, na kuomba serikali kufanya uhakiki kwenye minala yote ya simu ili kuwachukua hatua za kisheria madalali wasio waadilifu.

Hayo yalibainishwa na Mwenyekiti wa Kijiji cha Bunango, Anna Peter, wakati akizungumza na vyombo vya habari, na kusema kuwa licha ya serikali ya kijiji kutolipwa mapato, wahusika wa mnala huo hawajamlipa aliyewapangisha kiwanja kilichojengwa mnala huo.

"Tumekuwa tukiomba mazungumzo na wamiliki wa mnala, lakini hawafiki na kutoa majibu ambayo hayaridhishi...sisi tumeamua kuufunga mnala huu kama moja ya njia za kuomba suluhu ya upatikanaji wa kodi ya kijiji, na fedha ya aliyewapangisha eneo la ujenzi," alisema Peter.

Aliyepangisha eneo la ujenzi wa mnala wa Kampuni ya Vodacom, Robert Busegwa, alisema ameshasainishwa mikata mbalimbali ukiwamo ya Sh. milioni 5.5, milioni 3.5 na milioni 1.1, na kwamba kila mkataba anaosaini ni tofauti ukilinganisha na fedha anayopatiwa kila baada ya mwaka mmoja.

Akijibu malalamiko hayo mmoja wa wasimamizi wa minala hiyo kutoka kampuni ya Helious Tower Tanzania (HTT), ambaye hakutaka jina lake liandikwe gazetini, alisema ili mmiliki wa eneo lililojengwa mnala na serikali ya kijiji wapate haki zao.



Vijana wakipaa samaki ili kujipatia kipato cha siku katika soko la Kimataifa la Magogoni (Feri), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mahakama zote kuendesha mashauri kwa Tehama

**Na Neema Emmanuel, MWANZA**

MAHAKAMA zote nchini zimeanza kutumia mifumo ya Tehama katika uendeshaji na usajili wa mashauri.

Lengo ni kuharakisha na kurahisisha upatikanaji wa huduma za kimahakama na kuzisogeza karibu na wananchi bila ya kufika mahakamani pamoja na kutekeleza maelekezo na tahadhari ambazo zimetolewa na serikali.

Akitoa taarifa ya uendeshaji wa shughuli za mahakama wakati huu wa tahadhari ya janga la corona, Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, alisema Tehama ni silaha muhimu katika kuzuia mikusanyiko, misongamano na wasindikizaji wakati wa kusikilizwa kwa mashauri ambayo kwa sasa yatasajiliwa kwa njia ya mashauri kielektroniki.

Alisema kanuni za kufungua mashauri kwa njia ya mitandao zilianza kufanya kazi tangu Aprili 13, mwaka 2018, hivyo kanuni hizo ni muhimu kwa sasa katika kufungua mashauri kimtandao na zitasambazwa ili wananchi na wadau watumie utaratibu huo.

"Matumizi ya Tehama ni matunda ya mpango wa miaka mitano wa maboresho ya Mahakama, hivyo wadau wetu ni lazima wakubali masharti ambayo tumeweka kama kutokuwa na wasindikizaji, kunawa mikono na kutumia mitandao zaidi," alisema Prof. Juma.

Aliongeza kuwa mashauri yote ya jinai jijini Dar es Salaam yanayoahirishwa kutokana na sababu mbalimbali watuhumiwa waliopo katika Gereza la Keko na Segerea hawatalazimika kufikishwa mahakamani badala yake mashauri hayo yataahirishwa kwa njia ya mahakama mtandao na hivi punde kesi za jinai zitasajiliwa na wahusika kupitia mitandao itakayotayarishwa kwa ajili hiyo.

Alisema Mahakama imeweka mitambo ya kisasa kwenye Mahakama Kuu, Masijala Kuu Dar es Salaam, Mahakama ya Kuu Mbeya, Mahakama Kuu Bukoba, kituo cha mafunzo Kisutu, Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto na magereza za Keko na Segerea.

"Nawaomba viongozi wote wa mahakama katika ngazi zote huu ndio wakati wa kuonyesha uongozi kwa kuwasaidia Watanzania waendelee kupata huduma za utoaji haki katika dunia, ambayo inapata msukosuko wa ugonjwa wa corona tukumbuke kuwa karne ya 21 ni karne ya ushindani, ni karne yenye usumbufu mwingi na yenye nafasi nyingi zinazohitaji mabadiliko," alisema Jaji Mkuu.

## Waziri awapa somo makamishna wapya

**Na Munir Shemweta, DODOMA MJINI**

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amewataka Makamishna Wasaidizi wa Ardhi wa mikoa kushirikiana na wakuu wa wilaya katika kutekeleza majukumu yao, ili kufanya kazi kwa ufanisi na kuondoa migogoro ya ardhi.

Dk. Mabula alitoa agizo hilo jana alipokutana katika kikao maalum na makamishna hao wa mikoa jijini Dodoma, ikiwa ni mara ya kwanza tangu kuanzishwa kwa ofisi za ardhi za mikoa ili kurahisisha utoaji huduma za ardhi na kupunguza migogoro.

Alisema ni vizuri makamishna hao walioteuliwa, kutumia nafasi zao kushirikiana na wakuu wa wilaya na ofisi za wakuu wa mikoa sambamba na kutoa elimu kuhusiana na masuala ya ardhi ili kuwajengea uelewa na ikiwezekana kuwapatia sheria za ardhi ili kupunguza migogoro ya ardhi.

Aliwataka watendaji hao wapya wa ardhi wa mikoa ya Tanzania Bara kusisitiza utendaji kazi kwa ushirikiano kati ya wataalamu wa sekta ya ardhi na kutolea mfano maofisa ardhi kushirikiana na wataalamu wa fani nyingine za ardhi katika kuandaa hati.

"Siyo ofisa ardhi pekee anaweza kushiriki katika uandaaji hati, bali wataalamu wengine wa sekta hiyo nao wanaweza kushiriki kazi hiyo maana wote wamesoma chuo kimoja na hilo limefanyika kwa baadhi ya maeneo," alisema.

Aliwataka makamishna hao kuhakikisha panakuwapo mawasiliano kutoka ofisa mmoja kwenda kwa mwingine kwenye majalada ya ardhi na kuipongeza Ofisi ya Ardhi ya Kanda ya Ziwa kwa kutoa mafunzo kwa watunza kumbukumbu wa ardhi katika ofisi za halmashauri za kanda hiyo baada ya kuona watendaji wake hawafanyi vizuri.

Akizungumzia utoaji hati za ardhi, Dk. Mabula alitaka kasi ya utoaji hati iongezeke na kubainisha kuwa ni vizuri watendaji hao wapya wa ardhi kuwasiliana na wakurugenzi wa halmashauri, ili hati zitolewe kwa pamoja badala ya kila mmiliki kuifuta katika ofisi za kanda au mkoa.

Vilevile, alisisitiza suala la upimaji maeneo yote ya umma na kupatiwa hati kwa lengo la kupuka migogoro inayosababishwa na uvamizi wa maeneo hayo kutokana na kutopimwa.

Dk. Mabula pia aliwataka makamishna hao kuhakikisha wakati wa utendaji wao, wanatilia mkazo ukusanyaji maduhuli ya serikali kupitia kodi ya pango la ardhi sambamba na kuingiza viwanja vyote kwenye mfumo wa kielektroniki.

Kamishana Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Shinyanga, Hezekiel Kitlya, aliishukuru wizara kwa uamuzi wa kuanzisha ofisi za ardhi za mikoa na kueleza kuwa ofsi hizo zitasaidia kutoa huduma za ardhi kwa wananchi na kupunguza migogoro ya ardhi.

Kitlya aliongeza kuwa, ili ofisi hizo zifanye kazi zake kwa ufanisi, kuna haja wizara kuhakikisha zinapatiwa vifaa na wataalamu wa kutosha kukidhi mahitaji yote ya sekta ya ardhi.

# LATRA yafunga vidhibiti mwendo Coaster Dar - Moro

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

MAGARI aina ya Coaster yanayofanya safari zake Mbezi kwenda Morogoro yamefungwa vidhibiti mwendo ili kuzuia ajali na kuzidhibiti kukatisha safari kwa mujibu wa usajili wao.

Kazi ya kufunga vidhibiti mwendo hivyo imefanywa jana na Mamlaka ya Usafiri wa Nchi Kavu (LATRA), katika stendi ya mabasi ya Mailimoja, mjini Kibaha.

Akiongea na waandishi wa habari kuhusu kazi hiyo, Ofisa wa LATRA, Stanley Ndunguru alisema, imefanyika kumlinda abiria, chombo cha usafiri na gharama za uendeshaji.

Alisema, baada ya kufungwa kidhibiti mwendo, dereva akivuka spidi 80 atatozwa faini na kufungiwa leseni yake, pia itasaidia kubaini madereva wanaokatisha ruti.

Aliwaomba wamiliki wa magari hayo kutoa ushirikiano kusaidia vyombo vyao vya usafiri kudumu kwa muda mrefu na kuokoa gharama ya mafuta ambayo ilikuwa ikitumika awali.

Alisema, magari yatakayofungwa vidhibiti mwendo yatakuwa na faida kwa wamiliki kwa kuwa watakuwa na uwezo wa kuona gari ilipo bila kupewa taarifa na dereva.

LATRA pia ilifanya ukaguzi kwa magari yanayopita katika stendi hiyo kuhakikisha hali ya usafi kwa abiria, dereva na kukagua kama wanatekeleza agizo la kinga dhidi ya virusi vya corona.

Mmoja wa madereva ambayeo gari yake ilifungwa kidhibiti mwendo, Mustapha Sadick, alipongeza uamuzi huo na kuomba wamiliki waanze kuwalipa mishahara.

"Hivi vidhibiti mwendo tulivyofungiwa ukizidisha mwendo faini inaingia kwa dereva sio mmiliki, na hapa zile ruti tulizokuwa tunaenda zilikuwa zinatusaidia kwakuwa hatuna mishahara, hili zoezi litasaidia matumizi ya mafuta lakini kwa upande wa hesabu litatuathiri," alisema Mustapha.

Aliomba wakati wa ufunguji vidhibiti mwendo ukiendelea washirikishwe zaidi wamiliki ili watambue kinachoendelea hata hesabu isipotimia kusiwe na migogoro.




Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Kata ya Kivukoni, Sharik Choughule (wa pili kushoto), akikabidhi vifaa na sabuni za kuosha mikono kwa Ofisa Mtendaji wa Kata hiyo, Remmy Mishekhe (wa pili kulia), kwa ajili ya kujilinda na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona, katika kituo cha Bajaj cha Feri, Dar es Salaam, juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Sababu watalii kuongezeka Hifadhi ya Taifa Saanane

**Na Daniel Sabuni, MWANZA**

HIFADHI ya Taifa ya kisiwa cha Saanane imeongeza idadi ya wataii wa ndani na wa nje katika kipindi cha miaka sita na kufanya jumla yao kufikia 74,890.

Hali hiyo imesababishwa na uhamasishwaji na kutangaza vivutio vilivyomo ndani na nje ya nchi.

Hayo yalielezwa na Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi na Mkuu wa Hifadhi hiyo, Eva Mallya, wakati wa programu maalumu ya kutangaza vivutio vilivyomo katika hifadhi hiyo ili kukukuza na kuongeza idadi ya watalii wa ndani.

Mallya alisema kati ya Julai 2013 na Oktoba 2019, hifadhi ilipokea idadi ya watalii wa ndani, wa nje na wa Afrika Mashariki 74,890 ambao ni ongezeko la wageni 5,968 kati ya mwaka wa fedha 2013/2014 na 2018/2019.

Akizungumzia mafanikio ya ongezeko la watalii wa ndani kutembelea hifadhi hiyo, Mallya alisema ni kutokana na juhudi mbalimbali za kutangaza vivutio vilivyomo kwenye shule, taasisi za umma na za watu binafsi pamoja na kufundisha elimu na faida za uhifadhi katika maisha ya binadamu.

"Pamoja na majukumu muhimu na makubwa tunayofanya hapa Saanane, kubwa kabisa ni kuhifadhi mazalia ya samaki, tunafanya doria za mara kwa mara ili majangili wasivue samaki kwa kutumia nyavu ndogo au kwa sumu," alisema na kuongeza. "Kwa kufanya hivyo mazalia yako salama na samaki zitaendelea kuzaliana vizazi hadi vizazi, tofauti na hivyo samaki na aina zake zitatoweka."

Alitaja vivutio vilivyomo Saanane kuwa ni wanyamapori wa asili na wakupandikizwa kama pimbi, fisi maji, paka mwitu, mamba, mijusi na aina mbalimbali za samaki kama sato na sangara, nyoka waina mbali mbali wakiwemo chatu, aina 70 za ndege wahamaji na wakazi.

# CCM yaomba ununuzi CT Scan Mount Meru

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

KAIMU Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Arusha, Denis Zakaria, ameishauri serikali kununua mashine ya CT Scan na MRI kwa ajili ya Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Mount Meru.

Zakaria alitoa ushauri huo wakati wa kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC), kilichokuwa kinapitia utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2019- 2020 pamoja na kupitia mapendekezo ya mpango na makadirio ya bajeti ya mwaka 2020-2021.

Alisema Ilani ya CCM inasisitiza kuwa na wananchi wenye afya bora, hivyo kuna kila sababu ya kuwa na kupaumbele cha kuboresha sekta ya afya katika hospitali ya hiyo, kwa kinunua mashine ya CT Scan na MRI ili wananchi wapate huduma kwa haraka, tofauti na sasa wanapolazimika kwenda hospitali za binafsi kwa gharama kubwa.

Alisema katika mpango huo haujaonyesha ununuzi wa mashine hizo muhimu kwa hospitali hiyo ya rufani, hivyo ni vyema vifaa hivyo vikaingizwa kwenye bajeti ya 2020- 2021.

Kuhusu malalamiko ya baadhi ya wagonjwa kukosa dawa kwenye vituo vya afya na zahanati kukosa dawa kutokana na madeni ya Bohari Kuu ya Dawa nchini (MSD), Zakaria aliutaka uongozi wa mkoa wa Arusha kulipa madeni hayo mara moja ili wananchi wananchi wapate huduma za dawa na chanjo za mama na mtoto.

Awali katika uwasilishwaji wa taarifa ya sekta ya afya, ilielezwa kwamba kuna ukosefu wa huduma za tiba ya kisasa katika Hospitali ya Rufani ya Mount Meru kwa kutokuwa na CT Scan na MRI.

Pia, taarifa hiyo ilieleza kuwa baadhi ya vituo vya kutolea huduma za afya zimezuiliwa kununua dawa MSD, kutokana na kuwa na madeni, lakini ukosefu wa bomba za chanjo kwa watoto hususani bomba zenye ujazo wa milimita 0.5.

Aidha, kikao hicho kimepitisha mpango wa mapendekezo ya bajeti ya mwaka 2020-2021 kiasi cha zaidi ya Sh. bilioni 298 ambazo kati ya hizo Sh. bilioni 42.59 za mapato ya halmashauri zinazohitajika kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo.



Mkuu wa Wilaya ya Karatu, mkoani Arusha, Theresia Mahongo, akizungumza na wadau wa afya na watu binafsi, kuhusiana na namna ya kutoa elimu juu ya virusi vya ugonjwa wa corona wilayani humo juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

## Ushirika wafunguka kasi ya kumaliza kesi

**Na Jaliwason Jasson, BABATI**

CHAMA Kikuu cha Ushirika mkoani Manyara cha Rift Valley Cooperative Union (Rivacu), kimetamba kuzimaliza kesi zinazokikabili chama hicho kwa muda mrefu.

Hayo yalisemwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Rivacu, Michael Tsaxara, wakati akizungumza na Nipashe.

Alisema Rivacu ina migogoro ya muda mrefu kama mgogoro wa shamba la Endarofta, ambao umefukuta kati yao na Kanisa Katoliki Jimbo la Mbulu.

"Juzi tulikaa na askofu na wanasheria wetu na wa kanisa, tulikubaliana shamba la Endarofta lililokuwa linalimwa na shule mgogoro uishe," alisema Tsaxara.

Aidha, alisema bodi hiyo ilipochaguliwa mwaka 2018 ilikaa na kanisa na kukubaliana waondoe mgogoro huo ambao ulikuwa unatumia fedha nyingi bila sababu.

Katika kuhakikisha mali za Rivacu zinakuwa salama, alisema uongozi wa Rivacu umehakiki mali zote na kubaini mali zisizoingizwa kwenye daftari ni pamoja na jengo la Bashay la ushirika.

Tsaxara bila kuwataja majina, alisema viongozi waliopita walizifanya mali za chama kuwa ni mtaji wao na kwenda kila mara mahakamani.

Mkazi wa Negamsii, Veronica Christopher, akizungumzia ushirika, alisema umebaki kuwa historia tofauti na zamani ulivyokuwa unasaidia.

Alisema ili kuufufua ushirika unahitaji watu wenye uthubutu ambao hawana tamaa za mali, vinginevyo jamii itabaki kuibiwa.

Mkazi mwingine, Patrick Thomas, akizungumza na Nipashe, alisema ushirika ni mzuri kwa kuwa unamsaidia mkulima kupata soko ila kitu kinachokwamisha ni migogoro inafukuta kila uchao ambayo mingi ni ya migongano ya kimaslahi.

# Minada marufuku Mbulu kisa corona

**Na Cynthia Mwilolezi, MANYARA**

MKUU wa Wilaya ya Mbulu mkoani Manyara, Chelestino Mofuga, amepiga marufuku kuendelea kwa shughuli za minada kwenye wilaya hiyo, ili kukabiliana na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona.

Wilaya hiyo ina minada mbalimbali ambayo baadhi hukutanisha makundi ya watu wa wilaya za Karatu mkoani Arusha, Iramba na Mkalama mkoani Singida.

Mofuga akizungumza jana, alisema kutokana na serikali kupiga marufuku mikusanyiko isiyo na lazima, ameagiza kusitishwa kwa shughuli za minada wilayani humo.

Alisema ameagiza shughuli za minada kusitishwa kwa muda wa siku 30, ili kuona hali itakavyokuwa kwenye maambukizi ya ugonjwa wa corona itakavyokuwa.

"Wilaya yetu inapakana na mikoa ya Arusha na Singida, hivyo ili kuondoka na mikusanyiko isiyo ya lazima, tumeagiza kusitisha kwa muda shughuli za minada yote hapa Mbulu," alisema Mofuga.

Aliwataka wananchi wa wilaya hiyo kuachana na mtindo wa kukusanyika bila sababu maalum na kunawa mikono kwa sabuni kwa kutumia maji yanayotiririka kila baada ya kumaliza kufanya shughuli yoyote.

Hata hivyo, Mkazi wa Kijiji cha Narakauo Kata ya Loiborsiret wilayani Simanjiro, Alais Koina, alisema taarifa ya Rais John Magufuli haijakataza kuwapo kwa minada na masoko nchini.

Koina alisema wananchi hawapaswi kujengewa hofu kwani tahadhari zilizotolewa na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, ziendelee kuchukuliwa na kuzidi kumwomba Mungu.

Diwani wa Kata ya Partimbo wilayani Kiteto, Paul Tunyoni, alisema wafugaji wote wanategemea minada kujipatia





# Akutwa amekufa mtoni

**Na Mwandishi Wetu, SIHA**

SEBASTIAN Laurent (22), maarufu Kabaka, mkazi wa Mji wa Sanya Juu wilayani Siha mkoani Kilimanjaro, amekutwa amekufa maji.

Kamanda wa Polisi mkoani Kilimanjaro, Salum Hamduni, aliiambia Nipashe jana kuwa Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi wa tukio hilo.

Kijana huyo alikutwa na wasamaria wema akiwa amekufa maji katika Mto Sanya juzi majira ya saa 10:15 jioni.

Mmoja wa mashuhuda wa tukio hilo, Fensee Kasimiri, ambaye ni rafiki wa karibu na marehemu, alidai kwamba kijana huyo amekuwa akisumbuliwa na ugonjwa wa kifafa.

"Huyu Kabaka, kabla ya kifo chake alikuwa tayari ameanguka mara tatu na ilipofika jioni ya jana (juzi), aliniambia anaenda mtoni kuoga, lakini hakurudi tena," alisema.

"Baada ya muda, tulipata taarifa kwamba rafiki yetu ameanguka mtoni na tulipofika tulikuta tayari ameshafariki. Hatujui ni kitu gani kilichomuua, tumekuta amelala tu juu ya maji."

Akizungumzia zaidi tukio hilo, Diwani wa Sanya Juu, Juma Jani (CCM), aliyefika eneo la tukio na kulazimika kuomba msaada wa polisi ili kuutoa mwili wa marehemu mtoni, aliwataka wakazi wa mji huo kuiachia mamlaka husika kufanya uchunguzi kuhusu tukio hilo na watu wasitengeneze maneno.

"Msitengeneze maneno kuhusu kifo hiki, waacheni wataalamu watasema kama chanzo ni ugonjwa wa kifafa. Ugonjwa ambao wataalamu wanasema unatokana na hitilafu au jeraha katika ubongo linalosababisha mgonjwa kuanguka, kukakamaa, kuzimia na wakati mwingine kutoa povu mdomoni," alisema.

# Maduka yafungwa kisa bei vifaa vya kujikinga corona

**Na Godfrey Mushi, HAI**

MADUKA makubwa matatu yanayouza vifaa muhimu vya kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona vinavyosababisha homa kali ya mapafu, yamefungwa wilayani Hai mkoani Kilimanjaro, baada ya kubainika kuuza barakoa na vitakasa mikono kwa bei kubwa.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Lengai Ole Sabaya, alithibitisha jana kuwa serikali kuchukua hatua hiyo ili kunusuru wanyonge dhidi ya unyonyaji kupitia bei ya vifaa hivyo.

"Tumeshayafunga maduka matatu katikati ya mji na hivi sasa bei ya kawaida imerejea katika maduka yote yenye 'masks' (barakoa) na 'hand sanitizers' (vitakasa mikono) katika wilaya yetu.

"Bado tunatafakari tutayafungua lini maduka hayo, lakini tunatafakari wamekosa utu kiasi gani kwa kufanya biashara ya ulanguzi wakati watu wako kwenye tahadhari," alisema.

Wiki iliyopita, Ole Sabaya aliamuru kukamatwa kwa wafanyabiashara watakaobainika kupandisha bei ya vifaa hivyo na kutaka maofisa biashara kufanya uchunguzi wa kimyakimya na watakapobaini, wachukue hatua ya kuyafunga maduka yote ambayo yatabainika kupandisha bei ya barakoa na vitakasa mikono.

Pia, aliagiza kufanyika kwa ukaguzi wa dharura kila siku katika maduka yanayouza vifaa vya kujikinga na maambukizo ya homa hiyo inayosababishwa na virusi vya corona.

Bei ya kawaida ya vitakasa mikono katika Wilaya ya Hai kwa sasa ni Sh. 2,500 na maski inauzwa kwa Sh. 2,000.

Kabla ya serikali kutangaza adhabu ya kuyafunga maduka yatakayobainika kupandisha bei, vitakasa mikono vilipaa sokoni kutoka bei ya Sh. 2,500 na kuuzwa kati ya Sh. 10,000 hadi 15,000 kwa pea moja.

Pia, majitiba yalikuwa yakiuzwa kwa Sh. 10,000, lakini bei yake ilipanda na kuuzwa kati ya Sh. 20,000 na Sh. 25,000.

Ugonjwa huo huambukizwa kwa njia ya hewa kwa kuingiwa na majimaji yenye virusi kutoka kwa mtu mmoja kwa njia ya kukohoa au kupiga chafya au kwa kugusa majimaji au kamasi kutoka kwa mtu mwenye virusi hivyo.

Dalili za ugonjwa huo, huanza kuonekana kati ya siku moja hadi 14 tangu kupata maambukizo.



Mbunge wa Jimbo la Kiteto, mkoani Manyara, Emmanuel Papian (kulia), akizungumza na wakazi wa Kata ya Dongo, juzi, wakati akikagua mradi wa maji uliokamilika na kuanza kutumika. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wakulima walia bidhaa kukosa soko

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

WAKULIMA wa vijiji vya pembezoni vinavyopakana kati ya Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro na Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, wameiomba serikali kutatua tatizo la muda mrefu la ukosefu wa soko la uhakika la mazao ya mboga na nafaka.

Kukosekana kwa soko hilo, kunadaiwa kusababisha hasara kubwa kwa wazalishaji ambao hutumia gharama kubwa kuzalisha na kushindwa kuuza.

Ombi hilo lilitolewa jana kwa nyakati tofauti na wananchi wa vijiji vya Msitu wa Tembo na Londoto vilivyoko wilayani Simanjiro, na Langasani, Mikocheni na Arusha Chini vilivyoko wilayani Moshi.

Mmoja wa wakulima hao, Beda Msumba, mkazi wa Msitu wa Tembo, alisema tatizo la upatikanaji wa masoko ya uhakika wa mazao wanayolima, limekatisha wengi ndoto zao kutokana na hasara wanayoipata. "Kutokana na hiyo hasara, wengi wetu tunashindwa kumudu gharama za kilimo na kulazimika kulima kilimo cha mazoea kisichokuwa na tija, badala ya kuendelea na kilimo cha kisasa.


"Tatizo la msingi kwetu linaanzia hapo ambapo tunashindwa kupata masoko ya uhakika na kusababisha kushindwa kuendelea kulima misimu inayofuata. Wakati mwingine tunalazimika kutumia mbegu ambazo tayari zilikuwa zimepandwa kama mazao ya kuuza na kuvuna mavuno kidogo," alilalamika.

Francis Mfuru, mkazi wa Londoto, alisema kwa muda mrefu tatizo la upatikanaji wa pembejeo bora na masoko, limekuwa ni kikwazo kikubwa cha wakulima kupiga hatua za maendeleo, hivyo wakaiomba serikali na wadau wa maendeleo kuwatafutia masoko ya uhakika na pembejeo bora.

Saida Ramadhan, mkazi wa Langasani, alisema: "Kwa sasa tunaiomba serikali kuangalia uwezekano wa kutoa vibali vya kusafirisha mazao nje ya nchi ili wakulima wanufaike na kurejesha mikopo katika taasisi za kifedha kama ombi hili litachelewa kutekelezwa."

Akiwajibu wananchi hao, Ofisa Masoko wa Shirika Lisilo la Kiserikali la Rikolto, linalotoa elimu ya kilimo na mnyororo wa thamani, Eliud Ng'umbi, alisema ili kukabiliana na tatizo hilo, taasisi hiyo imeanza kutoa mafunzo kwa wataalamu pamoja na wakulima wa maeneo hayo.

"Pamoja na kuwaunganisha na taasisi za fedha kupata mikopo ya kilimo, lakini tunawaunganisha na masoko kwa kuingia mikataba ya wakulima na wanunuzi kununua mazao yao," alisema.



Ukurasa 14

**DK. MAKONGORO MAHANGA 1955-2020**

## Corona inavyokoleza 'mipasho' kati ya Wamarekani na China



Ukurasa 17




Ukurasa 19

## Siasa ni kama utani wa jadi uhasama ni wa nini?


# siasa

JUMATANO MACHI 25, 2020

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU




Ukurasa 20

## Corona kirusi kilicholeta amani Mashariki ya Kati

TUME HURU YA UCHAGUZI

# Sasa imetimia miaka 28 kulilia mabadiliko

**Na Gaudensia Mngumi**

SUALA la Tanzania kuwa na tume huru ya uchaguzi ni jambo ambalo limekuwa kwenye majukwaa ya wadau wa siasa takribani miongo mitatu sasa.

Madai ya tume hiyo yalianza tangu mwaka 1992 wakati mfumo wa vyama vingi ulipoanza kutumiwa nchini kwani ilionekana kuwa ni lazima kuwa na chombo huru kinachosimamia mchakato katika mazingira ya mitizamo tofauti ya kiitikadi.

Wadau wanaotaka kuwe na tume hiyo ni pamoja na vyama vya siasa, taasisi za kidemokrasia, wadau wa maendeleo wakiwamo wanachama wa Umoja wa Ulaya (EU), Umoja wa Afrika (AU) , asasi za kirai na taasisi mbalimbali zinazohimiza masuala ya kidemokrasia.


**INAENDELEA UK.16**





Rais mstaafu Benjamin Mkapa, miaka sita baada ya kuanza mfumo wa vyama vingi aliunda Tume ya Jaji Kisanga mwaka 1998. Mwenyekiti wa NEC mstaafu , Jaji Damian Lubuva, ndiye aliyetangaza matokeo ya urais mwaka 2015.. **PICHA: MTANDAO.**

## Jenerali Tumukunde anayepania kumng'oa Rais Museveni Ikulu

Ukurasa 18

# SAFARI YA DK. MAKONGORO MAHANGA 1955 HADI 2020

• Muasisi wa majimbo Ukonga na Segerea • Alibobea uhasibu na ugavi kwa mpigo • Aliibukia siasa ghafla na akang'ara



Dk. Makongoro Mahanga (kulia) aliponadiwa kwa mara ya kwanza alipowania ubunge. **PICHA: MTANDAO**

**Na Sabato Kasika**

JUZI asubuhi, kama ilivyo kawaida ya mitandao ya mawasiliano nchini na kimataifa, ilivyo 'fasta' ni taarifa nyingine ya kifo cha Dk. Milton Makongoro Mahanga, mkazi wa Tabata Segerea, vilevile aliyewahi kuwa mbunge wa jimbo la Ukonga na hata pale lilipogawanywa, aliwania nafasi hiyo kwa jimbo la nyumbani kwake Segerea.

Hili ni pigo, kwa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kwani hadi taarifa ya msiba, uliotokea katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), jijini Dar es Salaam, alikuwa mwenyekiti wa chama hicho, Mkoa wa Ilala.

Katibu wake mkoani Ilala, Jerome Olomi, alithibitisha kutokea kwa kifo hicho taarifa za awali wakizipata kutoka kwa mke wake.

Ni wastani wa takriban miongo miwili sasa, kwa maana ya miaka 20 kasoro miezi kadhaa tangu aanze kuonekana na kung'ara katika anga za siasa nchini.

Huenda kutokana na sababu mbalimbali kama vile umri, ufuatiliaji kwa hatua na weledi wa namna mbalimbali vinawafanya watu kumfahamu Dk. Mahanga kuanzia ngazi tofauti za miaka; Kuna wanaomfahamu kuanzia siasa za uchaguzi mwaka 2000, wengine alipobeba jina kubwa la naibu waziri.

> Ndani ya zama zote ametumikia nafasi ya naibu waziri, hususan katika Wizara ya Kazi na Ajira.

Pia wapo walioanza kumfahamu, pale alipokipa kisogo Chama Cha Mapinduzi (CCM) na kujiunga na Chadema, akiwa sehemu ya "timu Lowassa", kupitia yale yaliyojiri katika kumsaka mgombea urais kwa tiketi ya CCM, ambayo undani wake hauna jipya la kuwasimulia wengi leo hii, katika siasa.

### ALIKOIBUKIA

Huko nyuma kabla ya mwaka 2000, hakuwahi kusikika, kuwa na jina linalotamba kitaifa kwa kiwango alichoonekana kisiasa, na hata kwa wanamjua, hakutabiriwa hata siku moja kwamba angejitosa kwenye siasa kubwa, eneo lililomeza jina lake hadi umauti.

Kwa kudodosa wasifu wake, huyu ni msomi aliyeshiba kitaaluma 'kisawasawa' hasa katika eneo la menejimenti na kwa 'kumchimba' zaidi, taaluma aliyosimama nayo kwa kina, ni fani ya ugavi, ambayo msingi wake aliupata katika Chuo cha Nyegezi Mwanza, ambacho sasa ni Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino (SAUT).

Dk. Mahanga, alizama zaidi katika taaluma hiyo na kupata cheti cha juu zaidi ya taaluma, kinachotolewa na Bodi ya Taifa ya Usimamizi wa Vifaa (NBMM), kiitwacho CSP (Certified Supplies and Purchasing Proffesion).

Ikumbukwe katika kipindi hicho, NBMM ikiwa ni taasisi changa, Dk. Mahanga ni miongoni mwa walaaluma wachache wa Kitanzania waliokuwa mhimili wa bodi hiyo.

Baadaye katika kujiendeleza, mwanasiasa huyo aliweka rekodi ya kipekee nchini pale alipoamua kuzama kusomea 'fani ndugu' na ugavi ambayo ni uhasibu, hata akakipata cheti cha juu kabisa cha uhasibu kinachofanana na CSP, hicho ni CPA (Certified Public Accountant), kinachotolewa na Bodi ya Taifa ya Uhasibu na Ukaguzi wa Hesabu (NBAA).

Umaarufu wake ndipo ukaanza kujidhihirisha katika ngazi ya umma, kwani itakumbukwa, mwazoni mwa miaka ya 1990 alipoajiriwa kuwa Mhasibu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Ilikuwa ni rekodi ya aina yake, msomi mwenye vyeti vya pande mbili kuajiriwa kusimamia fedha za wasomi wenzake, tukio la kuajiriwa kwake kwa wasifu huo hata UDSM, ikatoa taarifa katika vyombo vya habari kujigamba imepata mhasibu mkuu aliyetukuka.

Hata hivyo, hakudumu sana chuoni hapo, baadaye alihama na kuajiriwa kama mkuu wa idara mojawapo ya Shirika la Nyumba Tanzania (NHC), huku kitaaluma akipiga hatua zaidi kwa kusomea Shahada ya Uzamili katika Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM), akiwa ni miongoni mwa wanafunzi wa awali kabisa tangu ngazi hiyo ya elimu kutolewa chuoni hapo.

Kuhusiana na wasifu wake, wa Shahada ya Udaktari wa Falsafa (Phd), kulishatokea mjadala wa kisheria, ambao pia uliwahusu baadhi ya wanasiasa wengine, kati yao wapo waliolazimika ku-

INAENDELEA UK.15

# SAFARI YA DK. MAKONGORO MAHANGA 1955 HADI 2020

INATOKA UK.14

rudi darasani tena kuweka sawa uhalali wake.

**AJITOSA SIASA**

Mwaka 2000, kukiwapo vuguvugu zinazojitosheleza za siasa, katika jimbo jipya la Ukonga, lililogawanywa kutoka Ilala, mara hii Dk. Mahanga, wakati huo akiwa na umri wa miaka 45, aliamua kuweka kando menejimenti aliyokuwa akiitumikia NHC, akiwania utawala wa kisiasa.

Hapo hasa ndipo jina lake lilipea kitaifa. Kwanini? Kwanza hakuna hata mmoja aliyemfahamu kwamba ni machachari hasa wa kisiasa, kuanzia kampeni za ndani za CCM kumsaka mgombea, hata akawapelekesha mbio wenye majina makubwa waliowania nafasi hiyo, wakongwe waliozaliwa ndani ya siasa hata wakiwa katika umri wa kuzeeka, aliwamudu.

Pale alipopitishwa na CCM kuwa mgombea wake jimboni Ukonga, vibweka vyake vya kampeni vinavyodaiwa viliendana na 'uwekezaji' mkubwa, vilikuwa na mafanikio makubwa.

Mtumishi mwenzake kutoka NHC, Khadija Kusaga, ambaye naye ameshatangulia mbele ya haki, alijitosa jimboni Temeke kwa mafanikio ingawa yake yalikuwa tofauti kidogo, kwa maana ya kuyatolea jasho jingi.

Ulikuwa wakati mgumu katika kampeni za Khadija, hata kuna wakati alilazimika kuja na staili mpya ya kuomba kura kwa kupiga magoti, ikiwa ni ishara ya namna fulani ili wapigakura wamuone kwa jicho la huruma kisiasa.

Jimbo la Ubungo nalo safari hiyo lilimpata mgombea wa CCM, mtendaji mwandamizi wa kiserikali katika halmashauri mbalimbali kitaifa, mara ya mwisho akiwa ni Mwenyekiti wa jiji la Dar es Salaam, Charles Keenja, ambalo wakati huo halmashauri ilikuwa imevunjwa, baada ya kukamilisha wajibu akaibukia katika siasa za ubunge.

Kuna wakati kampeni hizo zikiwa 'zimenoga' kila mmoja akifanya tathmini za ndani; Keenja na Dk. Mahanga, wanaona viashiria vya mambo mazuri, walilazimika mara kadhaa kwenda 'kumsapoti' Khadija kwenye kampeni zake Temeke, mshindani wake mkuu akiwa ni Richard Hizza Tambwe wa Chama cha Wananchi (CUF), naye kwa sasa ni marehemu.

Ubunge wake ulimpatia majibu ya manufaa, hata akakwea kuwa naibu waziri. Ulipofika uchaguzi unaofuata mwaka 2005, Dk. Mahanga alifanikiwa kutetea tena kiti chake, lakini safari hii akipata mchuano mkali kuanzia kura za maoni ndani ya CCM.

Kama kuna kipindi, mwanasiasa huyo alianza kushuhudia ugumu wa siasa za uchaguzi ni mwaka 2010, akiwa katika jimbo jipya la Segerea, kuzipata kura za wakazi wa maeneo anakoishi kwa maana ya Kifuru, Segerea na pande zote za Tabata ilikuwa ngumu kwake.

Kwa kutumia stadi za kisiasa, akishirikiana na wenye weledi kutoka ndani ya chama chake, kwa kiasi kikubwa, aliwekeza katika maeneo ambayo yeye na chama chake walikubalika zaidi, mathalani Buguruni na Vingunguti na kunufaika na idadi kubwa ya wapigakura, alifanikiwa kutetea ubunge wake kwa mara ya tatu.



Dk. Makongoro Mahanga alipokuwa Chadema. **PICHA: MTANDAO**

> Wao ndiyo wanaojua kama Chadema ni mzigo wa maji kwenye gunia au ni mwamba na jabali unaokwenda kuibomolea mbali CCM mwaka huu. Ati gunia la maji?

Zilipofika siasa za uchaguzi ndani ya CCM na sintofahamu katika kumtafuta mgombea urais wa chama hicho, hata kukatokea mgawanyiko, Dk. Milton Makongoro Mahanga, alikuwa miongoni mwa waliomsaidia Edward Lowassa, kuinua jamvi lao wakisonga kuelekea Chadema, kuanza maisha mapya.

Ndani ya zama zote ametumikia nafasi ya naibu waziri, hususan katika Wizara ya Kazi na Ajira.

**MSIMAMO WAKE**

Mwaka 2015 kulikuwa na wimbi kubwa la wanasiasa na hasa wa CCM wakiwamo vigogo, ambao walihamia Chadema.

Katika uhai wake amewahi kukaririwa na vyombo vya habari akizungumzia hatua ya vigogo wenzake kurudi CCM na kusema, walikosa kilichopeleka upinzani lakini yeye hakuwa na mpango huo.

"Siwezi kurubuniwa, kununuliwa, siwezi kurudi CCM, kwa sababu sijaja Chadema kwa sababu ya cheo, mimi nilikuwa waziri, niliacha uwaziri bado kuna miezi mitatu mbele, mawaziri huwa wanakwenda mpaka Novemba siku wakati rais anaapishwa mimi nilitoka mwezi wa nane kwa hiyo mawaziri wenzangu waliendelea, mwishoni huwa kuna viposho, lakini mimi nikaviacha. Sikuja Chadema kutafuta cheo," alikaririwa enzi ya uhai wake.

Mbali na hilo, hata kwenye uchaguzi ndani ya Chadema uliofanyika Desemba mwaka jana, Dk. Mahanga alitoa neno kuhusu baadhi ya wanachama wa chama hicho waliokosa nafasi na kurudi CCM.

Dk. Mahanga alisema, Chadema imekua na itaendelea kubebwa na viongozi, wanachamana wafuasi mahiri waliokubali kwa dhati itikadi falsafa na dira ya chama hicho bila kuweka mbele maslahi yao binafsi.

"Wao ndiyo wanaojua kama Chadema ni mzigo wa maji kwenye gunia au ni mwamba na jabali unaokwenda kuibomolea mbali CCM mwaka huu. Ati gunia la maji? Ningekuwa bado kijana ningemjibu," alisema.

Hizo ni miongoni mwa kauli zake za mwisho alizotoa mwaka huu akiwazungumzia wanachama waliokosa uongozi ndani ya Chadema na kuamua kurudi CCM huku wakilalamika.

**ULIMI WATELEZA**

Katika kampeni za uchaguzi mdogo wa jimbo la Ukonga, Dk. Mahanga alikuwa miongoni mwa wapigadebe wa Chadema wakimnadi mgombea wa chama hicho, Asia Msangi, aliyekuwa akichuana na Mwita Waitara.

Jimbo la Ukonga lilikuwa wazi tangu Julai mwaka 2018, baada ya aliyekuwa mbunge wake, Mwita Waitara (Chadema) kuhamia CCM na hivyo kulazimika kufanyika uchaguzi mdogo.

Dk. Mahnga aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo kwa miaka 10 kuanzia mwaka 2000 hadi 2010 akiwa CCM, alikaririwa na vyombo vya habari akitamka ulimi na kudai kwamba aliongoza jimbo hilo 'kwa kununua kura'.

Akawataka wananchi wa Ukonga wasikubali tena kuuza kura zao na badala yake wamchague mgombea kupitia Chadema, lakini kauli hiyo ikapingwa vikali na CCM kwamba anadhalilisha elimu yake.

***Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. Amina.***

TUME HURU YA UCHAGUZI

# Sasa imetimia miaka 28 kulilia mabadiliko



Bunge Maalumu la Katiba likiwa kazini jijini Dodoma mwaka 2014, kujadili rasimu ya Warioba. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**INATOKA UK.13**

Hata sasa, taifa linapoelekea kwenye uchaguzi mkuu wa Oktoba mwaka huu, vyama vya upinzani vinaendeleza dai hilo na Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe, ameanza kuiibua tena haja ya kuwa na tume ya huru ya uchaguzi.

Mapema February 6, 2020 akiwa bungeni jijini Dodoma, Mbowe Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, anamuuliza Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, swali la papo kwa papo ni lini Tanzania itakuwa na tume huru ya uchaguzi?

Akijibu, Waziri Mkuu anasema tume iliyoko leo ni huru na hata kikatiba tume hiyo iko huru, hivyo itaendelea na kazi zake.

Wiki hii, watendaji na viongozi wa vyama vya siasa pamoja na Tume ya Uchaguzi (NEC) wameibua tena hoja ya tume huru, wakiitaka NEC ithibitishe kwa matendo, tamko la Rais John Magufuli, kuwa uchaguzi wa 2020 utakuwa huru na haki.

Pamoja na Rais kutoa ahadi hiyo kwenye kuukaribisha mwaka mpya wa 2020, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Profesa Palamagamba Kabudi, akiwa Uswisi, aliiahidi jumuiya ya kimataifa kuwa uchaguzi wa mwaka huu utakuwa wa haki na uhuru.

> Kwa hiyo ni wazi kuwa dai la kuwa na tume huru ni kilio cha wadau wengi na si kwamba ni jambo linaloibuka sasa wakati taifa likielekea kwenye uchaguzi huo.



Mwenyekiti wa NEC mstaafu, Jaji Damian Lubuva, ndiye aliyetangaza matokeo ya urais mwaka 2015.



Jaji Joseph Warioba, Tume yake iliainisha namna ya kupata tume huru ya uchaguzi. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**KUTAKA MABADILIKO**

Pamoja na wapinzani hasa Mbowe kuzungumzia suala la tume hiyo zama hizi, ni wazi historia ya mabadiliko ya kutaka kuwa na tume huru hayajaanza leo wala si madai ya Chadema, hata Kamati ya Jaji Robert Kisanga ya mwaka 1998, ilipokusanya maoni ya wananchi kuhusu masuala ya katiba, ilitaka kuundwa kwa chombo huru cha kusimamia uchaguzi.

Hata hivyo, rais wa wakati huo, Benjamin Mkapa, hakutekeleza mapendekezo ya Kamati ya Kisanga na mambo yakabaki kama yalivyo.

**TUME YA WARIOBA**

Tume ya Mabadiliko ya Katiba iliyoongozwa na Jaji Joseph Warioba, iliyofanyakazi mwaka 2013, ilipendekeza kuwa na tume huru ya uchaguzi na ikaanisha mchakato wa namna ya kuipata.

Ibara ya 190 ya rasimu ya Warioba inaainisha namna ya kuundwa tume huru ya uchaguzi ikionyesha taratibu za kuwapata wajumbe kwa uwazi kupitia utaratibu wa kuomba nafasi hizo na pia kuchujwa na Kamati ya Uteuzi kabla ya kuteuliwa rasmi na rais kuwa mwenyekiti makamu, au makamishna wa tume hiyo.

Aidha, kupitia Rasimu ya Warioba, wananchi wanatoa maoni ya muundo wa tume wakitaka mwenyekiti, makamu wake na makamishna au wajumbe wa tume hiyo wathibitishwe na bunge.

Aidha, rasimu hiyo inapendekeza kuwa pengine si jambo jema mbunge, wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, au la Tanzania au mjumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar kuteuliwa kuwa mjumbe wa tume huru.

Aidha, ibara ya 191 ya rasimu hiyo inawataja wajumbe wa kamati ya uteuzi ambao ni pamoja na Majaji wakuu wa Tanzania na Zanzibar, Maspika Bunge na Baraza la Wawakilishi na Mwenyekiti wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

Halikadhalika, ibara ya 194 inaeleza kuhusu namna ya kushughulikia kesi za uchaguzi na kupendekeza zifunguliwe Mahakama Kuu mapema iwezekanavyo baada ya tume huru ya uchaguzi kutangaza matokeo.

Aidha, ibara ya 195 inapendekeza namna ya kumteua Mkurugenzi wa Uchaguzi, ambaye atateuliwa na Rais baada ya kupendekezwa na Tume ya Utumishi wa Umma na kuthibitishwa na Bunge. Pia, inaweka vigezo na sifa za kuwa mkurugenzi wa uchaguzi.

Hata hivyo, rasimu ya katiba ya Warioba, haikukubaliwa na mchakato wa kupata katiba mpya haukukamilika hadi sasa na suala hilo likabakia kama lilivyo.

**TUME HURU NININI?**

Ibara ya 74(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiyo inayounda tume ya sasa na inatamka kuwa kutakuwa na tume ya uchaguzi na wajumbe wake watateuliwa na Rais, ambao ni pamoja na Mwenyekiti , Makamu na wajumbe wengine, lakini pia hata Mkurugenzi wa Uchaguzi anateuliwa na Ikulu.

Hilo ndilo wapinzani, wadau wa uchaguzi wakiwamo wapiga kura wanalolilalamikia wakisisitiza kuwa kuna haja ya mabadiliko na kwa ujumla kinacholalamikiwa kuhusu tume hiyo inayozungumzwa tangu mwaka 1992 hadi leo ni namna ya kupata wajumbe wa tume hiyo.

Kinachogomba kwa mujibu wa Mbowe na wadau wengine wa siasa ni namna ya kuwapata wajumbe wa tume hiyo, ambayo imeanishwa kwenye ibara ya 74 (1).

Wapinzani wanachokisimamia ni kutaka kuwe na utaratibu mwingine wa kuwapata wajumbe wa tume ya uchaguzi tofauti na huu wa sasa ambao, wote huteuliwa na Ikulu.

**KUPINGA MATOKEO**

Suala ambalo linazungumzwa na wadau wa siasa na wapinzani mara kwa mara ni pamoja na kutaka matokeo ya uchaguzi wa urais yapingwe mahakamani.

Kwa mujibu wa sheria za uchaguzi na katiba ya Tanzania, matokeo ya urais yakishatangazwa na tume hayaruhusiwi kuhojiwa au kupingwa mahakamani kwa namna yoyote ile.

Lakini, kwa upande wa vyama vya upinzani vinasisitiza kuwa hakuna sababu ya kukataza matokeo hayo kupingwa mahakamani kwani yote hiyo ni michakato ya kidemokrasia.

Upinzani unaamini kuwa ni haki ya wapiga kura, wagombea wa urais kueleza malalamiko yao na kusema yale wanayodhani ni kasoro kwenye uchaguzi huo kwa vile yote hiyo ni michakato ya kidemokrasia.

**UMUHIMU**

Kwa mtizamo mwingine uchaguzi ni mchakato ambao una wadau wengi kuanzia, wapiga kura, wagombea, vyama vya siasa wapinzani na kinachotawala , taasisi za kidemokrasia, waangalizi wa uchaguzi wa ndani na nje ya nchi, Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika, jumuiya za kikanda na mataifa wahisani.

Iwapo wadau wengi wanataka kuwe na chombo hicho au tume huru pengine wanaona kuwa mchakato hauwafurahishi na wanafikiria kuwa tume iliyopo inatakiwa kuboreshwa zaidi hivyo pengine suala hilo linahitaji kujadiliwa.

Ni vyema kusikilizana na kufanya uamuzi kwani ni kilio cha miaka 30 sasa.

**TAKWA LA AFRIKA**

Baadhi ya masuala yanayotajwa kwenye mtangamano wa Afrika (AU) ni umuhimu wa kuzingatia demokrasia, utawala wa sheria na kuheshimu haki za binadamu.

AU ina Mkataba wa Afrika wa Demokrasia, Uchaguzi na Utawala Bora (ACDEG) na suala la kuwa na tume huru za uchaguzi kwa wanachama wa AU linasisitizwa.

Sura ya Saba ya ACDEG, inawaagiza wanachama wa Umoja wa Afrika kuwa na tume huru na vyombo huru vya kusimamia uchaguzi. Aidha, inaeleza kuwa vyama vya siasa viwe na wajibu wa kukubali matokeo au pale vinapoona mambo hayajakaa sawa vinaweza kuyakataa matokeo ya uchaguzi kwa kutumia taratibu na sheria zilizopo. Inataka yafikishwe mahakamani na kuhojiwa.

Kwa hiyo ni wazi kuwa dai la kuwa na tume huru ni kilio cha wadau wengi na si kwamba ni jambo linaloibuka sasa wakati taifa likielekea kwenye uchaguzi huo.

**VIPI MUDA?**

Wakati huu suala hili huchagizwa na upinzani hasa Chadema kwa kutaka umuhimu wa kipekee wa tume hiyo kabla ya Oktoba 2020 kwenye uchaguzi mkuu.

Kinachojiri ni je, muda unatosha kwa uchaguzi wa 2020, ikiwa imebakia miezi sita mchakato huo unaweza kufanyika? Na kwa vile hitaji la msingi la kisheria ni kufanya marekebisho ya katiba ili kuwa na tume hiyo ambayo msingi wake ni katiba itawezekana?.

Kwa vile kila mmoja anaona uchaguzi umekaribia pengine ni wakati wa wadau wa uchaguzi kuanzia vyama vya siasa, serikali, chama tawala , bunge, baraza la wawakilishi na mihimili mingine ukiwamo wa sheria kukaa na kukubaliana kuhusu kusogeza mbele uchaguzi na kuboresha muundo wa tume au kueleza michakato mingine.

Ni jukumu la wadau hao kueleza iwapo wanaona umuhimu wa kusogeza mbele uchaguzi huo ili kuandaa muswada wa sharia wa kurekebisha katiba na kuuwasilisha bungeni na kwenye baraza la wawakilishi pengine kwa hati ya dharura ili kuandaa sharia ya kurekebisha katiba hiyo itakayosainiwa na Rais ili iwe sheria na mchakato uanzishwe.

> Ni vyema kusikilizana na kufanya uamuzi kwani ni kilio cha miaka 30 sasa.

Pengine ni vyema kujadiliana na kuona lipi linawezekana kwa wakati huu, kuliko kwenda kwenye uchaguzi huku baadhi ya wadau wakinung'unika na kutaka kuwe na mabadiliko ya tume ambacho ndicho chombo kinachosimamia uchaguzi huo.

Hata hivyo, hilo ni suala ambalo linawahusu wadau wote pamoja na baadhi ya wananchi wanaoona kuna umuhimu wa kuwa na marekebisho au viraka kwenye katiba ili kufanya marekebisho kwenye tume hiyo.

Je wadau hawaoni kuwa ni muda wa kushauriana na kutoa maelezo ya kilio hicho katika kusaka maridhiano na kujenga umoja na uvumilivu wa kisiasa na kitaifa?

## Corona inavyokoleza 'mipasho' kati ya Wamarekani na China



Trump kushoto na hasimu wake Rais wa China, Xi Jinping. **PICHA: BBC**

NI wazi kuwa sasa dunia iko katika wakati mgumu ina uhusiano kati ya Marekani na China haujatengamaa.

Rais Donald Trump wa Marekani amekuwa akitoa matamshi ya mara kwa mara ya kejili kuwa virusi vya corona ni "virusi vya China"-'China virus'.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Mike Pompeo naye anaviita "virusi vya Wuhan", kwenye jimbo la Wuhan ndiko chimbuko la COVD 19 , jambo ambalo pia limeikera sana China.

Rais na waziri wa mambo ya nje wote wanailaumu China kwa kushindwa kukabiliana na mlipuko huu, lakini msemaji wa China amekanusha madai yao na kusema kuwa waliokuwa China walishuhudia kuwa ilikuwa wazi katika tatizo hilo kuanzia mwanzo kabisa.

Kwa sasa kwenye mitandao ya kijamii kuna tetesi zinazodai kuwa ugonjwa huu umesababishwa na mpango wa wanajeshi wa Marekani.

Wakati wanasayansi wanapinga madai hayo na kusema kuwa ugonjwa huo virusi vyake ni vya asili na hakuna aliyevitengeneza, kila mmoja anamini lake.

Lakini, hii si vita ya maneno peke yake, kuna mapambano zaidi yanayoendelea.

Mapema mwezi huu, wakati Marekani ilipotangaza kufunga mipaka yake yote kwa wasafiri wengi wa mataifa ya bara la Ulaya, Italia ikiwemo serikali ya China imetangaza kutuma vifaa tiba Italia, taifa ambalo linaongoza kwa maambuizi mengi ya virusi vya corona au COVID 19.

China imetuma msaada wa kukabiliana na corona kwa nchi za Iran na Serbia pia. Ni wakati ambao tunaona ishara kubwa, China inasema.

Hii ni ishara ya mapambano ya taarifa kwa kile ambacho kiko nyuma ya pazia, huku China ikiwa inapata unafuu katika janga hili lakini janga limegeuka kuwa la dunia.

China inaongeza kuwa kiukweli, mapambano haya kwa Marekani, ni wakati ambao inabidi washushe mikono yao chini.

Taarifa zinasema msaada wa vifaa tiba wa ndege ndogo ya vita ya Marekani nchini Italia ni mgumu kuwa msaada wa kutosha.

Huu ni wakati mgumu ambao mamlaka na mfumo wa kisiasa katika mataifa yote yanakabiliana nao na hawajawahi kukutana na hali kama hii hapo kabla.

Viongozi watakuwa katika hali ngumu ya kiuchumi na kwamba viongozi ambao wako madarakani watalaumiwa kwa kushindwa kuabiliana na tatizo hili, ufanisi wao katika uongozi utahukumiwa na watu kwa kushindwa kukomboa nchi zao kutoka katika ugonjwa huu mpya.

Ugonjwa wa corona umekuja wakati ambao Marekani na China walikuwa tayari katika uhusiano ambao si mzuri. **BBC**

# Jenerali Tumukunde anayepania kumng'oa Rais Museveni Ikulu



Henry Tumukunde (kushoto) na hasimu wake wa kisiasa- Museveni. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mashaka Mgeta**

MGOMBEA urais wa Uganda, Jenerali (mstaafu) Henry Tumukunde, ni miongoni mwa watiania wanaojitokeza kuwania urais katika uchaguzi mkuu unaokuja, wakiwa na historia ndefu ya kupambana na kiongozi wa taifa hilo aliyetokea msituni mwaka 1986.

Tumukunde bado anaamini kwamba pamoja na majaribu aliyoyapitia kwa nyakati tofauti, tangu alipokuwa mbunge akiliwakilisha jeshi, kuteuliwa kuwa waziri na baadaye 'kutumbuliwa', bado ana uwezo wa kumuondoa Museveni madarakani.

Ingawa wapo wagombea 'lukuki' waliojitokeza kupambana na Museveni kwenye kinyang'anyiro hicho, lakini Jenerali Tumukunde anaendelea kuweka historia ya wale wanaopata kadhia mbalimbali ikiwamo kukamatwa na kuwekwa ndani, katika hali inayohusishwa na harakati za kisiasa.

Miongoni mwa matukio yaliyomsibu ni pale alipokamatwa nyakati za usiku na timu ya pamoja na walinzi na wana-usalama iliyongozwa na Mkuu wa Idara ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai (CID) Grace Akullo.

Timu hiyo iliyowajumuisha pia maofisa kutoka kitengo cha intelijinsia cha jeshi la nchi hiyo ( (CMI), ilivamia ofisi binafsi za Jenerali Tumukunde zilizopo Kololo jijini Kampala wakiwa na waranti ya kumpekua na kumkamata.

Hata hivyo, mwanajeshi mstaafu Tumukunde, aliyewahi pia kuwa Waziri wa Usalama kwa kipindi cha kati ya 2016 na 2017, alitaka kuwapo mwanasheria wake, lakini alijikuta akiburuzwa kwenda ofisi za Makao Makuu ya CID huko Kibuli, umbali wa kiasi cha kilomita nne.

> Kukamatwa kwake kunahusiana na kauli ya uchochezi alizozitoa kwenye mfululizo wa mahojiano kupitia vituo cya redio na runinga, zinazoweza kuchochea chuki na kusababisha machafuko, uchochezi na kuibua vurugu kwa ujumla.

Baadaye alisafirishwa kwenda kitengo mahususi cha upelelezi kilichopo Kireka, kwenye wilaya jirani ya Wakiso na kushikiliwa kwa usiku huo.

Kwa mujibu wa taarifa ya polisi, Jenerali Tumukunde, alistahili kushtakiwa kwa tuhuma za uhaini wa matamshi (treason for utterances) alizozitoa wakati akihojiwa kwenye kituo cha runinga, akionekana kuunga mkono hatua ya Rwanda kuingilia siasa za Uganda.

"Kukamatwa kwake kunahusiana na kauli ya uchochezi alizozitoa kwenye mfululizo wa mahojiano kupitia vituo cya redio na runinga, zinazoweza kuchochea chuki na kusababisha machafuko, uchochezi na kuibua vurugu kwa ujumla."

"Pia alielezea kutafuta msaada kutoka nchi jirani, kumsaidia ili afanikishe kuiondoa serikali iliyopo madarakani kwa kupitia ama pasipokuwa sanduku la kura." Akasema Msemaji wa Polisi, Fred Enanga.

Siku chache kabla ya kutimuliwa kazi na Rais Museveni mwaka juzi, Jenerali Tumukunde alishiriki maziko ambapo katika salaam zake za rambirambi, alimpongeza mpinzani mkuu wa Rais Museveni, Kanali Kizza Besigye kwa kumuita kuwa ni kiongozi mashuhuri aliyepo.

### KABLA KUTUMBULIWA

Hata kabla ya kutumbuliwa kwake, Jenerali Tumukunde alishashiriki matukio makubwa mawili. Mwaka 2015-16 aliwania urais, akishindana kwa karibu sana na aliyewahi kuwa Waziri Mkuu, Amama Mbabazi, wakitaka 'kunyakua kitumbua cha urais' kutoka kwa Museveni.

Baada ya uchaguzi huo, ndipo alipoteuliwa kuwa Waziri wa Usalama katika baraza la mawaziri la awali baada ya ushindi wa Rais Museveni.

Baada ya kuenea kwa taarifa kwamba aliondolewa walinzi wake watatu, hisia za kwamba atawania urais zilizoibuka miongoni mwa Waganda.

### KUTANGAZA NIA

Alipokuwa akisherehekea miaka 61 ya kuzaliwa kwake, Februari 28, 2020 Jenerali Tumukunde aliiandikia Tume ya Uchaguzi akiijulisha nia yake ya kuwania urais katika uchaguzi mkuu ujao.

Ingawa vyombo vya habari vya Uganda vinamtaja kama 'Ofisa Mwandamizi wa Jeshi' mwingine anayetaka kumuondoa Museveni kutoka madarakani kupitia uchaguzi mkuu, amekuwapo hapo kwa takribani miaka 16 iliyopita, akiwa wa pili kutoka kwa Besigye aliyeshiriki kinyang'anyiro hicho kwa kipindi cha ndani ya miaka 20 sasa.

Uhusiano wa 'mabwana wa vita ya msituni' hao Tumukunde na Museveni, ulianza kudorora mwaka 2004, ilipowekwa wazi kwamba mabadiliko ya Katiba yalipaswa kufanyika ili kuondoa ukomo wa awamu mbili za utawala wa Rais aliyepo madarakani.

### KUANZA UPINZANI

Kiongozi huyo alikuwa mbunge akiwakilisha jeshi bungeni, alijitokeza hadharani na kupinga mpango huo wa kuondoa ukomo wa kipindi cha rais madarakani.

Alilazimishwa kujiuzulu kutoka bungeni, akakamatwa na kufunguliwa mashtaka kwenye mahakama ya kijeshi kwa kueneza propaganda chafu akitumia majukwa yasiyo sahihi.

Kwa hali hiyo, inaweza kutafsiriwa kwamba Jenerali Tumukunde amekuwa mpinzani wa Rais Museveni kwa kipindi kirefu kuliko Besigye ambaye mara kadhaa ameadhibiwa kwa kuhusishwa na kumpinga Museveni.

### KATIBA YA 2005

Kama mabadiliko ya kuondoa ukomo wa urais yasingepitishwa kama Jenerali Tumukunde alivyoyapinga, utawala wa Museveni ungeweza kufikia ukomo wake mwaka 2006, takribani miaka 14 iliyopita.

Kwa hivi inafahamika rasmi kwamba baada ya kuenguliwa kwake kutoka kwenye uwaziri mwaka 2018, Jenerali Tumukunde aliwekeza zaidi katika mradi wake wa kuusaka urais wa Uganda.

Azma ya Jenerali Tumukunde kuwania urais inarejesha nyuma kumbukumbu ya mwaka 2000-2001 wakati umma wa Uganda ukitajwa kutaka kuiona 'damu mpya' ikimuondoa Museveni madarakani, ndipo alipotokea Besigye aliyempiku Aggrey Awori.

Sasa, Jenerali Tumukunde akiwa na wadhifa wa kijeshi anakutaka na changamoto ya mgombea mwingine mwenye damu changa- Bobi Wine anayegusa hisia za Waganda mara kadhaa pengine zaidi na ilivyokuwa kwa Awori mwaka 2000. Swali linabaki kuwa, je, Jenerali Tumukunde ataweza kushindana na Bobi Wine ama atakuwa tayari kuunganisha nguvu ili kufanya kazi pamoja?

Kwa ufupi, Jenerali Tumukunde bado ana futsa nyingi zinazompa uzoefu wa kuimudu kazi ya urais kwa kuaminiwa, ikiwamo uzoefu wake kwenye jeshi na masuala mengine ya kikanda na kimataifa.

Wanamapinduzi wa jana ni wazee wa sasa lakini bado wana 'makonde' mazito. Wanahitaji utulivu ambao Bobi Wine hawezi kuwathibitishia raia wa Uganda. Wanahitaji pia ukuaji uchumi wenye kuzingirwa na siasa kidogo na wingi wa usimamizi bora wa masuala ya kiraia, tofauti na ilivyo kwa utawala wa Museveni.

Pia wanahitaji Museveni astaafu kwa amani kama inavyotokea kwa nchi majirani za Tanzania na Kenya. Lakini je, wingi wa vijana wanaotaabika kwa kukosa ajira watakuwa tayari kumpigia kura ya ndio?

### KUFUKUZWA KAZI

Mwaka 2018, Rais Museveni alimtumbua, Jenerali Tumukunde kutoka kwenye baraza la mawaziri, pamoja na aliyekuwa Mkuu wa Polisi, Jenerali Kale Kayihura.

Hata hivyo, wanaharakati walipongeza hatua ya kuondolewa ofisini kwa Jenerali Kayihura kwa madai kwamba alipokuwa kwenye wadhifa huo, alizingirwa na shutuma za kutesa watu na kuzuia maandamano ya raia.

Akizungumzia hatua hiyo, Rais Museveni aliweka wazi kutoridhishwa na uwezo wao wa kukabiliana na uhalifu. Ingawa ni hivyo, Jenerali Tumukunde aliongoza kampeni dhidi ya 'mjeshi' mwenzake, Kayihura-lakini wote wawili wakatumbuliwa.

***Makala haya yameandikwa kwa msaada wa vyanzo mbalimbali vya kwenye mtandao.***



Mkusanyiko kama huu wa wana-CCM hautakuwa na mshindani iwapo Mwenyekiti wa Chadema Freeman Mbowe na wafuasi wake hatakuwapo kutoa ushindani na changamoto za kisiasa. **PICHA MTANDAO.**

# Siasa ni kama utani wa jadi uhasama ni wa nini?

**Na Mwal. Magabilo Masambu**

KATIBA ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inakumbusha kuwa hii ni nchi inayofuata misingi ya demokrasia, inayozingatia haki ya kijamii na kwa hiyo-wananchi ndiyo msingi wa mamlaka yote na serikali inapata madaraka na mamlaka kutoka kwa wananchi.

Kutokana na maelezo hayo ya katiba ni wazi kwamba nchi zote zinazozingatia uongozi wa kidemokrasia nguvu ya madaraka hutoka kwa wananchi. Hii inamaanisha kuwa wananchi ndiyo wenye nchi ndiyo wanaowachagua viongozi kupitia sanduku la kura.

Kwa hiyo ni muhimu sana kuheshimu maamuzi ya wananchi na kuzingatia demokrasia. Kuzingatia demokrasia huko kutatokana na watu wote ndani ya nchi kuamini kuwa taifa halina mmiliki maalumu bali wamiliki ni raia wenyewe.

Ikiwa kila mmoja atatambua kwamba demokrasia ndiyo msingi wa maendeleo utakuwa ni mwanzo mpya wa kuepusha mapigano ya wenyewe kwa wenyewe na chuki zinazotokana na migogoro ya kisiasa. Kuheshimu demokrasia ni kuwajengea watu uzalendo katika taifa, maana wataona hakuna sababu ya kupigana na kuiharibu nchi ambamo kila mmoja wao anaishi, badala yake wataungana kujenga na kupenda taifa lao.

### SIASA KAMA SOKA?

Siasa si uadui tuifanye kama soka. Mathalani, siku ya mechi ya Simba na Yanga Uwanja wa Taifa Jijini Dar es Salaam, licha ya kwamba mashabiki wa pande zote ni marafiki, wakati wa pambano kila mmoja hukaa upande wake.

Wakifika uwanjani wapenzi wa Simba hukaa kwenye jukwaa lao na wapinzani wao au Yanga hujipanga pia kwenye jukwaa lao na watashangilia timu yao kikamilifu kulingana na mafanikio.

Hakuna uadui mechi ikimalizika kwa kufungana, sare au kufungwa inakubalika, si suala la kuanzisha uhasama bali marafiki wanaoshabikia timu tofauti huendelea na maisha na kuheshimiana kama ilivyokuwa hapo awali.

> “Kutoka nje zaidi, mathalani, uhusiano wa kisiasa katika Afrika unajengwa katika taswira hasi ambayo imeonekana kutukosanisha, kutufitinisha na kutuvuruga wananchi bila sababu za msingi.

Ndivyo unavyotakiwa kuwa uhusiano wakisiasa maana hizo ndizo timu au vyama tunavyovishangilia lakini haimaanishi kuwa sisi ni maadui hata kama tunaunga mkono chama tawala au upinzani.

Nimeutoa mfano huo wa mchezo wa mpira kwasababu inawezekana tayari watu wamejifunza kutokana na siasa za chuki tulizo nazo katika mechi zetu, kwamba adui yako mwombee njaa. Kuombeana njaa huko ni kutokana na chuki miongoni mwetu na chuki siku zote huwa na chanzo.

Hakuna sababu ya kuwa na chuki za kisiasa kwani ni matokeo ya mwisho ya uvumilivu yaani kwa kuwa umemshindwa basi unajaribu anagalau kuonyesha hasira zako kwenye chuki, ukikataa kushiriki katika shughuli mbalimbali za kisiasa, kijamii na hata kiuchumi.

### NDANI YA VYAMA

Leo tumeanza kuona chuki katika vyama vyetu vya siasa wako watu hawazungumzi kabisa wamekosana kutokana na ushabiki wa vyama vya siasa, wengine ndoa zimevunjika kwasababu ya ushabiki wa vyama vya siasa.

Kutoka nje zaidi, mathalani, uhusiano wa kisiasa katika Afrika unajengwa katika taswira hasi ambayo imeonekana kutukosanisha, kutufitinisha na kutuvuruga wananchi bila sababu za msingi.

Kwa mfano Sudan Kusini, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Nigeria na DRC je, kuna sababu za msingi za kutofanya wananchi wa nchi hizo wasielewane na kuishi kwa amani kama ndugu na jamaa?

Wapo watu wanaosema kuwa vurugu hizo za kisiasa hazipo Afrika tu bali hata katika mataifa mengine duniani.Ni kweli baadhi ya nchi za Ulaya zina vurugu za kisiasa lakini hoja haina msingi kwa sababu huwezi kuhalalisha mabaya na maovu kwa sababu wengine hufanya hivyo.

Ifike mahali Waafrika waone aibu na wa kuondoa aibu hiyo si wengine bali ni sisi wananchi pamoja viongozi wetu ambao tayari tupo na siasa hizo zinafanywa na walioko madarakani. Wafahamu kuwa chuki hazijengi, uvumilivu na upendo baina ya mashabiki au wanachama ndilo jambo la msingi.

### MANDELA NI KIOO

Aliyewahi kuwa Rais wa kwanza mweusi Afrika ya Kusini Nelson Mandela, pamoja na kwamba alifungwa gerezani kwa miaka 27 kwa sababu ya kupigania haki za watu weusi dhidi ya ubaguzi wa rangi na ukandamizaji wa haki za binadamu hakuwa na chuki.

Alipotoka gerezani hakupigana na watesi wake wala kuwaadhibu. Baada ya kupata dhamana hiyo ya kuwa rais wa nchi ategemeo ya wengi hasa weusi wenyewe yalikuwa kulipa visasi kwa wale waliomfunga na kuwanyanyasa weusi.

Mandela hakufanya hivyo. Alitaka maridhiano, uvumilivu wa kisiasa na mshikamano wa kitaifa licha ya kufungwa miaka mingi gerezani , kuteseka na kunyanyaswa na makaburu.

Mandela hana tofauti na viongozi wengi wa Kiafrika ni kaka yao wanatakiwa tu kumwiga , waache kupigania maslahi yao binafsi badala yake wahudumu katika serikali kwa muda usiozidi miaka ule uliopangwa na katiba na kuachia madaraka kwa heshima, amani na utulivu. Kama viongozi wa Sudani Omar al Bashir na Robert Mugabe wa Zimbabwe, wasingeumia na kukutana na sokomoko la nguvu ya umma inayotaka kuwaondoa madarakani.

Afrika iendelee kujifunza kwa Mandela mwenye busara na hekima ya hali ya juu na wakati wa uongozi na utawale wake hakutaka kulipa visasi kwa wale waliomtesa.

Badala yake baadhi yao alifanya nao kazi akiwa Rais nao wakiwa watendaji wake wa chini na kama angelikuwa ni mtu wa chuki, basi yangelifunguliwa magereza mengi ya makaburu pekee na kuwafunga humo na kama angelifanya hivyo , yeye pia angelikuwa kaburu tofauti yake na wao ingelikuwa ni rangi kwamba Mandela kaburu mweusi na wao makaburu weupe.

Viongozi wa Afrika ni lazima kukubaliana na kuamini kuwa utawala wa sheria na kuheshimu demokrasia havifanyika kwa hiari ni kwa mujibu wa katiba pekee. Hata hivyo si zama za kuamini kuwa wamezaliwa ili wawaongoze wengine na kwamba wao na watoto wao ndiyo watawala, kama inavyoendelea kwa baadhi ya mataifa ya Afrika Mashariki.

### UTANI WA JADI

Wakati wa kuifanya siasa kama utani wa jadi umefika. Kwa maana kama wewe ni mshabiki wa timu ya Mtibwa Sugar ukumbuke utakapoiombea Simba ama Yanga isambaratike, Mtibwa itacheza na nani? Kama unaona faida na umuhimu wa kuwepo kwa Mtibwa Sugar vivyo hivyo itakuwa ni faida kuwepo kwa vilabu vingine kama, Simba na Yanga.

Maana huwezi kujitungia mtihani wewe mwenyewe na ukajisahihisha peke yako.

Katika moja ya machapisho yake Mwalimu Julius Nyerere aliwahi kusema haya...“Pamoja na kwamba vyama ni vibovu, lakini vipo, kama vipo, basi muanze kujifunza maadili ya kuwa na vyama vingi na kama mna vyama vingi hampuuzi maoni ya wananchi” (Nyerere, J.K 1995 Nyufa)

Mwalimu alikuwa akisisitiza umuhimu wa kuvumiliana kisiasa huo haukuwa ujumbe kwa Tanzania pekee bali ni kwa bara zima la Afrika ambako bado kumekuwa na shida hasa kwenye kuzingatia demokrasia ambayo msingi wake mkuu ni wananchi wenyewe kuwa msingi wa kila jambo.

Demokrasia ikitendeka hakuna mtu atakaye kuwa na mawazo ya kishetani ya kusaliti ama kuiuza nchi kwa vipande vya fedha, mikataba mibovu ya madini na uwekezaji, ufisadi, uhujumu uchumi na ukandamizaji wa demokrasia wa aina yoyote.

Hivyo ni muhimu kuchunga demokrasia, uvumilivu wa kisiasa na kuendeleza utawala wa sheria katika nchi za Kiafrika ili kufikia azma ya kuwa na washirika wengi au vyama vingi vya kisiasa.

# Corona kirusi kilicholeta amani Mashariki ya Kati



Rais wa Iran Hassan Rouhani, nchi yake imetikiswa na corona, hali iliyosababisha hofu na kutulia kwa mapigano Mashariki ya Kati. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Ani Kija**

UNAWEZA kushangaa lakini ni kweli janga la ugonjwa wa virusi vya corona limepelekea mabadiliko ya mwelekeo wa eneo la Mashariki ya Kati, ambalo limekumbwa na vita vinavyobadilishana maeneo ya mapigano kila kukicha, mradi tu isiwepo amani.

Sasa kuna utulivu , ulioingia kutokana na mahangaiko ya makundi tofauti ya jamii kukabiliana na hatari ya kuenea kwa homa ya corona.

Kusambaa kwa virusi hivyo Iran katika eneo la Mashariki ya Kati, na taarifa za mwanzo wa wiki zilionyesha kuwa hali ya homa ya corona nchini Iran ni mbaya kuliko inavyoelekea kukiri serikali ya nchi hiyo. Mashirika ya nje yalikuwa yakipeleleza undani wake hata kwa satellite.

Utawala wa Hamas jimbo la Gaza ulikuwa unasisitiza hadi mwishoni mwa wiki kuwa hakuna tukio la ugonjwa huo eneo hilo, huku maofisa wake wakisema wataendelea kuhakikisha utulivu unaendelea katika mpaka na Israel.

Walisema huu siyo wakati wa kuendeleza mapambano dhidi ya Israel. Mapema wiki iliyotangulia Israeli ilitoa vifaa 200 vya kupima homa ya corona, ofisa wa kijeshi wa Israel aliyetoa vifaa hivyo akisema Israel imepania kuzuia homa hiyo kuenea Gaza pamoja na 'Judea na Samaria,' yaani Ukingo wa Mashariki, kwa Wapalestina.

Rais Mahmoud Abbas, ambaye ni Mwenyekiti wa Mamlaka ya Palestina, alikuwa katika taabu ya kutafuta njia za kuzuia kuenea kwa homa ya corona, ambayo imelipukia mjini Bethlehem, alikozaliwa Masihi Yesu Kristo, eneo muhimu la utalii.

> Ukanda wa Magharibi wa Mto Jordan, kanisa la eneo alikozaliwa Masihi limefungwa baada ya mahujaji (au wageni) wawili kutoka Ugiriki kugundulika wameathirika na corona.

Kujua kuwa hali si rahisi kwa Hamas, hapakuwa na ukaguzi wa wakazi wa Misri wakiingia eneo la Gaza kwa shughuli za biashara, lakini shinikizo la wakazi wa Gaza likalazimisha kupimwa kwa wanaoingia eneo hilo.

Hadi kufikia katikati ya mwezi utawala wa Hamas ulikuwa umepima watu 14 waliohofiwa kuwa na virusi hivyo lakini wakaonekana wako salama, ila siku mbili baadaye tukio la corona likatangazwa rasmi kama ilivyokuwa kwa upande wa Tanzania, tukio la kwanza liliripotiwa.

Hata hivyo, utawala wa Hamas ulitoa tangazo kwa wananchi 2,667 ambao waliingia Misri na kurudi Gaza kujitenga kwa muda majumbani mwao huku wakifuatiliwa.

Mikutano ya zaidi ya watu 100 pia ilipigwa marufuku, lakini hapakuwa na ushirikiano wa wazi kuhusu vita ya corona, Gaza na Palestina.

Hamas ilikuwa inajitahidi kupata thawabu za kisiasa kutokana na mwelekeo wake wakati wa gonjwa la corona,ambalo limesambaa kwa kiwango kikubwa nchini Israel, kukiwa na zaidi ya wagonjwa 200. Walisema mradi adui Israel anahangaika na corona asishambuliwe kwa mabomu ya miavuli mradi Israel nayo isifanye shambulio lolote dhidi ya Hamas eneo la Gaza. Licha ya kuwa Hamas ilikuwa inaongea kwa kujiamini kwani ugonjwa ulikuwa bado kusambaa eneo hilo, dunia ilikuwa inajiuliza kutatokea nini endapo corona itasambaa, kwa ufinyu wa uwezo wa tiba na ujazo wa watu karibu milioni mbili katika eneo dogo tu. Israel haikuwa unahofiwa na mashirika ya Umoja wa Mataifa au Ulaya licha ya waathirika kuzidi.

Ukanda wa Magharibi wa Mto Jordan, kanisa la eneo alikozaliwa Masihi limefungwa baada ya mahujaji (au wageni) wawili kutoka Ugiriki kugundulika wameathirika na corona.

Utawala wa Palestina Machi 5, ulitangaza hali ya hatari ya gonjwa hilo na kufunga shule, vyuo na vyuo vikuu, misikiti na makanisa. Eneo la Bethlehem ndiyo lilikuwa na wagonjwa zaidi, tisa kati ya 22 katika hatua za awali wawili ya kwanza ya mwezi Machi.Hadi waathirika wa corona walipofikia 38, wote bado walikuwa Bethlehem ila mmoja akagundulika Tulkarm.

Marekani ilitingishwa na hali ya corona katika Mashariki ya Kati ilipotangazwa kuwa watu 38 waliokuwa wamewekwa eneo la kuzuiwa kutokana na virusi hivyo wakatoroka walikuwa wametokea Iran.

Ndiyo nchi yenye maambukizi makubwa zaidi Mashariki ya Kati, na kutoroka kwa watu hao kumesambaa maeneo tofauti nchini humo kama wasingepatikana haraka ilikuwa ni hali ya kutisha. Rais Donald Trump, alilazimika kutangaza hali ya hatari nchini kote kutokana na waliotoroka.

Wachunguzi walisema hali ya corona ni mbaya zaidi nchini Iran kuliko ambavyo serikali ilikuwa inakiri. Taarifa ambazo Iran ilihakikisha zilisema ugunduzi wa corona ulishafikia waathirika 6,000 na watu 145 wakiwa tayari wamefariki, lakini baadhi ya mashirika ya upelelezi yalikuwa uanatilia shaka taarifa hizo.

Baadhi ya wachambuzi wa habari Ulaya na Marekani walikuwa wakielezeza hali ilivyo ngumu kwa utawala wa Iran kushughulikia janga la corona katika mazingira ya vikwazo vya uchumi vilivyowekwa na Marekani.

Taarifa ya gazeti la The Guardian nchini Uingereza ikasema kuwa utawala wa Iran ulikuwa umechimba makaburi ya kuzika watu wengi eneo la Qom, lililosheheni makuhani wa madhehebu tawala la Iran.

Taasisi ya upelelezi ya Worldometer ilisema mwanzo wa wiki kuwa kuna matukio 124, 9912 ambayo tayari yamegundulika Iran na vifo vilishafikia 853, na kabla ya hapo ilielezwa kuwa shughuli za kijeshi la vikosi maalum vya Iran nje ya nchi hiyo zimesimamishwa. Iraq ilikuwa inajitahidi sana isipate virusi kutoka Iran, ilikozidi.

Nchini Afghanistan, ambako wapiganaji wa Taliban ni marafiki wa Iran walisema ugonjwa wa homa ya corona bado haujathiri shughuli zao za kivita, wakati nchi hiyo ikifikia matukio 16 ya corona. Cha kushangaza ni kuwa matukio ya kutumia silaha kushambulia yalifikia 16 kwa siku moja, Jumapili wakati Ijumaa kulikuwa na matukio 95 ya mashambulizi, ikiwa inajumlisha urushaji wa maroketi au kulipuka kwa mabomu ya kuteawa katika majimbo tofauti nchini.

Taarifa zilisema kuwa kuenea kwa virusi vya corona kumepunguza kwa kiasi viwango vya mashambulio kote nchini, hali ambayo wananchi hao hawakuizoea.

Baada ya kufikiwa makubaliano kati ya Marekani na kundi la Taliban kuwa ipunguze mashambulio au isifanye tena mashambulio kwa miezi mitatu huku Marekani ikiondoa askari wake kwa sehemu kubwa, hitilafu ilitokea.

Upande wa serikali ya Afghanistan ambao haukushirikishwa katika majadiliano hayo ukatoa msimamo kuwa haitawaachia wapiganaji 5,000 wa Taliban inaowashikilia, dhana ikiwa ni kushinikiza kundi hilo lijadiliane na serikali hiyo, wakati Taliban siku zote haitambui serikali iliyopo Kabul na inaongea tu na Marekani. Baada ya hilo tamko, uongozi wa Taliban ukaanza tena mashambulio ila sio dhidi ya Marekani.

Taarifa nyingine zilisema kuwa kundi la Dola ya Kiislamu (Daesh) lilitoa agizo kwa wapiganaji wake kuchukua tahadhari za kiafya kuhusiana na virusi vya corona na kuangalia nyendo zao kwa makini. Mwenyekiti wa Kamati ya Usalama ya Bunge la Afghanistan alisema maelekezo hayo yanatoa ishara kuwa kutakuwa na utulivu kutokana na kusembaa kwa janga la corona.

Ni kama vile wababe wa vita wanavuta pumzi corona iishe waendelee na shughuli zao kama kawaida, kwani kuna hisia kuwa sasa wanacheleweshwa. Ni jambo la kushangaza, bila corona amani hakuna!



HABARI MBEYA

# Mbaroni tuhuma za wizi magodoro

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

JESHI la Polisi mkoani Mbeya linawashikiliwa watu wawili, akiwamo Ofisa Mauzo wa Kampuni ya ya Chang Qing inayojihusisha na utengenezaji, usambazaji na uuzaji wa magodoro, Fredy Ngodoki (34), kwa tuhuma za kuvunja ghala la kampuni hiyo na kuiba magodoro 161.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alimtaja mtuhumiwa mwingine kuwa ni mfanyabiashara wa magodoro, Thadei Matamba (30), ambaye ni mkazi wa Veta jijini Mbeya.

Alisema watuhumiwa walikamatwa kufuatia msako mkali uliofanywa na jeshi hilo kati ya Machi 21 na 22, mwaka huu, katika maeneo ya Jiji la Mbeya, Mji wa Mbalizi na Kijiji cha Ikonya wilayani Mbozi katika Mkoa wa Songwe.

"Baada ya kumkamata Ofisa Mauzo Ngondoki, alikiri kuiba magodoro yenye ukubwa tofauti 161 yenye thamani ya shilingi milioni 12.5 na kuyauza kwa Matamba," alisema Kamanda Matei.

Alisema  baada ya kumkamata Matamba alikiri kuuziwa magodoro hayo 143 kwa thamani ya Sh. milioni 10 na kupewa risiti, lakini alikuwa bado hajalipa pesa.

Alisema kwenye msako huo magodoro 89 yalipatikana nyumbani kwa mtuhumiwa Matamba na Ofisa Mauzo wa Kampuni hiyo ya kichina alikiri kuwa aliuza magodoro mengine 10 katika eneo la Uyole.

Kamanda Matei alisema upelelezi wa shauri hilo unaendelea na kwamba baada ya kukamilika, watuhumiwa hao watafikishwa mahakamani.

Aliwataka wananchi wa Mkoa huo kufanya biashara kwa kufuata taratibu zilizopo ili kuepuka kukumbwa na mkono wa sheria, huku akiwataka wananchi wenye taarifa za wahalifu kutoa taarifa hizo kwa Jeshi la Polisi.

# Wodi wazazi hospitali rufani yazidiwa

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

HOSPITALI ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya, inakabiliwa na msongamano wa wagonjwa kwenye wodi ya mama na mtoto kutokana na wodi hiyo kuwa ndogo kuliko mahitaji.

Hali ya msongamani inasababisha wagonjwa kulala wawili kwenye kitanda kimoja.

Hayo yalisemwa na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Salum Manyatta, wakati Benki ya Posta (TPB) ilipokuwa inakabidhi msaada wa mifuko 300 ya saruji kwa ajili ya ujenzi wa jengo la mama na mtoto katika hospitali hiyo.

Alisema kutokana na hali hiyo, serikali ya kwa kushirikiana na wadau, waliamua kuanza ujenzi wa jengo jipya ambalo litakuwa la ghorofa tatu, na kwamba litasaidia kumaliza tatizo hilo.

Alisema harakati za kuanza ujenzi huo zilianza Machi 8, mwaka huu wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani ambapo waliandaa harambee kwa ajili ya kukusanya fedha za kuanza ujenzi huo mapema.

"Kwenye jengo lililopo tumefanya kila jitihada kuongeza vitanda ili kinamama wasilale chini na wala wasilale wawili kwenye kitanda kimoja, lakini imeshindikana kutokana na eneo kuwa dogo, kwa sasa wanalala kinamama wawili kwenye kitanda kwa hiyo ukijumlisha na watoto wao unakuta kitanda kimoja wanalala wanne," alisema Dk. Manyata.

Alisema kwenye harambee waliyoifanya walipata zaidi ya Sh. milioni 170 na ahadi mbalimbali ikiwamo mifuko hiyo 300 ambayo Benki ya Posta iliahidi.

Akikabidhi msaada huo, Mkurugenzi wa Teknolojia na Operesheni wa TPB, Jema Msuya, alisema waliamua kuchangia mifuko hiyo baada ya kubaini kuwa hospitali hiyo inakabiliwa na tatizo la wagonjwa kulala kwa kusongamana.

Alisema msaada waliokabidhi una thamani ya Sh. milioni 4.8 na kwamba waliguswa baada ya kupelekewa maombi na serikali ya mkoa ikiomba wachangie.

"Tunatambua kuwa kitengo cha mama na mtoto ni muhimu sana na watoto ndio taifa letu la kesho, hivyo tuliona ni muhimu sana kuchangia ili kuhakikisha jengo hilo linajengwa haraka," alisema Msuya.

Aliwaomba wadau wengine waendelee kuchangia ujenzi huo ili kuhakikisha jengo hilo linakamilika na wananchi wanaendelee kupata huduma bila msongamano.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Glory Mbwile, alisema pamoja na kwamba jengo lililopo ni dogo, lakini limechakaa na linavuja wakati mvua inaponyesha.

Alisema kwa mujibu wa wahandisi waliokadiria jengo jipya linalotarajiwa kujengwa ni kwamba litagharimu Sh. bilioni tatu na kwamba mifuko 300 ya saruji waliyopewa na TPB itatukika kufyatua tofali.

Akipokea msaada huo kwa niaba ya Serikali ya Mkoa, Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Mariam Mtunguja, aliishukuru Benki ya TPB kwa msaada huo huku akiomba kuendelea kuchangia.

Alisema mahitaji bado ni makubwa kutokana na makadirio ya gharama yaliyotolewa na wataalamu hivyo akasisitiza wadau kuendelea kuguswa na kuchangia ili kuwaondolea kinamama adha ya kulala wawili kwenye kitanda kimoja.

Alisema waliamua kuanza kuchangishana badala ya kusubiri fedha kutoka Serikali Kuu ili kuepuka mradi huo kuchelewa kuanza kujengwa.



Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Mariam Mtunguja (kulia), akipokea msaada wa mifuko 300 ya saruji kutoka kwa Mkurugenzi wa Teknolojia na Operesheni wa Benki ya Posta (TPB),  Jema Msuya (kushoto), jijini Mbeya jana, kwa ajili ya ujenzi wa wodi ya mama na mtoto kwenye Hospitali ya Rufani ya Mkoa huo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mvua yasababisha mgawo wa maji

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

WAKAZI wa Jiji la Mbeya, wameanza kupata maji kwa mgawo kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha kuharibu miundombinu na kukosekana kwa umeme kwenye mitambo ya kusafisha, kutibu na kusukuma maji.

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, Mkoa wa Mbeya imesema kuna upungufu mkubwa wa uzalishaji wa maji kwa ajili ya matumizi ya wananchi, kutokana na athari za mvua zinazoendelea kunyesha ikiwamo uharibifu wa miundombinu.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Ndele Mengo, alipokuwa akizungumza na wanahabari na kueleza kuwa  kutokana na uharibifu wa miundombinu ya maji uliosababishwa na mvua zaidi ya Sh. milioni 50 zimetumika kukarabati.

"Katika kipindi hiki cha mwezi wa tatu kuanzia 16 kumekuwa na uhaba wa maji kwa baadhi ya maeneo ya Jiji na Mji Mdogo wa Mbalizi kukosekana huku kwa maji kumesababishwa na mvua kubwa zilizonyesha zimechangia vyanzo vya maji kujaa michanga na matope, mabomba kusombwa na mafuriko ya maji na kukosekana kwa umeme kwenye mitambo ya kusafisha, kutibu na kusukuma maji," alisema Mhandisi Ndele.

Alisema katika kukabiliana na uharibifu wa miundombinu ya maji, mamlaka hiyo inaendelea kuchukua hatua mbalimbali kama kufanya usafi kwenye vyanzo mara mvua inapokuwa imeleta athari, kufanya matengenezo ya haraka mabomba yanaposombwa na mafuriko.

Hata hivyo aliyataja maeneo yaliyoathirika na upungufu wa maji kuwa ni Simike, Nzovwe, Iyunga, Kalobe, Isyesye, Iyela, Ikuti, Itezi, Gombe, Utukuyuna Igawilo.

Baadhi ya wakazi mkoani Mbeya, wamesema siku za hivi karibuni wamepata shida ya upatikanaji wa majisafi na salama, hali ambayo inaweza kuhatarisha afya na kuathiri shughuli za kiuchumi.

Mamalishe katika eneo la Sokoine, Devotha Ndele, alisema kukosekana kwa maji ya uhakika kunakwamisha shughuli zake za biashara ya chakula, hali inayosababisha kuchelewa kutoa huduma na kukosa fedha.





# Watoto wenye mahitaji maalumu waandikishwa shule za misingi

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SERIKALI imesema hadi sasa watoto 54,000 wenye mahitaji maalumu wameandikishwa kwenye shule za msingi nchini ikiwa ni mara mbili ya idadi iliyokuwapo mwaka 2015.

Pia, imejenga shule ya sekondari kwa ajili ya watoto hao ambayo haijawahi kuwapo tangu nchi ipate uhuru.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) anayeshughulikia sekta ya elimu, Gerald Mweli alipokuwa akizungumzia uboreshaji wa miundombinu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu, jijini hapa.

Alisema ongezeko hilo la uandikishaji ni kutokana na Mpango wa elimu bila malipo na mwamko wa wazazi kuacha kuwaficha watoto wenye ulemavu.

"Uandikishaji wa watoto wenye mahitaji maalumu umeongezeka mara mbili ikilinganishwa na watoto waliokuwapo mwaka 2015, hii imetokana na kipaumbele cha serikali cha kuhakikisha watoto wote wanapata elimu," alisema.

Mweli alisema kutokana na ongezeko hilo, serikali ilianza kutoa mafunzo kwa walimu 60,000 wa elimu ya awali hadi darasa la nne ili wahudumie watoto hao watakaokuwapo kwenye shule husika.

"Sisi tunataka shule zetu hizi za kawaida pamoja na kwamba sio za watu wenye mahitaji maalumu, lakini shule zingine zimeimarisha miundombinu yake ili kutoa huduma kwa watoto na tumenunua vifaa vya kutosha," alisema.

Kuhusu shule ya sekondari, Mweli alisema shule hiyo itakuwa jumuishi.

"Shule ipo Patandi, imejengwa kwenye chuo ambacho serikali imekianzisha kwa ajili ya kufundisha walimu watakaofundisha watoto wenye mahitaji maalumu, tayari tumepeleka walimu saba na miundombinu yake ipo hatua ya mwisho na shule inajengwa kupitia mpango wa lipa kulingana na matokeo," alisema.

Naibu Katibu huyo alisema lengo la kujenga shule hiyo ni watoto hao watakapofaulu waendelee elimu ya sekondari.

"Awali walishindwa wengine kuendelea na shule kutokana na kutokuwa na miundombinu rafiki, tumeweka sera ya elimu jumuishi ili watoto wasio na changamoto wawasaidie wenye uhitaji," alisema.

Mweli alisema baadhi ya shule zimeimarishwa ikiwamo ya Buhangija na Mtindu zilizopo Shinyanga.

Alitoa wito kwa jamii kuwatoa watoto na kuacha kuwaficha ili wapate fursa ya elimu.

"Serikali imejipanga kupokea watoto hawa, tusiwafiche na tuwalinde ili wapate elimu," alisema.




Magari ya majitaka, yakimwaga kwenye bwawa maalum yaliyopo katika eneo la Swaswam, jijini Dodoma jana. Uwepo wa mvua nyingi zinazoendelea kunyesha nchini, umetoa fursa ya kibiashara kwa kazi hiyo, kutokana na vyoo vingi na mashimo ya majitaka kujaa haraka. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Duwasa kujenga bomba la majitaka

**Na Ibrahim Joseph, DODOMA**

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (Duwasa) imetenga Sh. milioni 250 katika mwaka wa fedha ujao 2020/21, ili kujenga bomba kubwa la pili la majitaka katika eneo la Swaswa.

Hayo yalielezwa jana jijini hapa na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa Mamlaka hiyo, Sebastian Warioba alipozungumza na waandishi wa habari ofisini kwake.

Warioba alisema Duwasa wametenga kiasi hicho ili kuongeza ujenzi wa bomba kubwa la pili katika eneo hilo na kuondoa kero ya mifereji ya majitaka inayopita kwenye mtaa huo kuzidiwa uwezo.

"Kama mnavyojua mifereji ya eneo hilo nyuma yake inapokea maji mengi kutoka kwenye makazi yote ya jijini hapa, kabla ya kufika kwenye mabwawa yetu ya maji taka yaliyopo Mtaa wa Swaswa, mvua za msimu huu zimewasaidia kubaini kero hiyo, hivyo inahitaji kuboreshwa," alisema.

Alisema kutokana na mvua nyingi zilizonyesha msimu mwaka huu zimesababisha mfereji wa kuingiza maji hayo kuzidiwa na mifuniko yake kusukumwa nje.

Alibainisha kuwa boma lililopo linazidiwa na maji kutokana na kuwa na kipenyo kidogo cha kupitisha maji yote ya mvua na taka, hivyo kujengwa kwa bomba hilo la pili kutaondoa kero hiyo.

Aliongeza kuwa mbele ya mabwawa hayo ya majitaka watachimba mengine kwa kushirikiana na Jiji la Dodoma ili kuelekeza maji yote yaingie kwenye eneo hilo bila kufika makazi ya watu.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Mtaa wa Swaswa, Charle Nyuma, aliwaomba Duwasa kuharakisha ujenzi wa bomba hilo ili kuwaondolea adha ya mafuriko ya majitaka wakati wa mvua.

## Dodoma kuwafikisha kortini wadaiwa 39 kodi pango

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma inatarajiwa kuwapeleka mahakamani wadaiwa sugu wa kodi ya pango la ardhi 39 wanaodaiwa kiasi cha Sh. milioni 278.

Hayo yalielezwa jana na Ofisa Ardhi, Damas Mwakindingo, alipokuwa akizungumza na Nipashe kuhusu utekelezaji wa agizo la Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi la kuwaburuza mahakamani wadai kuanzia Machi 23, mwaka huu.

Alisema bado wanaendelea kuwakusanya wengine na ni wale wanaodaiwa miaka mingi huku madeni yao yakianzia Sh. 200,000 na kuendelea.

"Madai yanatofautiana kutokana na aina ya matumizi ya kiwanja wapo ambao wana viwanda, wengine makazi, hivyo kodi haziwezi kulingana," alisema.


Juzi, wizara hiyo ilitangaza kuanza kuwafikisha mahakamani wadaiwa wote sugu kuanzia Machi 23, katika maeneo mbalimbali nchini ikiwa ni jitihada za wizara hiyo kuhakikisha wamiliki wote wa ardhi wanalipa kodi kwa mujibu wa sheria.

Uamuzi wa kuwafikisha mahakamani wadaiwa hao unafuatia kushindwa kulipa madeni yao hata baada ya kupelekewa ilani ya madai inayowataka kulipa madeni ya kodi ya pango la ardhi ndani ya wiki mbili baada ya kupokea hati ya madai.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Kitengo cha Kodi wizarani hapo, Denis Masami, malengo ya wizara kwa mwaka wa fedha 2019/20 ni kukusanya Sh. bilioni 180 kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato ya ardhi ikiwamo kodi ya pango la ardhi, ada za upimaji ardhi, usajili wa hati na nyaraka pamoja na ada zinazotozwa kupitia Mabaraza ya Ardhi ya Nyumba ya Wilaya.

Alisema takriban wiki mbili sasa maofisa kutoka wizarani kwa kushirikiana na watumishi wa mikoani wamesambazwa maeneo mbalimbali nchini katika operesheni maalumu ya kusambaza ilani za madai kwa wadaiwa sugu.

"Machi 23, 2020 jumla ya mashauri 847 yatapelekwa katika Mabaraza ya Ardhi ya Nyumba ya wilaya katika mikoa ya Dar es Salaama, Mwanza na Lindi, katika mkoa wa Mwanza mashauri 450, Lindi 121 na Dar es Salaam Ilala 200 na Temeke 76 na lengo hapa ni kuhakikisha tunakusanya kodi yetu ya pango la ardhi kama sheria ya umiliki ardhi inavyoelekeza," alisema Masami.



# Zanzibar watakiwa kubakia majumbani

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAZIRI wa Afya Zanzibar, Hamad Rashid Muhamed, amesema kuwa silaha kubwa ya kujikinga na ugonjwa ya corona kwa wananchi ni kubaki majumbani mwao na kuacha tabia ya kutembea ovyo, hasa katika mikusanyiko ya watu.

Alieleza hayo alipokuwa akitoa taarifa kwa waandishi wa habari kuhusu hatua mbali mbali zinazochukuliwa na serikali kukabiliana na maradhi hayo.

Aliwataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari zaidi ya kinga katika kukabiliana na maradhi ya corona, ikiwamo kupunguza mikusanyiko na safari zisizokuwa za lazima.

"Ni bora kubaki ndani nyumbani kwako kama huna ulazima wa kutoka nje au kwenda sokoni baki ndani ili usije ukaambukizwa corona," alisema Hamad.

Aidha, waziri huyo aliwataka wananchi kuwa na utamaduni wa kuosha mikono yao kila baada ya saa moja ili kujikinga kutopata maambukizi ya ugonjwa huo.

Waziri Hamad alisema kuwa serikali imejipanga na kuhakikisha kuwa wageni wote watakaoingia Zanzibar watawekwa karantini kwa kipindi cha siku 14 na kujilipia gharama wenyewe.

Aliwataka Wazanzibari waliopo nje ya nchi hasa katika nchi ambazo zimekumbwa na ugonjwa wa corona waendelee kubaki huko waliko ili wasije kuambukiza wengine.

Hata hivyo, Waziri wa Afya alisema kuwa hadi sasa mgonjwa wa corona aliyegundulika Zanzibar bado ni mmoja, na anaendelea na matibabu kwenye kituo maalum kilichotengwa huko Kidimni Wilaya ya Kati Unguja.

Aliwataka wananchi kukubali utaratibu uliowekwa na serikali wa kupunguza msongamano katika Hospitali ya Mnazimmoja kwa kutoa nafasi watu wawili tu kuangali mgonjwa mmoja.

"Nimepita Hospitali ya Mnazimmoja nimekuta mkusanyiko mkubwa wa watu wanaoenda kuangalia wagonjwa wao waliolazwa hospitalini hapo kwa maradhi mbalimbali... niwaombe tu wananchi katika kipindi hiki kuacha tabia hiyo na badala yake mgonjwa mmoja kuangaliwa na watu wawili tu ili kujikinga na corona," alisema.



Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (Tamwa), Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, akizungumza na waandishi wa habari (hawako pichani) mjini Zanzibar jana, kuhusu wananchi kuchukua tahadhari ya maambukizi ya virusi vya corona. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Tamwa yatoa tahadhari kisa watoto kuzurura ovyo mitaani

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

LICHA ya serikali kuzifunga shule zote na madrasa ili watoto wabaki nyumbani kwao na kujikinga na virusi vya corona, kundi kubwa la watoto wanaonekana wakizurura mitaani hali ambayo ni hatari kwa afya zao.

Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania, (Tamwa) kimewataka wazazi walezi, na jamii kwa ujumla kuhakikisha watoto wanabakia ndani katika kipindi hiki ambacho hawendi shule wala madrasa.

Akizungumza na waandishi wa habari Mkurugenzi wa Tamwa Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, alisema katika maeneo mbalimbali bado watoto wanaonekana wakicheza nje kwa vikundi jambo ambalo linaweza kupelekea maambukizi ya maradhi hayo hatari.

Alisema ni muhimu wazee kuhakikisha kuwa watoto wanabaki ndani wanajisomea na kufanya shughuli nyingine chini ya uangalizi makini wa wazazi.

"Tunawaomba wazee pia kuwaelimisha watoto sababu ya kuzuiwa kutokwenda shule na madrasa kwamba wabakie ndani na siyo kuzurura mitaani," alisema Dk. Mzuri.

Alieleza kuwa hali hiyo itaweza kuwalinda dhidi ya maradhi hayo mabaya ya kuambukiza kwa aina tofauti ikiwamo kushika sehemu ambayo mwenye maambukizi ameshika.

Dk. Mzuri alieleza kuwa kubakia ndani chini ya uangalizi maalum pia kutawalinda dhidi ya watu wabaya ambao wakati mwingi hutumia nafasi wanayoipata na kuwafanyia vitendo viovu watoto, ikiwamo kuwabaka.

"Tamwa, inapenda kuwapa pole wanajamii, serikali na dunia kwa jumla kwa kupitia katika kipindi hichi kigumu cha maradhi ya COVID-19 ambayo yanaendelea kuyatesa mataifa mengi ulimwenguni," alisema.

# Misitu wakamata msumeno wa moto wa kukatia minazi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

IDARA ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka Zanzibar, imefanikiwa kukamata msumeno wa moto uliokuwa ukitumika kwa kukata minazi katika eneo la Machui Wilaya ya Kati Unguja.

Mkurugenzi wa idara hiyo, Sudi Moh'd Juma, alisema baada ya kupata taarifa kutoka kwa wasamaria wema kikosi cha kazi cha doria cha idara hiyo kilifika katika eneo hilo na kukuta zaidi ya vijana wanane wakiendelea na shughuli ya ukataji wa minazi.

Alisema kuwa zaidi ya minazi 40 imekatwa katika eneo hilo na kusababisha uharibifu mkubwa wa mazingira.

Mkurugenzi huyo aliwataka wananchi kufuata sheria, na kwamba serikali imeshapiga marufuku utumiaji wa msumeno wa moto na watahakikisha wanawafuatilia na kuwakamata watu wote watakaobainika kuwa wanatumia misumeno hiyo kwa siri.

Aidha, alisema lengo la serikali la kutoa heka tatu kwa wananchi ni kwa ajili ya uzalishaji na sio kufanya uharibifu, hivyo ameiomba Wizara ya Ardhi kuwachukulia hatua watakaoshindwa kuziendeleza heka hizo na kuwapa watu wengi waziendeleze kwa shughuli za kilimo.

Naye Msimamizi wa Sheria Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka, Haji Hassan, alisema licha ya kutowakamata vijana hao, lakini wamefanikiwa kuwatambua na watahakikisha wanawachukulia hatua za kisheria, ikiwamo kupelekwa mahakamani kwa kulipa faini, kifungo au vyote kwa pamoja.

**Mkurugenzi huyo aliwataka wananchi kufuata sheria, na kwamba serikali imeshapiga marufuku utumiaji wa msumeno wa moto na watahakikisha wanawafuatilia na kuwakamata watu wote watakaobainika kuwa wanatumia misumeno hiyo kwa siri.**

# DC akerwa usimamizi Bwawa la New Sola

**Na Happy Severine, SIMIYU**

MKUU wa Wilaya ya Maswa mkoani Simiyu, Dk. Seif Shekalaghe, ameeleza kukerwa na usimamizi dhaifu wa Bwawa la New Sola lililoko katika Kijiji cha Zanzui, humo ambacho ndicho chanzo kikuu cha maji katika mji wa Maswa.

Alisema baadhi ya vijiji vilivyopo karibu na bwawa hilo hufanya shughuli za uvuvi haramu wa kutumia sumu na kuhatarisha maisha ya binadamu na viumbe hai wanaotumia maji ya bwawa hilo.

Hali hiyo imezua hofu kubwa kwa watumiaji wa maji ya bwawa hilo, ambalo hutumiwa na wakazi zaidi ya 110,000 waliopo katika mji huo na vijiji vipatavyo 11 vinavyopata huduma ya chanzo hicho kinachomilikiwa na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mjini Maswa (Mauwasa).

Dk. Shekalaghe alisema hayo jana katika kijiji cha Zanzui wakati wa ziara yake ya kushuhudia nyavu na sumu zilizokamatwa na Mauwasa kandokando ya bwawa hilo, baada ya wavuvi hao kukimbia.

Alisema kuendelea kuwapo kwa vitendo hivyo kunatokana na usimamizi dhaifu licha ya bwawa hilo kulindwa kwa muda wa saa 24 na Kampuni ya Ulinzi ya Maziku Seneta ya mjini Maswa.

Alisema baadhi ya wavuvi waliopo kwenye vijiji hivyo katika Kata ya Zanzui wanadaiwa kuvua kwa kutumia sumu za mimea kwa lengo la kuua samaki.

"Hawa wavuvi waliokimbia na kutelekeza nyavu na sumu hii iliyoko kwenye makopo na dumu hili lita tano... na tumebaini kuwa ni sumu inayomwagwa kwenye maji kwa ajili ya kuua samaki ni ile ya mimea inayojulikana kwa jina la Thiodan (R) 4EC inayotengenezwa viwandani, na hii ni hatari kwa maisha ya binadamu na viumbe hai wanaotumia maji haya hasa kwa matumizi ya kunywa," alisema.

Alisema kuwa bwawa hilo limekuwa likilindwa na kuzuia shughuli za kilimo kufanyika ndani yake lakini cha kushangaza sasa wavuvi haramu wa kutumia sumu wameingia na jukumu la usalama wa bwawa hili uko chini ya Mauwasa.

Naye Mkurugenzi wa Kampuni ya Ulinzi ya Maziku Seneta, Mussa Maziku, alisema wavuvi hao hufanya kazi hiyo nyakati za usiku kuanzia saa nane mpaka saa tisa na wanashindwa kudhibiti kutokana na eneo la bwawa kuwa kubwa, hivyo kuomba msaada wa serikali.

Alisema kuwa wapo baadhi ya viongozi wa kisiasa katika eneo hilo wamekuwa wanahamasisha wananchi kufanya vitendo hivyo na vingine kama kuchungia mifugo na kufanya shughuli za kilimo katika eneo la bwawa, na wanapowakamata hupigiwa kelele za kuomba msaada na kisha askari wao huanza kushambuliwa na wananchi kwa silaha za jadi.

Awali Kaimu Mhandisi wa Mauwasa, Mhandisi Nandi Mathias, alisema kuwa shughuli za uvuvi haziruhusiwi katika bwawa hilo, na waligundua kufanyika kwa uvuvi huo haramu walipokuwa kwenye ukaguzi wao wa kawaida wa bwawa hilo, ndipo walipotoa taarifa kwa Jeshi la Polisi wilayani humo na kufanikiwa kukamata nyavu na sumu hiyo.




Wasichana waliokimbia ukeketaji na kulelewa katika kituo cha nyumba salama cha Mugumu, wilayani Serengeti, mkoani Mara, kinachomilikiwa na Shirika lisilo la kiserikali la Hope for Girls and Women Tanzania, wakiwa wenye furaha baada ya Shirika la Misaada la Marekani USAID Tanzania, kukabidhi msaada wa gari katika kituo hicho, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## WRATZ yabaini kilio wanawake, wasichana

**Na Elizabeth Zaya**

MUUNGANO wa Utepe mweupe wa Uzazi Salama (WRATZ), umesema katika kampeni iliyofanywa na wadau 359 kutoka katika nchi 114 duniani ikiwamo Tanzania, walibaini kilio kikubwa cha wanawake na wasichana wanataka huduma bora za afya ya uzazi katika vituo vya afya.

Mratibu wa Muungano wa Utepe Mweupe, Rosemary Mlay, alisema kampeni hiyo ilifanyika mwaka 2018 na lengo lake ni kufahamu mahitaji makubwa ya wanawake katika huduma za afya.

Mlay alisema katika kampeni hiyo wanawake na wasichana walisema wanataka dawa na vifaa tiba vipatikane kwa urahisi na haraka katika vituo vyote vya afya.

Pia, alisema walitaka damu salama itolewe bure hususani kwa wanawake wanaojifungua na upatikanaji wa vifaa na vitendea kazi vingine vya kujifungulia uwe rahisi zaidi.

"Wanawake wanataka pia huduma za uzazi wenye heshima na utu, huduma rafiki na watoa huduma wenye adabu, huduma zilizoboreshwa, ustawi na afya ya uzazi na afya kwa ujumla, kuongezwa vituo vya afya vinavyofanya kazi kwa ukamilifu na viwe karibu na kinamama na wasichana," alisema Mlay na kuongeza:

"Pia wanahitaji ushauri nasaha na ufahamu kuhusu afya ya uzazi na afya kwa ujumla, wanataka taarifa zitolewe kuhusu uchungu na kujifungua, kuwapo watoa huduma wakati wote, huduma na vifaa vya kuzalishia, kuongezwe watoa huduma wenye stadi , kuwapo na mazingira mazuri ya kazi kwa watoa huduma."

Pia Mlay alisema katika kampeni hiyo, wanawake walipendekeza upatikanaji wa majisafi na salama kila wakati katika vituo vyote vya afya, vitanda vya kutosha pamoja na shuka na godoro.

"Kwa kipindi kirefu sana tumekuwa tukipiga kelele juu ya kuhakikisha vituo vyote vya afya nchini vinatoa huduma zote za dharura za uzazi salama kwa wanawake wanaojifungua, ikiwamo upatikanaji wa vifaa vya kujifungulia, damu salama, wataalamu wenye weledi. Jambo hili limefanyiwa kazi japokuwa tunahitaji kuendelea kuboresha zaidi," alisema Mlay.

## Mil. 300/- za FAWCO kutokomeza ukatili kwa wanawake, wasichana

**Na Sabato Kasika**

SHIRIKA la Kimataifa la Wanawake la FAWCO Foundation, linaloundwa na wajumbe kutoka nchi za Ulaya, limeridhia kutoa fedha zaidi ya Sh. milioni 300 kutokomeza ukatili kwa wanawake na wasichana na ndoa za utotoni mkoani Mara.

FAWCO Foundation, ambayo husaidia mashirika yanayotekeleza miradi ya kijamii duniani, imeahidi kutoa fedha hizo zitakazotumika kutekeleza mradi huo mkoani humo kuanzia Juni mwaka huu hadi Juni 2022.

Hatua hiyo imefikiwa baada ya shirika lisilo la kiserikali la Hope for Girls and Women Tanzania kutangazwa mshindi kwa kupata kura zaidi ya 85 za wajumbe wa FAWCO, kati ya mashirika 15 toka mataifa mbalimbali kwa kukidhi vigezo kwa kuonyesha kikamilifu kazi ambazo limekuwa likifanya za kupambana na ukeketaji, ndoa za utotoni na kupigania haki za wanawake kwa kushirikiana na wadau mbalimbali na serikali wilayani Serengeti.

Mkurugenzi wa Hope for Girls and Women Tanzania, Rhobi Samwelly, aliliambia gazeti hili jana kuwa hiyo ni hatua nzuri ya kuendelea kupambana na vitendo vya ukatili Serengeti na Mara kwa ujumla.

"Shirika letu limetangaza kwa njia ya 'Video Confrence Zoom' kutokea Jimbo la Loxembourg nchini Ubelgiji juzi katika mkutano ambao pia niliufuatilia, ambapo msimamizi wa mradi huo utakaotekelezwa Mkoa wa Mara, Tharien Van Eck kutoka FAWCO Foundation alisema mradi huo utaleta mabadiliko kwa jamii," alisema Rhobi.

Rhobi alisema shirika lake limekidhi vigezo na kuonekana linapigania jambo jema linalohusu afya za mabinti na usawa kwa wanawake na kwamba FAWCO nalo linapigania kuhakikisha maisha ya kinamama na afya zao vinakuwa salama.

"FAWCO wanajua madhara ya ukeketaji kwamba ni mabaya kiafya, unachangia magonjwa ikiwamo Ukimwi, festula na kuwaathiri kisaikolojia wasichana hasa wanaokeketwa kwa lazima," alisema.

Alisema kwenye baadhi ya nchi zinazokeketa, shirika hilo limekuwa likisaidia mapambano hayo, na kwamba limeamua kufadhili kiasi hicho cha fedha liendeleze mapambano dhidi ya mila potofu kwa miaka miwili.

Mkurugenzi huyo alisema, wanataka kuhakikisha vitendo vya ukatili vinakwisha kwa kutoa elimu ili watoto wasikeketwe wala kuolewa wakiwa na umri mdogo, na kuitaka jamii kutoa ushirikiano mradi huo utakapoanza.

## HABARI KIMATAIFA

## Watu 402 waambukizwa virusi vya corona

**JOHANNESBURG,** Afrika Kusini

AFRIKA Kusini inaendelea kukumbwa na maambukizi ya virusi vya ugonjwa hatari wa corona ambao Shirika la Afya Duniani (WHO) liliutaja kuwa ni janga la kimataifa.

Hadi kufikia jana idadi ya wananchi walioambulizwa ugonjwa huo walikuwa 402.

Wakazi wa Afrika Kusini, moja ya nchi zinazoendelea kuwa na matukio mengi ya maambukizi ya virusi vya ugonjwa huo barani Afrika, wana hofu kuwa idadi ya maambukizi huenda ikaongezeka na kuenea katika maeneo mbalimbali ya nchi.

Wasafiri kutoka mataifa ya Ulaya na mataifa mengine ndio wanaripotiwa kuwa wengi kuambukizwa virusi vya ugonjwa huo nchini Afrika Kusini, ingawa idadi ya maambukizi ya ndani pia inaongezeka.

Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Wizara ya Afya zaidi ya nusu ya matukio yanayotokea Afrika Kusini vimepatikana katika Jimbo la Gauteng, linalolijumuisha Jiji la Johannesburg, ambalo ni kubwa kabisa nchini humo lenye idadi ya watu milioni 5.7, na mji mkuu Pretoria ambao una watu milioni 2.4. **RFI**

## Wagonjwa wa corona Uganda, Rwanda waongezeka

**KAMPALA,** Uganda

IDADI ya wagonjwa wa virusi vya corona katika nchi za Afrika Mashariki za Uganda na Rwanda imepaa kwa kasi huku nchi hizo zikipambana kuzuia maambukizi zaidi.

Hadi kufikia jana usiku Uganda walitangaza wagonjwa wapya nane na kufikisha idadi ya wagonjwa tisa.

Wagonjwa hao wapya wanane wote ni raia wa Uganda ambao wamerejea nchini humo kutokea Dubai kati ya Machi 20 na 22, mwaka huu.

Waziri wa Afya wa Uganda, Jane Ruth Aceng, alisema kuwa kufikia sasa nchi hiyo imebaini wasafiri 2,661 wakiwamo raia wa nchi hiyo ambao wanaweza kuwa na hatari ya kusambaza maambukizi na watu hao wapo chini ya uangalizi maaalumu.

"Kati ya hao, watu 1,356 wanafuatiliwa kwa ukaribu; watu 774 wapo karantini kwenye maeneo maalumu yaliyotengwa huku 582 wakijitenga wenyewe kwa kujiweka karantini," alisema Aceng.

Kwa mujibu wa waziri huyo wasafiri 1,305 tayari wameshamaliza kipindi cha siku 14 za kujitenga na kufuatiliwa hali zao.

Mgonjwa wa kwanza wa virusi hivyo anaelezwa kuendelea vizuri katika hospitali ya Entebbe.

Wagonjwa wapya wa virusi vya corona 17 wametangazwa jana usiku nchini Rwanda na kufanya idadi ya maambukizi nchini humo kufikia watu 36. **BBC**

# China yaruhusu wakazi wake kutoka majumbani

**BEIJING,** China

WAKATI nchi nyingi duniani zikifunga mipaka yao hususani viwanja vya ndege kwa hofu ya kusambaa kwa virusi vya ugonjwa wa corona, China imewatangazia wakazi wa Jimbo la Hubei kutoka majumbani baada ya kujifungia kwa miezi miwili.

Jimbo la Hubei ndiko ambako mlipuko wa virusi vya ugonjwa wa corona ulianzia mwishoni mwa mwaka jana, utawaruhusu wakazi ambao wako kwenye hali nzuri kiafya kusafiri kuanzia jana usiku, miezi miwili baada ya kuamliwa kukaa majumbani mwao.

**Jimbo la Hubei ndiko ambako mlipuko wa virusi vya ugonjwa wa corona ulianzia mwishoni mwa mwaka jana.**

Ugonjwa wa virusi vya corona uligundulika mwaka jana nchini China katika Jiji la Wuhan lililopo Jimbo la Hubei na kupewa jina la COVID-19, umeshasambaa katika nchi zaidi ya 110 duniani na kusababisha vifo 14,300 huku 320,000 wakiambukizwa.

Lakini katika taarifa iliyotolewa jana na serikali ya China ilieleza kuondoa vikwazo vya usafiri katika eneo ambalo lilikuwa kitovu cha janga la virusi hivyo ambalo ni Hubei.

Hatua hiyo ya kuondoa zuio hilo, ambayo haitatekelezwa katika Jiji la Wuhan ambao ndio ulioathirika zaidi hadi Aprili 8, inakuja wakati Uingereza na New Zealand zikiungana na mataifa ya Ulaya, Mashariki ya Kati, Amerika Kaskazini na Asia katika kutangaza hatua ya watu kubakia majumbani katika jitihada za kupunguza maambukizi mapya. **DW**



Maofisa wa Jeshi la Polisi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) wakiwa katika doria katika mitaa ya Jiji la Goma wakivalia barakoa (Mask) kwa kujilinda na maambukizi ya ugonjwa wa virusi vya corona. **PICHA: REUTERS**

# Malawi kufanya uchaguzi marudio Julai 2

**LILONGWE,** Malawi

UCHAGUZI wa urais nchini Malawi unatarajiwa kurudiwa tena Julai 2, mwaka huu kwa amri iliyotolewa na mahakama ya juu nchini humo.

Hatua hiyo imekuja baada ya matokeo ya uchaguzi huo uliofanyika mwaka jana kufutwa kufuatia udanganyifu uliotolewa.

"Kufuatia maamuzi ya mahakama ya katiba ya Februari 3, yaliyofuta matokeo ya uchaguzi wa urais na kuagiza kufanyika uchaguzi mpya, kwa sababu ya dosari tunatangaza kwamba chaguzi zitafanyika Julai 2," alisema mwenyekiti wa tume hiyo Jane Ansah wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Katika maamuzi ya kwanza kabisa kuwahi kufikiwa nchini humo, mahakama ilibatilisha matokeo ya uchaguzi uliofanyika Mei 2, mwaka jana na kumrejesha madarakani kwa awamu ya pili Rais Peter Mutharika.

Katika tamko hilo, Mahakama ilieleza kuwa matokeo ya uchaguzi kwa kiasi kikubwa yaligubikwa na udanganyifu hususani matumizi makubwa ya wino mweupe wa masahihisho kwenye karatasi za kupigia kura.

Hivyo, iliagiza kufanyika kwa chaguzi mpya katika kipindi cha siku 150, lakini Mutharika alikata rufani maamuzi hayo. Rufani yake hiyo itasikilizwa na mahakama ya juu zaidi kuanzia Aprili 15.

Rais Mutharika hadi sasa bado hajakubali kusaini mapendekezo kuhusu mabadiliko ya sheria ya uchaguzi yanayotaka mtu kupata wingi wa zaidi za asilimia 50 ili kuingia mamlakani kwa awamu ya pili.

Mapendekezo hayo ni kizingiti kikubwa kwa Mutharika, ambaye alitangazwa mshindi kwa ushindi wa asilimia 35.8 tu ya kura.

Ansah, amesema iwapo rais atagoma kuyaridhia mapendekezo hayo ya sheria mpya kabla ya siku ya uchaguzi, basi tume ya uchaguzi italazimika kuandaa uchaguzi chini ya sheria zilizopo.

Ili kujiwekea mazingira mazuri zaidi kwenye uchaguzi unaokuja, pande kuu mbili zinazopingana wiki iliyopita zilisaini makubaliano baina yao kuelekea kwenye uchaguzi huo.

Chama cha upinzani cha Malawi Congress, MCP pamoja na United Transformation Front, UTM walisaini makubaliano ya kuungana kwenye uchaguzi huo katika hafla iliyohudhuriwa na maelfu ya wafuasi wao katika mji mkuu, Lilongwe.

Kwa upande wa Mutharika na chama chake cha Democratic Progressive mapema mwezi huu waliungana na chama kidogo cha upinzani cha United Democratic Front, kilichoshika nafasi ya nne kwenye uchaguzi wa mwaka jana.

Taifa hilo la kusini mwa Afrika bado halijaorodhesha kisa hata kimoja cha COVID.19, lakini kuna wasiwasi kwamba kusambaa kwa virusi vya maradhi hayo vya corona kunaweza kutishia kucheleweshwa zaidi kwa uchaguzi huo.

Hii ni mara ya kwanza kwa matokeo ya uchaguzi wa urais kupingwa kisheria nchini Malawi tangu taifa hilo lilipopata uhuru mwaka 1964. **DW**

# Udhibiti corona mabasi daladala changamoto

**Na Maulid Mmbaga**

KUFUATIA mlipuko wa ugonjwa wa homa ya mapafu unaosababishwa na virusi vya corona, changamoto ya kujikinga imeibuka kwa watumiaji wa usafiri wa mabasi ya daladala.

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alitangaza kusitishwa kwa muda baadhi ya huduma za kijamii na kutoa agizo kwa wamiliki wa magari ya abiria kuhakikisha kila mtu anakaa kwenye kiti.

Hata hivyo, wanaoendesha vyombo hivyo jijini Dar es Salaam, wameonekana kujaza watu kupita kiasi hali inayoweza kusababisha maambukizi kuwapata watu wengi.

Akizungumza na mwandishi wa habari hizi, kondakta wa daladala inayofanya safari kutoka Gongolamboto kwenda Mawasiliano, aliyetambulisha kwa jina moja la Alli (28), alisema wanajitahidi kujikinga na corona katika shughuli zao za kila siku, lakini kutokana na changamoto ya usafiri ndio sababu wanabeba abiria wengi.

"Shida ya usafiri ndiyo inayosababisha abiria kulazimika kupanda kwenye gari hata pale wanapoona siti zote zimeshakaliwa, na sisi tunatafuta pesa na bosi jioni anataka hesabu yake ya siku, na ukilinganisha hali ngumu ya maisha ya sasa hatuwezi kuwazuia," alisema Alli.

Mmoja wa abiria aliyeongea na Nipashe, Blandina Hassani (32), alisema sababu ya watu wengi kulazimika kujazana kwenye vyombo vya usafiri ni mazoea ya kila siku kwa sababu mabasi ni machache na watu ni wengi.

Alisema kipindi ugonjwa huo haujaingia, adha ya usafiri ilikuwapo hasa wakati wa asubuhi na kwamba hata kipindi cha tishio hilo abiria wanalazimika kuendelea kujazana ili kwenda kwenye shughuli za kutafuta kipato.

"Kila mtu anataka kuwahi kazini na kwa wale walio ajiriwa ikitokea umechelewa kazini bosi inakua ngumu kukuelewa kuwa kunashida ya usafiri," alisema.




Abiria wakinawa mikono ili kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona, kabla ya kupanda mabasi ya kwenda Chalinze, katika stendi ya Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Waganga wa kienyeji waonywa kurubuni wagonjwa kifua kikuu

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAGANGA wa kienyeji mkoani Shinyanga, wameonywa kukaa na wagonjwa wa kifua kikuu kwa madai ya kuwatibu na kutakiwa kuwaruhusu kwenda hospitali wakapate tiba.

Mhudumu wa afya katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga, anayehusika kutoa dawa kwa wagonjwa wa kifua kikuu, Deborah Mpanduji, alitoa tahadhari hiyo wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema waganga wa kienyeji hawana tiba ya kifua kikuu, bali hospitali pekee na kuwataka waganga hao waache tabia hiyo na kuwasalimisha hospitali.

"Naomba waganga wa kienyeji waache tabia ya kurubuni wagonjwa wa kifua kikuu kuwa wanaweza kuwatibu, bali wawaache waje kutibiwa hapa hospitali ndio kwenye tiba sahihi," alisema Mpanduji.

"Wagonjwa hapa hospitali tunawapata kupitia kwa wahamasishaji wetu, ambao wanawaibua huko vijijini kwa waganga wa kienyeji, na tatizo hili linaonekana kuwa kubwa waganga hawa kujifanya wanayo tiba," alisema.

Kaimu Mratibu wa Kifua Kikuu na Ukoma Mkoa wa Shinyanga, Dk. Peter Mlacha, alisema kati ya watu 100,000 wenye ugonjwa wa kifua kikuu ni 161, huku uwezo wa ugunduzi kwa watu wenye TB ukiwa ni asilimia 43, kwa mwaka 2018 vilishuhudiwa vifo 16 sawa na asilimia 4.5 ikiwa juu ya ile ya taifa asilimia nne.

Alisema zaidi ya asilimia 50 ya wagonjwa waliogundulika kuwa na kifua kikuu mkoani humo, wanatoka migodini, viwandani, pamoja na maeneo yenye msongamano wa watu, na yale yaliyo karibu na barabara kuu, huku wilaya ya Kahama ikiongoza kwa kuwa na wagonjwa wengi ikifuatiwa na Shinyanga Vijijini.

Pia, mwaka 2018 matokeo ya wagonjwa waliotibiwa wakapona ni asilimia 93, wakati malengo ya taifa yalikuwa asilimia 90, pia mwaka huo waliweka malengo ya kupata na kuwatambua wagonjwa 3,254, lakini walipata 2,431, huku mwaka 2019 waliweka lengo la kuwafikia wagonjwa 3,349, na kuwapata 2,885 sawa na asilimia 86.

Mmoja wa wagonjwa waliofika hospitali ya Mkoa wa Shinyanga kufanya vipimo vya kifua kikuu, Maria Nkwambi, alisema kwa miezi miwili sasa amekuwa akisumbuliwa na kifua, kukohoa, kifua kubana, mwili kutoa jasho na kuchemka, baada ya hali kuzidi aliamua kufika hospitalini hapo kufanya vipimo na sasa anasubiri majibu, huku akiwashauri watu kujenga utamaduni wa kupima kuliko kukimbilia dawa za kienyeji.

# Tanesco yaomba radhi kisa kukatika umeme

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

SHIRIKA la Umeme Tanzania (Tanesco) mkoani Shinyanga, limeomba radhi wateja wake kutokana na kukatika kwa umeme mara kwa mara.

Umeme umekuwa ukikatika majira ya jioni na kuwasababishia usumbufu.

Aliyeomba radhi jana ni Ofisa Uhusiano na Huduma kwa Wateja, kutoka Mkoa wa Shinyanga, Sarah Libogoma, wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema Shirika hilo linaomba radhi kwa usumbufu uliojitokeza kwa kukatika katika kwa umeme, na kubainisha tatizo hilo liliitokana na hitilafu kwenye miundombinu ya njia ya kusafirisha umeme kutoka kidatu kwenda Iringa, ambapo mto Ruaha ulijaa maji na kusababisha nyaya za umeme kugusa maji.

"Shirika la Umeme Tanzania Tanesco Mkoa wa Shinyanga, tunaomba radhi sana wateja wetu kutokana na tatizo la kukatika katika kwa umeme kwa siku tano, ambapo kwenye njia zetu za kusafirisha umeme zinazopita kando ya mto Ruaha zilipata hitilafu sababu ya maji kujaa na kugusa nyaya za umeme," alisema Libogoma.

"Tatizo hili halitajitokeza tena, kwa sababu mafundi wetu wameshalifanyia kazi, na sisi Tanesco mkoani Shinyanga tutaendelea koboresha huduma kwa wateja wetu pamoja na kuondoa nguzo za umeme ambazo zimeshachakaa, na kukata miti ambayo ipo karibu na nyaya za umeme," aliongeza.

Aidha, alisema kutokana na kukatika kwa umeme, hakuna taarifa yoyote iliyotolewa ya madhara kwa wananchi, huku akitoa wito pale watakapoona kuna tatizo la umeme watoe taarifa mapema, pamoja na kutunza miundombinu ya Shirika na kutoiharibu.

Jackson Mapolu, mkazi wa Ndala, alisema umeme umekuwa ukikatika saa moja na nusu jioni na kurudi saa tatu usiku, hivyo kuwa kero kwao, ikiwamo kukosa kuangalia taarifa ya habari saa 2 usiku.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA /MASHAMBA

**VIWANJA VINAUZWA,** Headline block ya viwanja vine inauzwa, Viko mbweni mpiji karibu na Shule ya Sekondari Mpiji . Eneo zaidi ya heka moja ) 4220 Sq mt . Viwanja Surveyed. Simu: 0711 506758 0787 445506, 0679 041220

## ELIMU/ MASOMO

**REGISTRATION OPPORTUNITIES**

**KELAND NURSERY AND PRIMARY SCHOOL** located at salasala announces registration opportunities for Nursery and Primary School students. Call: 0713 327613.


*NIPASHE NI JIBU LAKO*

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


## KUPOTEA KWA CHETI



**CLARA ELINAWINGA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.212/0021 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MACHAME GIRL'S SEKONDARI mwaka 1996.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: DAR/STA/RB/256347/2020.

115678702

## KUPOTEA KWA CHETI



**ALEX NGOWI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia LYAMUNGO SEKONDARI mwaka 1996.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Control No: 991081206014 4.

115678602

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FOMU II**

**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya MOSHI MJINI**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 36/2020**

**Ombi la MARIANA EUGENE MALALE kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu EUGENE MICHAEL MALALE**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 15/04/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo .

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 24/3/2020.

HAKIMU ANAYEHUSIKA

SAHIHI YA HAKIMU

115679302

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA KONDOA**

**MAOMBI NA 11 YA MWAKA 2020**

**NMB BANK……………….MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

1. **SAIDI OMARY NKUSA**
2. **T/A PAHI STATIONARY AND BOOKSHOP………WAJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**KWA: SAIDI OMARY NKUSA NA T/A PAHI STATIONARIES AND BOOKSHOP**

Fahamu kwamba shauri hili limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 3/04/2020 saa 3:00 asubuhi, mbele ya Mh. O. MBEGA Mwenyekiti wa Baraza. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Kumbukumbu zote za kesi zinazohitajika zinapatikana Baraza la Ardhi la Wilaya Kondoa. AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu nakiri, Muhuri wa Baraza hili leo tarehe **13 Mwezi 03, 2020.**

MH. O. MBEGA
MWENYEKITI WA BARAZA LA ARDHI
WILAYA YA KONDOA

215679402


*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe

www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII



**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# MATA AELEZEA NAFASI YAKE MAN UNITED




**MANCHESTER,** England

JUAN Mata ameelezea nafasi yake muhimu ndani ya vyumba vya kubadilishi nguo vya Manchester United, huku kiungo huyo mkongwe akiwakaribisha wachezaji wapya na vijana kwenye kikosi cha kwanza.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 ni mmoja wa wachezaji wenye umri mkubwa zaidi pale Old Trafford, na anaamini kwamba ana uwezo wa kuwa mfano kwa wachezaji wa United katika kuijenga timu ya muda mrefu.

Mata pia anaamini kocha Ole Gunnar Solskjaer anathamini mchango wake katika kuwasaidia wachezaji wapya kuimarika, huku kiungo huyo bado akitajwa kwamba ataendelea kubakia hapo kwenye kikosi hicho chenye njaa ya mataji.

Mchezaji huyo wa zamani wa Chelsea alisaini mkataba mpya na United kipindi cha majira ya joto kilichopita, sasa yupo klabuni hapo kwa mwaka wa sita.

Mata ameiambia televisheni ya Manchester United: "Najihisi kijana, kiukweli kwenye mwili wangu na akili. Lakini nimekuwa nacheza katika klabu za Uingereza kwa miaka 12, 13 sasa.

"Hivyo hili linanipa mimi uzoefu mkubwa hasa wakati tunapokabiliwa na hali ngumu, kuwapa ushauri wachezaji vijana namna ya kupambana na hali hiyo. Nafikiri yeye (Solskjaer) anathamini hilo pia.

"Mimi kama mchezaji, ninachoweza kukifanya ni kujitoa zaidi dimbani, lakini pia kufanya kila linalowezekana nje ya uwanja na kuwashauri wachezaji kama Bruno (Fernandes) na Odion (Igahlo) na wachezaji vijana wanaotoka kwenye akademi yetu kama (Williams), Chongy (Tahith Chong), Angel (Gomes) na Jimmy (Garner).

# Maldini, mwanawe kupona corona ndani ya wiki

**MILAN,** Italia

PAULO Maldini anatarajia kupona virusi vya corona "ndani ya wiki" baada ya kubainika ameambukiza na kuthibitishwa na Milan wikendi iliyopita.

Gwiji huyo wa zamani wa timu ya taifa ya Italia, Maldini, ambaye sasa anafanya kazi pale Rossoneri kama mkurugenzi wa ufundi, alibainika kuwa na virusi vya COVID-19 pamoja na mtoto wake wa kiume mwenye umri wa miaka 18, Daniel, ambaye kwa sasa ni mchezaji wa Milan.

Taarifa ya klabu iliyotolewa Jumamosi ilibainisha kwamba wote wawili wamemaliza wiki mbili ya kujitenga nyumbani na watabakia karantini hadi watakapopona kabisa.

Maldini aliposti video kwenye ukurasa wake wa Instagram akishukuru kwa wale wote waliomtakia heri ya kupona haraka.

"Kwa video hiyo nataka kuwashukuru wale wote waliooneshwa kuguswa kwao na hali yangu mimi na kijana wangu kwenye mitandao ya kijamii, nawapenda sana na asanteni," alisema.

"Tupo vizuri. Tunapona kabisa ndani ya wiki moja. Asante kwa kuendelea kututakia heri ya kupona.






# *Barca kumpa msimu mmoja zaidi Dembele*

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA imeripotiwa kwamba, itampa msimu mmoja zaidi Ousmane Dembele ili kuthibitisha thamani yake baada ya kuwa na misimu mitatu ya majanga pale klabuni.

Dembele amekuwa akikumbwa na majeruhi tangu alipotua pale Nou Camp kipindi cha majira ya joto mwaka 2017 kwa ada iliyoripotiwa kuwa ni pauni milioni 135 kutoka kule Borussia Dortmund.

Wakati huo winga huyo wa kimataifa wa Ufaransa alikuwa akitajwa kama mmoja wa wachezaji vijana bora zaidi wanaochipukia barani Ulaya.

Ripoti za miezi ya hivi karibuni zimebainisha kwamba, Barca inaona mfumo mbovu wa chakula wa Dembele ndio sababu ya kukabiliwa na majeruhi ya mara kwa mara kwa kipindi cha misimu mitatu.

Lakini licha ya madai hayo, benchi la ufundi la Barca linaonekea kuamua kuwa na uvumilivu nae, huku gazeti la Diario Sport likiripoti kwamba wanampa nafasi moja nyingine.

Kocha wa Barca, Quique Setien anaonekana kuvutiwa zaidi na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 na anaamini kwamba kipaji chake kinaweza kumfanya aendelea kucheza nchini Hispania.

Dembele aliumia wakati Barcelona ikicheza na Borussia Dortmund kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya Novemba mwaka jana, majeraha ambayo yalitarajiwa atakaa nje ya dimba kwa miezi miwili.

Licha ya kukumbwa na majeraha ya mara kwa mara, Dembele katika msimu wake wa tatu amefunga mabao 19 na kutengeneza asisti 17 katika mechi 74 alizochezea klabu hiyo.

HABARI MICHEZO

# Hleb: Messi na Ronaldo njooni mcheze soka Belarus

**MINSK,** Belarus

LIONEL Messi na Cristiano Ronaldo wanaweza kuhamia kucheza kwenye Ligi Kuu ya soka ya nchini Belarus kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, ametania mchezaji wa zamani wa Arsenal na Barcelona, Alexander Hleb.

Virusi vya COVID-19 vinavyosababishwa corona vimesabisha ligi nyingi duniani kusimamishwa kuanzia Ligi Kuu ya England, Serie A, LaLiga, Bundesliga na Ligue 1, huku Euro 2020 na Copa America 2020 imesogezwa mbele kwa mwaka mmoja.

Hata hivyo, nchini Belarus msimu wa Ligi Kuu unaendelea kama kawaida ukiwa umeanza Alhamisi, huku mashabiki wakiruhusiwa kuhudhuria viwanjani.

Hleb alijaribua kupaza sauti kwa mamlaka za Belarus kusimamishwa ligi hiyo, lakini hakuna aliyejali na sasa amewatania nyota wa Barcelona, Messi na mkali wa Juventus, Ronaldo kwenda kucheza huko.

"Dunia nzima kwa sasa inaangalia Ligi Kuu ya Belarus. Kila mmoja anatakiwa kwenda kwenye televisheni na kutuangalia sisi," alisema Hleb akiliambia gazeti la The Sun.

"Wakati Ligi Kuu ya mpira wa makongo ya Marekani ilipositamishwa, wachezaji wengi walikwenda Urusi kucheza. Pengine Lionel Messi na Cristiano Ronaldo waweza kuja Belarus kuendelea na ligi. Unajua?

"Ni sehemu pekee Ulaya unaweza kucheza soka. Angalau watu wa Belarus watakuwa na furaha."




# CHELSEA YAJIPANGA KUMSAJILI CHILWELL




**LONDON,** England

CHELSEA wanaamini wanaweza kumsajili beki wa kushoto wa Leicester na timu ya taifa ya England, Ben Chilwell kipindi cha majira ya joto, lakini watalazimika kulipa ada kubwa ili kumchukua.

Blues hao wamevutiwa na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 na kocha Frank Lampard ameelezea kwamba nafasi ya beki ya kushoto inahitaji kuimarishwa.

Mtandao wa Goal umedai kuwa Chelsea wanaongoza kwenye mbio za kumuwania 'dogo' huyo kipindi cha majira ya joto, lakini Leicester hawatamuuza kwa bei rahisi.

Ripoti zimebainisha kwamba, Leicester wanataka pauni milioni 80 kwa ajili ya kumuachia Chilwell, bei sawa na ile iliyolipwa na Manchester United wakati wanamsajili Harry Maguire kipindi cha majira ya joto kilichopita.

Leicester haina presha ya kumuuza Chilwell kwa sababu pia wana nafasi ya kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Leicester wapo juu ya Chelsea kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya England, lakini Blues hao wanapigania kuhakikisha Chilwell anatua pale Stamford Bridge.

Lampard kwa sasa anasaka beki wa kushoto mpya kwani anajua kwamba eneo hilo linahitaji maboresho zaidi.

Marcos Alonso na Emerson Palmieri ndio wanaocheza nafasi ya beki ya kushoto kwa Chelsea na wote wanaonekana kama wataondoka mwishoni mwa msimu huu.

# *Man kumsajili Ighalo kwa pauni mil. 15*

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United ipo tayari kumsajili Odion Ighalo hadi kwa pauni milioni 15 kipindi cha majira ya joto kijacho baada ya mkataba wake wa dharura wa mkopo wa mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Nigeria utakapomalizika Mei 31, mwaka huu.

Gazeti la Daily Mail limebainisha kwamba mkataba wa muda mfupi wa Ighalo kutoka Shanghai Shenhua unatarajia kumalizika mapema zaidi kwa mwezi mmoja kuliko mikataba mingine ya mkopo.

United inaweza kufanya makubaliano ya kumwongezea mkataba na klabu hiyo ya Ligi Kuu ya China kuanzia Aprili hadi Juni, ingawa umoja wa chama cha wachezaji wa kulipwa duniani, FIFPro, unaangalia suluhisho kwa kile kilichosababisha na mlipuko wa virusi vya corona.

Miamba hao wa Old Trafford wapo tayari kumsajili Ighalo kwa mkataba wa kudumu baada ya mshambuliaji huyo wa zamani wa Watford kufunga mabao manne katika mechi zake nane za mwanzo.

Shanghai wanajiandaa kumuuza Ighalo na wameweka thamani yake kuwa ni pauni milioni 15, mchezaji huyo ambaye atafikisha umri wa miaka 31 Juni mwaka huu.

Hawakutaka na kuomba ada ya mkopo Januari kwa sababu United ilikubali kuchangia mshahara wa Ighalo kwa pauni 130,000 kati ya pauni 300,000 anazolipwa kwa wiki.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ARTETA: NIMEPONA KABISA CORONA

## Wachezaji Arsenal waendelea kujitenga, asimulia alivyojisikia baada ya kubainika...

**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta amesema amepona kabisa corona (COVID-19) baada ya kusumbuliwa na virusi hivyo kwa takriban wiki mbili sasa.

**Mhispania huyo, Arteta mwenye umri wa miaka 37, alikuwa kocha wa kwanza Ligi Kuu England kukutwa na maambukizi ya virusi vya corona Machi 12, mwaka huu.**

Aliripotiwa kutojisikia vizuri baada ya Machi 10, mwaka huu kuthibitika mmiliki wa Olympiakos ya Ugiriki, Evangelos Marinakis, klabu ambayo ilicheza na Arsenal kwenye mechi ya Europa League Februari, kubainika ana maambukizi ya virusi vya corona.

Arteta alisema: "Ilinichukua siku tatu ama nne kuanza kujisikia vizuri, na kuwa na nguvu zaidi, kuziacha dalili nyuma."

Akizungumza na chaneli ya Televisheni ya Hispania, La Sexta, aliongeza: "Nipo vizuri sana kwa sasa. Ninajisikia kuwa nimepona."

Wachezaji wa Arsenal waliripotiwa kutakiwa kuanza mazoezi jana, baada ya kumaliza siku 14 za kujitenga kufuatia Arteta kubainika kuwa na corona, lakini kurejea kwao kuliahirishwa.

"Kama matokeo ya hali ya sasa, sisi ni wazi kuwa itakuwa haifai na kutowajibika kuwataka wachezaji kurejea kwa wakati huu," klabu hiyo ya kaskazini mwa London ilieleza katika taarifa yake. "Kwa hiyo kikosi chetu cha kwanza cha timu ya wanaume, wanawake na cha makinda wote wataendelea kubaki nyumbani. Wabaki nyumbani na kuokoa maisha."

Wachezaji wachache wa Arsenal wamekuwa wakijitenga binafsi baada ya taarifa ya Marinakis kukutwa na maambukizi, wakati 'Gunners' ilitakakiwa kuvaana na Manchester City katika Uwanja wa Etihad Machi 11, mwaka huu.

Akizungumza Jumapili, Arteta aliongeza: "Nilipokea simu kutoka kwa bodi ya wakurugenzi baada ya mazoezi wakati nilipokuwa ndani ya gari langu na waliniambia rais wa Olympiakos alikutwa na maambukizi chanya, na kila mmoja aliyegusana naye alikuwa hatarini.

"Niliendelea kuwaeleza kuwa sijisikii vizuri na kwamba tulikuwa na hali hiyo kwa sababu wachezaji wengi waligusana nao.

"Tulikuwa na mechi dhidi ya Manchester City siku iliyofuata na ni wazi hatukuweza kuwaweka watu wengi hatarini pasipo kusema chochote.

"Ni wazi wote waliogusana na mimi walipaswa kwenda kujitenga, na kwa sababu hiyo michezo ilipaswa kuahirishwa."

## ZISIKUPITE

### CHELSEA YAMTAKA RICE

CHELSEA inavutiwa kumsajili kiungo mkabaji wa West Ham na England, Declan Rice, 21, majira haya ya joto. ***(Sky Sports)***

### ANUKIA JUMLA NEWCASTLE

NEWCASTLE inatumai itakuwa tayari kumsajili jumla beki wa pembeni wa England, Danny Rose, 29, anayeichezea klabu hiyo kwa mkopo akitokea Tottenham wakati soko la usajili la majira ya joto litakapofunguliwa tena. ***(I Sport)***

### ARSENAL KUMFUATA EDOUARD

ARSENAL inataka kumsajili mshambuliaji wa Celtic, Odsonne Edouard, 22, katika majira ya joto wakati huu ikipanga kujijenga kuelekea msimu ujao. ***(Mirror)***

### MOURINHO ASAIDIA WAZEE

KOCHA wa Tottenham, Jose Mourinho amekuwa akisaidia wakati wa milipuko wa virusi vya corona kwa kugawa vyakula jamii ya wanachama wazee waliopo karibu na uwanja wa mazoezi wa Spurs huko Enfield. ***(Football.London)***

### UNITED YAACHIWA JUDE

MANCHESTER United imepewa nguvu ya kumsajili kiungo wa Birmingham, Jude Bellingham kufuatia Borussia Dortmund kuachana na mipango hiyo ya kuisaka saini ya nyota huyo raia wa England mwenye umri wa miaka 16. ***(Mirror)***

### ALABA KUITOSA MAN CITY

BEKI wa Bayern Munich na Austria, David Alaba, 27, atakataa kusajiliwa na Manchester City majira haya ya joto ili kutoa nafasi ya kujiunga na ama Real Madrid au Barcelona. ***(Bild, via Sports Mole)***

### EPL KUHAMISHWA LONDON

MECHI za soka zinaweza kuchezwa nje ya London wakati michezo itakaporuhusiwa kurejea tena kwa sababu ya idadi kubwa ya maambukizi ya virusi vya corona. ***(Telegraph)***

### OSIMHEN AONGOZA UNITED

MSHAMBULIAJI wa Lille na Nigeria, Victor Osimhen, 21, amekuwa 'kipaumbele' cha kwanza kusajiliwa na Manchester United katika dirisha la usajili lijalo. ***(Le10 Sport, via Star)***

### SANDRO AIVUTIA MAN CITY

MANCHESTER City inavutiwa kumsajili kiungo wa Brescia na Italia, Sandro Tonali, 19. ***(Corriere dello Sport, via Sport Witness)***

### SPURS YAMGEUKIA EZE

TOTTENHAM inavutiwa kumsajili kiungo wa QPR, Muingereza Eberechi Eze, 21, ingawa Crystal Palace na Sheffield United, ambao walikuwa na nia ya kuinasa saini ya mchezaji huyo hazipo tayari kulipa pauni milioni 20 ambazo QPR inataka. ***(Express)***

### MMAREKANI AITAKA DERBY

BILIONEA wa Kimarekani, Michael Dell, 55, ambaye anasemekana kuwa na utajiri wa pauni bilioni 26.9, anajadili kuhusu uwekezaji wake katika klabu ya Daraja la Kwanza ya Derby County. ***(NBC Sports)***

HABARI MICHEZO

## MZFA: Alliance FC, Mbao mjitathmini

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

CHAMA cha Soka Mkoa wa Mwanza (MZFA), kimezitaka timu zote za mpira wa miguu zinazoshiriki ligi mbalimbali mkoani humo kuhakikisha zinafanya tathmini katika ushiriki wao wa ligi ikiwamo Ligi Kuu Tanzania Bara jambo ambalo linaweza kuzinusuru na janga la kushuka daraja.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Mwanza jana, Katibu Mkuu wa MZFA, Leonard Malongo, alisema baadhi ya klabu hapa nchini hazipo katika nafasi katika ushiriki wao wa ligi, hivyo ni muhimu kufanya tathmini kwa muda huu wakati ligi zikiwa zimesimama kutokana na hofu ya kuenea kwa virusi vya corona.

Alisema timu za mkoani hapa ambazo zinashiriki Ligi Kuu, Alliance FC na Mbao FC, zipo katika hali mbaya kutokana na kutokuwa katika nafasi nzuri, hivyo bila jitihada za kufanya tathmini ya kina na kurekebisha kasoro zilizojitokeza hali itaweza kuwa mbaya zaidi.

## Corona yatibua kalenda BAZA

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

CHAMA cha Mpira wa Kikapu Zanzibar (BAZA), kimesema ni vigumu kuendelea kufuata kalenda yake ya mwaka huu kutokana na kutokea mlipuko wa virusi vya corona unaotikisa dunia kwa sasa na kusababisha kusimama kwa shughuli zote za michezo.

Akizungumza na gazeti hili Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Rashid Hamza Khamis, alisema kutokana na kupokea agizo kutoka serikalini kupitia Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar (BTMZ), la kusitisha shughuli zote za michezo katika kipindi hiki, hali hiyo imeathiri kalenda yao kwa mwaka huu.

Alisema miongoni mwa mambo ambayo yaliyomo katika kalenda yao ni pamoja na Ligi Kuu Zanzibar ambayo ilikuwa ukingoni mwa msimu, kushiriki Ligi ya Muungano iliyopangwa kufanyika Tanzania Bara Aprili 20, mwaka huu, pamoja na michuano ya Kombe la Karume iliyopangwa kufanyika baada ya Ligi ya Muungano.

# NAMUNGO FC YAZIBEBA TIMU RUANGWA KUPITIA SPORTPESA

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya michezo ya Kubashiri Matokeo ya SportPesa Tanzania, imesema kufanya vizuri kwa Namungo FC kwenye msimu huu wa Ligi Kuu Bara ndiko kumewavutia wao kumwaga vifaa vya michezo Ruangwa mkoani Lindi.

SportPesa wiki iliyopita ilikuwapo mkoani humo kwa ziara fupi ya ugawaji vifaa vya michezo kutoka klabu za Uingereza ambazo kampuni hizo zinazidhamini kupitia Kampeni yake ya Kits for Afrika.

Katika ziara yao hiyo, SportPesa iliwagawia vifaa hivyo timu nane za Ruangwa ikiwamo mipira ya kisasa na yenye ubora inayotumiwa na klabu hizo kubwa baadhi zikiwa ni Hull City na Everton.

**Akikabidhi vifaa hivyo, Mkurugenzi wa Uwekezaji na Udhibiti wa SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas, alisema hawajutii udhamini walioutoa kwa Namungo ambayo kwa sasa ipo nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara.**

Tarimba alisema Namungo inastaili pongezi nyingi kutokana na kupanda kucheza Ligi Kuu msimu huu na kufanya vizuri na hiyo ni kutokana na ubora wa timu hiyo.

"Ninaitabiria Namungo kufanya vizuri zaidi katika misimu mingine ijayo, kama imeweza kuwa katika nafasi nne za juu ikiwa ni msimu wa kwanza tangu ilipopanda.

"Hivyo hatujutii udhamini huu tulioutoa kwa Namungo kutokana na kutuwakilisha vema kwenye ligi kwa nafasi waliyopo kwenye msimamo.

"Namungo imetushawishi kuja kutoa msaada wa vifaa vya michezo kwa timu nyingine zinazoshiriki ligi mbalimbali, lengo likiwa ni kuona zinapatikana timu nyingine kama ilivyokuwa Namungo hapa Ruangwa," alisema Tarimba.



Wachezaji wa timu ya Fedha FC, Abdallah Sultan (kushoto) na Masoud Rashid akimiliki mpira wakati wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Hospitali ya Kivule jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Corona yaifanya DStv kupanua wigo kwa wateja*

**Na Mwandishi Wetu**

PAMOJA na changamoto iliyopo duniani kwa sasa, MultiChoice inawahakikishia wateja wake wa DStv kuwa inazingatia mahitaji yao hasa ukizingatia kwa sasa watu wengi wanalazimika kukaa nyumbani katika jitihada za kuzuia maambukizi ya virusi vya corona (Covid-19).

Mkurugenzi Mtendaji wa MultiChoice Tanzania, Jacqueline Woiso, jana aliwaambia waandishi wa habari jijini Dar es Salaam kuwa wanaendelea kupanua wigo mpana wa habari kwa kufungua chaneli za habari kwenye vifurushi vyao.

"Tunazingatia mawasiliano ya mara kwa mara na mamlaka husika na tutashiriki kikamilifu katika kupambana na kuenea kwa ugonjwa wa Covid-19. Ni muhimu sana sote tuzingatie maelekezo na maagizo yanayotolewa na mamlaka sahihi na wataalamu wetu ili kuhakikisha kuwa tunalinda afya zetu na za wenzetu," alisema Woiso.

Mkurugenzi huyo alitangaza rasmi kwamba kuanzia jana wamefungua chaneli ya CNN (401) na Euronews (414) kwa wateja wa vifurushi vyote kuanzia kile cha chini kabisa cha DStv Bomba ikiwa ni pamoja na kufungua chaneli maarufu ya habari za Afrika Africanews (chaneli 417) kwenye vifurushi vyote hadi Mei Mosi, mwaka huu, ambapo itakuwa inapatikana kuanzia kifurushi cha DStv Family.

"Kwa kuzingatia kuwa watoto wetu wako likizo kipindi hiki, maudhui ya elimu yamezingatiwa ambapo chaneli ya elimu ya Da Vinci (Chaneli 318) na ile ya burudani ya Cartoon Network (channel 310) sasa zimefunguliwa kwa vifurushi vyote kuanzia cha chini kabisa cha DStv Bomba. Hii ni katika jitihada za kuhakikisha watoto wetu wanaendelea kupata elimu na burudani wakati huu wakiwa nyumbani.

"Kama unavyofahamu, matangazo mubashara ya michezo mbalimbali yameathiriwa kutokana na mingi sasa kusitishwa, hata hivyo ili kuhakikisha kuwa mteja hapungukiwi na burudani kipindi hiki ambacho unashauriwa kupunguza mizunguko na safari zisizo za lazima, tunakuletea makala maalum za michezo (sport documentaries) kutoka kila pembe ya dunia pamoja na kuonyesha matukio makubwa ya kimichezo yaliyotokea siku za nyuma.

"Pia chaneli maarufu ya michezo SuperSport1 (201) sasa imefunguliwa katika kifurushi cha DStv Compact na DStv Compact Plus. Chaneli hii itakuwa na matukio yaliyoweka rekodi katika ulingo wa michezo duniani. Kwa wale wapenzi wa mbio za magari wataburudika na chaneli ya SuperSport7 (207) ambayo imefunguliwa kwa vifurushi vyote," alisema.

Kuhusu huduma kwa wateja, Woiso alima wanajali afya zao na wafanyakazi wao, katika kipindi hiki cha tahadhari na kwamba wameandaa utaratibu ambapo baadhi yao watafanya kazi wakiwa nyumbani.

"Hii ina maana kuwa kunaweza kukawa na kuchelewa kupata huduma, hata hivyo tuna njia nyingi mbadala za kidijitali, kimtandao ambapo mteja anaweza kupata huduma nyingi kwa urahisi na ufanisi zaidi.

# Michezo

Jumatano Machi 25, 2020

Nipashe




Arteta: Nimepona kabisa corona UKURASA 30

SASA NIPO FITI...



Kipa wa KMC, Juma Kaseja, ambaye alifanya kazi kubwa ya kuiwezesha Taifa Stars kufuzu Fainali za CHAN zilizotarajiwa kuanza Aprili 4-25, mwaka huu nchini Cameroon kabla ya kuahirishwa. Mlindamlango huyo amepania kurejea katika kikosi cha Stars baada ya awali kuachwa kutokana na kuwa majeruhi. **PICHA: MAKTABA**

# Sadney, Balinya waishtua Yanga

## ●●● Yasema haitafanya tena makosa, Eymael aachiwa kazi ya usajili amalize mwenyewe...

**Na Saada Akida**

BAADA ya 'kubugi stepu' katika dirisha kubwa la usajili lililopita, uongozi wa klabu ya Yanga umeamua kuliacha jukumu hilo kwa Kocha Mkuu, Mbelgiji Luc Eymael ili kutafuta nyota anaoamini wanaweza kumsaidia kujenga kikosi imara msimu ujao.

**Uongozi huo umeamua kufikia hatua hiyo baada ya kukiri mwanzoni mwa msimu huu ulisajili wachezaji ambao hawakuwa msaada kwa timu yao na hatimaye kuishia kuvunja mikataba na kuondoka katikati msimu.**

Wachezaji ambao wanaonekana kuishtua Yanga na kuifanya kutotaka kurudia makosa ni washambuliaji Mganda Juma Balinya ambaye alikuwa mfungaji bora nchini Uganda na Mnamibia Sadney Urikhob, waliokuwa gumzo wakati wa usajili wao, lakini wakashindwa kuonyesha cheche Ligi Kuu Bara na kuishia kuvunja mikataba yao na kuondoka.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Fredrick Mwakalebela, alisema jukumu kubwa la usajili kwa sasa liko chini cha Eymael ambaye anafahamu wachezaji wazuri wa kuweza kusaidia timu yao.

Alisema hatua hiyo ni kutokana na uongozi kutotaka kurudia makosa ya nyuma ya kusajili wachezaji ambao hawakufikia malengo waliyotarajia.

"Hatuwezi kurudia makosa, Eymael anafanya majukumu yake na anapomuona mchezaji ambaye atakuja kusaidia timu, viongozi wanaenda kumalizana na mchezaji au klabu kama bado ana mkataba nayo," alisema Mwakalebela.

Alisema Luc amepewa jukumu hilo kwa kuwa amekuwa akifanya kazi kwa ukaribu na wachezaji wengi na Kamati ya Usajili ya Yanga haina mpango wa kumuingilia kwenye majukumu yake.

Yanga tayari imekata tamaa ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Bara, ambao inaukosa kwa msimu wa tatu mfululizo na kushuhudia watani zao, Simba wakilibeba taji hilo linalotoa nafasi ya kushiriki Ligi ya Mabingwa Afrika. Hadi sasa Simba ipo kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo, ikiwa na pointi 71 baada ya mechi 28, wakati Yanga iliyopo mchezo mmoja nyuma ipo nafasi ya tatu ikiwa na alama 51, tatu nyuma ya Azam FC katika nafasi ya pili.

Ligi hiyo kwa sasa imesimama kwa kipindi cha mwezi mmoja kutii agizo la serikali la kuepuka mikusanyiko ya watu ili kupunguza kasi ya maambukizi ya virusi vya corona vinavyoendelea kupuputisha uhai wa maelfu ya watu duniani.

Katika mapumziko hayo, klabu zimekuwa zikiyatumia 'kurusha ndoana' zao huku na kule kwa kuanza kufanya mazungumzo na wachezaji inaotaka kuwasajili katika dirisha lijalo.

# Ndayiragije amgusa Kaseja kurudi Stars

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Kocha Mkuu wa timu ya soka ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), Etienne Ndayiragije, akisema atalazimika kuita wachezaji wapya wa kuunda kikosi chake mara ratiba mpya ya michuano ya kuwania kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2021 na Fainali ya Wachezaji wa Ndani (CHAN), kipa mkongwe nchini, Juma Kaseja amepania kuwamo ndani.

Taifa Stars ilivunja kambi yake ya kujiandaa na mechi ya kufuzu Afcon na dhidi ya Tunisia pia kujiwinda na michuano ya CHAN, baada ya Shirikisho la Soka Afrika (Caf) kuahirisha mchezo na michuano hiyo kutokana na kasi ya kuenea kwa virusi vya corona (COVID-19) duniani.

Na Tayari Ndayiragije amesema atalazimika kuita kikosi chake upya kulingana na kiwango watakachoonyesha wachezaji wakati ukifika, jambo ambalo Kaseja amepania kurejea baada ya kuwa nje kwa muda mrefu akiuguza majeraha ya goti.

Kaseja alimwambia mwandishi wetu kuwa atapambana kurejesha kiwango chake baada ya kupona maumivu ya goti ili awe fiti na kurejeshwa kwenye kikosi cha Taifa Stars kwa ajili ya fainali za CHAN.

"Nitapambana, nitarejesha kiwango, na ninaamini nitakuwamo kwenye timu," alisema Kaseja ambaye ni kipa wa klabu ya KMC, baada ya kuzitumiakia pia Moro United, Simba, Yanga, Mbeya City na Kagera Sugar.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >